**31 OKTOBA, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

______

## MAJADILIANO YA BUNGE

______

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

### Kikao cha Tatu – Tarehe 31 Oktoba, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 35 la tarehe 30 Agosti, 2024;
2. Toleo Na. 36 la tarehe 06 Septemba, 2024;
3. Toleo Na. 37 la tarehe 13 Septemba, 2024;
4. Toleo Na. 38 la tarehe 20 Septemba, 2024;
5. Toleo Na. 39 la tarehe 27 Septemba, 2024;
6. Toleo Na. 40 la tarehe 04 Oktoba, 2024;
7. Toleo Na. 41 la tarehe 11 Oktoba, 2024;

8. Toleo Na. 42 la tarehe 18 Oktoba, 2024; na
9. Toleo Na. 43 la tarehe 25 Oktoba, 2024.

**SPIKA:** Ahsante sana!

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Ahsanteni sana, tutaanza na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge kutoka Mbinga Vijijini.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali kupitia Taasisi yake ya Hifadhi ya Chakula ilitoa ahadi ya kununua mahindi kwa wakulima wote nchi hii. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa bei nzuri ya mahindi lakini na mpunga na kwa kweli wananchi wa Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa, Njombe na mikoa mingine yote inayolima mpunga pamoja na mahindi wamefurahishwa sana na bei nzuri ya mazao haya, lakini hivi karibuni kumekuwa na shida kidogo, mahindi yamepokelewa lakini malipo yamechelewa kidogo na wakulima wameanza kutuuliza sisi Wabunge, lakini wanauliza Serikali ni lini sasa mahindi yale yanaenda kulipwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu hili siyo swali la kisera, lakini ni jambo ambalo linawagusa wananchi wengi, kwa hivyo nakupa fursa ulijibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imepanua wigo wa masoko ya mazao ya wakulima ikiwemo mazao haya ambayo yamekuwa kibiashara, lakini pia yamekuwa yana uhitaji mkubwa kama chakula ikiwemo mahindi, mpunga nayo pia tumeboresha masoko yake. Pamoja na kuruhusu sekta binafsi kwa maana ya wafanyabiashara kuyanunua mazao haya lakini pia Serikali tumeona umuhimu wa kuhifadhi kwenye maghala ya Kitaifa kwa ajili ya dharura, lakini pia na uhifadhi endelevu wa chakula hiki. *NFRA* tumeipa jukumu kwa niaba ya Serikali kununua mazao na inanunua karibu mikoa yote na nikiri kwamba *NFRA* walichelewa kidogo kufanya malipo kwa sababu ya taratibu za kifedha.

Mheshimiwa Spika, nashukuru swali hili limekuja kwa sababu jana, juzi tumekuwa tukikutana na Wabunge wanaotoka kwenye maeneo hayo, nimepokea jana Mheshimiwa Aida Khenani kutoka Mpanda, wewe mwenyewe unalirudisha hapa kama swali, Mheshimiwa Mwenisongole, Mbunge wa Songwe naye pia ameuliza swali hili na tumeendelea kuwahakikishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nitumie nafasi hii kuwahakikishia wakulima wote waliouzia mazao haya kupitia *NFRA*: kwanza, malipo yameshaanza kulipwa toka juzi bado kukamilisha taratibu za kifedha na wanaendelea kufanya hivyo kwa wakulima wote waliouzia *NFRA*. Kwa kweli Serikali tunawashukuru sana wakulima kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kuzalisha mazao mengi ya chakula na biashara msimu uliopita na inatuhakikishia Taifa letu kuwa na akiba ya kutosha ya chakula kupitia makusanyo yanayofanywa na *NFRA* na kuweka kwenye maghala yetu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashuhudia pia wafanyabiashara wengi wa ndani hata nje ya nchi wakiingia nchini kuja kupata mazao haya. Kwa hiyo zoezi la ununuzi kupitia *NFRA* litaendelea kwa wakulima na wale waliobaki na mahindi sasa na kama wanatafuta masoko *NFRA* itanunua na italipa malipo halali kwa wakulima wenye mazao haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nitumie nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmekuja kwetu:

Mheshimiwa Khenani; Mheshimiwa Kapinga; Mheshimiwa Mwenisongole; na wale wote ambao wanakaa kwenye maeneo haya ambako wakulima wameuza mazao haya, kwamba *NFRA* ambayo inakusanya mazao haya, kuyanunua kwa bei hii nzuri ambayo inafurahiwa na wakulima tutaendelea kuyanunua mahindi yote na tutalipa, kila mmoja atapata stahiki yake kadri ya mazao haya yalivyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu swali, pamoja na kuipongeza Serikali na hasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa namna ilivyoandaa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kukipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa namna kilivyosimamia mchakato wa kuwapata Wagombea wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2016, Serikali kupitia tamko la Waziri Mkuu hapa Bungeni ilisitisha kuanzisha maeneo mapya ya utawala hasa kwenye vijiji, vitongoji na kadhalika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini ukiangalia matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022, tuna vijiji na vitongoji ambavyo vimekua sana kiasi kwamba kusimamia maendeleo kwenye ukuaji huo mkubwa kiasi hicho inakuwa shida na hivyo hata utawala wake inakuwa tabu. Je, Serikali sasa iko tayari kupitia upya msimamo wake huo wa kuzuia kuanzishwa kwa maeneo mapya ya utawala na hivyo kusaidia kusukuma maendeleo na hasa ikizingatiwa kuwa uanzishwaji wa vitongoji na vijiji hauna gharama kubwa ukilinganisha na faida tutakayoipata ya kuruhusu kuanzishwa kwa vijiji na vitongoji vipya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sasa umejitokeza uhitaji mkubwa wa kupandisha hadhi na kutoa mamlaka za utawala

maeneo mapya ili kukidhi utoaji huduma kwa urahisi kwa wananchi wanaozungukwa na maeneo hayo. Zoezi la utoaji mamlaka lilisitishwa kwa mara ya mwisho pale ambako Serikali ilitoa vibali vya kuanzisha mamlaka kwa ngazi za za vijiji, kata, halmashauri, wilaya na mikoa. Baada ya tamko lile kazi kubwa iliyofanyika ni kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu wezeshi ili iweze kusaidia watumishi na wananchi kupata eneo la kutolea huduma. Uanzishaji huu na mahitaji haya, lakini tuliyalinganisha pia na uwepo wa rasilimali watu na rasilimali fedha ambazo zitawezesha pia kwenye utoaji huduma kwenye maeneo haya mapya.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo haya hayana gharama kubwa, lakini bado tunauhitaji wa uimarishaji wa miundombinu inayoweza kuwezesha kufika kwenye makao makuu hayo. Kwa sasa timu ya utafiti ambayo inapita kuona ukamilishaji wa miundombinu hiyo ili kuweza kutoa mapendekezo kwa mamlaka ambayo inatoa kibali cha uanzishaji mamlaka mpya, ambaye ni Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI ambaye ni Mheshimiwa Rais, watakapokamilisha ukaguzi huu na tathmini hii itakapowasilishwa wakati wowote ikimpendeza mamlaka atatoa kibali kwenye ngazi hizi zote. Tuichukue hii ambayo haina gharama kubwa kuwa ni sehemu ya mapendekezo ili kuimarisha na kufikia na kufikia hatua ya kumwezesha kutoa kibali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama kwamba hatua hizi ambazo tumezipitia za kujaribu kukusanya rasilimali fedha na rasilimali watu, tupate watendaji wa vijiji tukijua kwamba bado kuna vijiji vinahitaji watendaji wa vijiji, watendaji wa kata. Jambo hili likikamilika na timu ya tathmini ikikamilika tutarudi tena kutangaza kwenye maeneo yenye uhitaji yaweze kuomba halafu kupitia taratibu na vigezo vya kuwa mamlaka zitapitiwa na kwa hiyo halmashauri zitapata taarifa ya maeneo yote haya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, hayupo. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nia njema ya Serikali kupeleka huduma kwa wananchi, Serikali yetu imekuwa na utaratibu wa kutoa na kuchukua maeneo kwa lengo la kuboresha au kuimarisha miundombinu ikiwemo Barabara, viwanja vya ndege, ujenzi wa kambi za jeshi na vitu kama hivyo. Mfano wa maeneo haya kwa uchache ni kama vile ujenzi na upanuzi wa kiwanja cha ndege kule Nachingwea, Kilwa Masoko, lakini pia kule Segerea kuna changamoto kama hiyo, lakini hata barabara ya Ifakara – Kidatu ina changamoto kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni pale ambapo Serikali inawasitisha wananchi kutoendeleza maeneo hayo mpaka pale taratibu za fidia zitakapokamilika, lakini kutokana na hali hii wananchi wamekuwa wakipata adha na shida kubwa. Je, sasa Serikali haioni ipo sababu ya kurejea upya utaratibu huu na badala yake wananchi waruhusiwe kuendeleza na kutumia maeneo yao na tathmini ifanyike mara tu pale ambapo fedha zitapatikana ili kuondokana na adha hii ambayo wananchi wanaipata? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli yako maeneo yanatwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu wezeshi kulingana na malengo ya taasisi inayotaka eneo hilo. Uchukuaji huu una sheria zinazoongoza endapo eneo linalotakiwa linakaliwa na watu, linatumika kama sehemu ya kilimo na yoyote iwe taasisi ya umma au taasisi binafsi inapohitaji ni lazima ilipe fidia, fidia hii

itamwezesha yule ambaye anafidiwa kuondoka eneo na kupisha ujenzi wa miundombinu hiyo wezeshi.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa ziko sheria ambazo zinaongoza pia taratibu zote hizi ikiwemo na kipindi au ukomo wa ukamilishaji wa fidia hiyo. Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua kwa nini Serikali isione uwezekano wa kuruhusu hawa wananchi waliofanyiwa tathmini kuendelea kuwekeza kwenye maeneo hayo. Kama tutaruhusu njia hiyo basi gharama za fidia zitakuwa zimepanda maradufu, lakini muhimu zaidi ni kwamba taasisi yoyote inayohitaji kuwekeza mahali ambako wananchi wanaishi, pamelimwa, ni lazima ijipange kabla ya zoezi hilo kuwa ina bajeti ya kuweza kufidia eneo hilo ili kuondoa usumbufu ambao si lazima kwa wale ambao wanafidiwa halafu wanakaa muda mrefu, hawafanyi maendelezo yoyote kwa sababu tu wamesitishwa na hakuna malipo na wala hakuna taarifa zozote na taasisi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe wito kwa taasisi zote, ziwe za umma au sekta binafsi pale ambako mnafikiria kuanzisha mradi na mradi huo unagusa maeneo ya wananchi ni lazima wajipange kwanza kibajeti kabla hawajaenda kufanya tathmini, ili wanapokwenda kufanya tathmini ukishapata gharama unalipa mara moja na wanachi wanaokaa kwenye eneo hilo waweze kupisha kwenda eneo lingine. Kwa hiyo utaratibu huu tutauzingatia na tutahakikisha kuwa tunasimamia tathmini zote kuwa taasisi husika lazima iwe ina bajeti stahiki ili kuweza kutoa fidia na wananchi wasipate usumbufu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pato la Taifa limekua na kufikia kiasi cha trilioni 148.39 ukilinganisha na trilioni 141.25 mwaka 2022, ukuaji huu ni sawa na asilimia 5.1. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukuaji huu kwa kiasi kikubwa umechangiwa na uwekezaji uliofanywa na

Serikali kwenye sekta za huduma. Bado ukuaji na mchango wa sekta za uzalishaji una mchango mdogo sana kwenye ukuaji wa pato la Taifa. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha ushiriki mkubwa wa sekta binafsi ili kuongeza mchango wa sekta ya uzalishaji kwenye ukuaji wa pato la Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua mkakati wa Serikali wa kuongeza uzalishaji ambao unafikiriwa kuwa unaweza kusaidia kuongeza pato la Taifa. Kwa upande wa Serikali tunakiri kwamba uzalishaji mali ndiyo ambao unaweza kuleta wigo mpana wa pato la Taifa kwa sababu unagusa sekta nyingi ambazo zenyewe zina uhitaji mkubwa kwa jamii na kwa hiyo pato lake pia linaweza kuwa kubwa. Mkakati wetu moja ni kuwa na sera nzuri ya uwekezaji ambayo inatengenezewa sheria wezeshi kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji unakuwa hapo, lakini pia kanuni na taratibu ambazo zinatumika kwenye uwekezaji ili kuwawezesha wale wawekezaji wa sekta za uzalishaji kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni ile hamasa ambayo tumeendelea kuwa nayo ya uanzishaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ambavyo pia, vinasaidia katika kuongeza thamani ya mazao tunayopata, ili tuweze kuyafikia masoko. Hii inasaidia pia, kupanua wigo mpaka ngazi ya vijiji panapokuwa na viwanda vidogo ambavyo wananchi wanaweza kuvimiliki na kuongeza thamani ya mazao tuliyonayo, akiyaingiza kwenye soko, tutapata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaendelea kuimarisha pia, maboresho ya uwekezaji kwa ujumla kupitia Kituo chetu cha Uwekezaji cha Taifa ambacho chenyewe kimeainisha zile huduma muhimu ambazo zinamuwezesha mwekezaji kuweza kuwekeza na kuendesha biashara yake ya uzalishaji bila tatizo lolote. Moja ni miundombinu ya usafirishaji, barabara, reli, kwenye

maziwa na Bahari, lakini pia, hata anga. Tumeimarisha hili ili kuruhusu wawekezaji kufanya biashara na kwenda popote ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme; sasa hivi tuna umeme mwingi wa kutosha na tunatarajia kuwa na umeme mwingi zaidi tutakapokamilisha Bwawa letu la Mwalimu Julius Nyerere, ili kuruhusu uwekezaji wa aina yoyote unaohitaji umeme kuwa na umeme wa kutosha. Pia, kwenye Sekta ya Madini ambayo tunaona vijana wengi sasa wanaingia kwenye uchimbaji na tumeweka utaratibu wa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, tuna Sekta ya Kilimo ambayo ndiyo inazalisha malighafi na maeneo mengine ambayo tunaendelea kuyaratibu na kuhakikisha kwamba tunapanua wigo wa uzalishaji kwa lengo hilo hilo la kuwa na pato kubwa ndani ya Serikali. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mpango Mkakati wa Serikali tuliouweka unaogusa maeneo yote haya sasa unawawezesha Watanzania, kila mwenye nia ya dhati, kuingia kwenye ujasiriamali wa uzalishaji kupitia mpango huu mkakati wa sheria na kuimarisha utoaji huduma. Sasa tuna fursa nzuri ya Watanzania kuzalisha na kupata pato kubwa la kutosha kupitia biashara hizo na sisi tutapata pato vilevile.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kusimamia kupitia kituo chetu cha uwekezaji kuhakikisha kwamba, uwekezaji mkubwa tunaupata. Juzi tu tulikuwa na Taifa la Urusi, lilikuja nchini, linaonesha nia ya kutaka kuwekeza. Tumewahakikishia kwamba, Tanzania ni nchi iliyowekwa kimkakati na Mwenyezi Mungu, leo hii Nchi nane jirani zinaitegemea Tanzania; Kenya, Uganda, Congo, Rwanda, Burundi, Zambia, Malawi na Msumbiji na pia, tuna Nchi mbili kama Comoro na Sudani Kusini zinategemea Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hii ni fursa kwetu Watanzania kuzalisha zaidi na kuingiza kwenye masoko bidhaa zetu. Tuna uhakika wa soko la ndani, watu milioni 61 *plus*, lakini pia, Afrika Mashariki na nchi zote ambazo zinaitegemea nchi hii. Huo ndiyo mpango wa Serikali ambao tunausimamia kwa sasa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa, suala la afya ya akili ni jambo la msingi sana katika ustawi wa binadamu yeyote, ambalo husaidia binadamu kujitambua kupambana na changamoto na kutoa mchango chanya kwenye jamii anayoishi, lakini pia, inamsaidia yeye kuweza kuzalisha kwa faida.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, suala hili lisiposhughulikiwa kwa wakati, linaleta madhara mengi katika jamii ikiwepo ulevi unaokithiri, mtu kufikiria tofauti na binadamu anavyofikiria, mwanamke kujiona mwanaume na mwanaume kujiona mwanamke na kutaka kuchukua majukumu ya kibaiolojia ambayo hayamhusu. Ikiwa ni pamoja na masuala ya kujiingiza kwenye vitendo vya ujambazi na kufikiri kwamba, huwezi kutajirika kwa kufanya kazi, kwa kutumia akili, labda ukatumie kiungo cha binadamu mwingine na hii imeleta madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali yetu mwaka 2008 kupitia Bunge lako Tukufu iliona kuna sababu ya kuanzisha sheria na tulitunga Sheria ya kusimamia Masuala ya Afya ya Akili Nchini. Kifungu cha 31(1)(b) kilitaka Serikali kuunda Baraza la Afya ya Akili Nchini ambalo litakuwa na jukumu la kusimamia muundo ambao utaratibu sekta mbalimbali za kitaaluma na kiutendaji, ili kuweza kushughulikia ufanisi wa suala la afya ya akili nchini na kutengeneza *scheme*, kwa ajili ya kuajiri wataalam watakaoshughulika na masuala ya afya ya akili nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halijafanyika mpaka leo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini kauli ya Serikali au msimamo wa Serikali ili tuweze kuwa na baraza hili na wananchi wa Tanzania waweze kupata huduma za afya ya akili, ili waweze kunufaika na kuwa vizuri katika nchi yao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Msambatavangu, Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Iringa, aah! Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, samahani sana.

Mheshimiwa Spika, namtambua Mheshimiwa Jesca, kwa muda mrefu ndani ya Bunge amekuwa kinara kwenye eneo hili la afya ya akili akiishauri Serikali namna bora ya kuweza kulishughulikia, ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, toka alipoanza kulisemea na kuishauri Serikali, Serikali imeliangalia hili kama suala mtambuka, lakini Serikali ilishaanza mchakato wa kuanzisha baraza. Tumeendelea kupokea ushauri wa Mheshimiwa Jesca kuhakikisha kuwa tunaimarisha uundaji wa baraza hili haraka sana, ili liweze kufanya kazi. Kwa hiyo, mpango wa Serikali ni kukamilisha taratibu zote za uundaji wa baraza, ili lianze kufanya kazi. Tutakapokamilisha utaratibu huu, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kwa kuwa, wewe umekuwa kinara wa jambo hili la afya ya akili, tutakushirikisha sana kuhakikisha kwamba, tunaweka mpangokazi na namna ya kutekeleza kwenye ajenda hii ya afya ya akili. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mujibu wa Mwongozo wa Fedha kwa Sheria za Serikali za Mitaa, 20% ya mapato ya ndani zinapaswa kurudi kwenye Serikali za vijiji, kwa ajili ya maendeleo mbalimbali ya wananchi. Kumekuwa na tabia ya halmashauri nyingi kutokurejesha fedha hizo kwa wananchi. Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa halmashauri ambazo hazifuati takwa hilo la kisheria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uko mwongozo, ni kweli, unaozitaka halmashauri kutenga fedha. Iko 20% kwa halmashauri za wilaya, lakini pia mwongozo unazitaka halmashauri za manispaa kutenga 40% kulingana na ukubwa wa pato lao, lakini pia, hata majiji kwa 60%.

Mheshimiwa Spika, zote hizi zimepewa mamlaka ya Mabaraza ya Madiwani kwenye halmashauri hizo kupanga mpango wa kupeleka na kujenga miundombinu ya maendeleo kwenye maeneo yao. Tunatambua ziko halmashauri katika nyakati kadhaa zimekuwa hazitekelezi na hii tumeipata pia, kutoka kwenye Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Serikali ya Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatua ambazo zinatakiwa zichukuliwe, moja, tumeyapa mamlaka Mabaraza yenyewe ya Halmashauri ambayo ndiyo yanakusanya. Yanapanga matumizi yake ukiwemo mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI wa kutenga kiwango cha fedha kulingana na ukubwa wa halmashauri, ziende zikafanye kazi za maendeleo kwenye halmashauri yake. Kwa hiyo, Baraza la Madiwani lenyewe linayo mamlaka hayo na ndiyo ambalo linapaswa kuchukua hatua ya awali.

Mheshimiwa Spika, Katibu Tawala wa Mkoa atasimamia hatua hizi zikichukuliwa baada ya kupata taarifa kwenye mkoa wake kwa halmashauri ambazo hazijatekeleza mwongozo huu na maagizo haya, lakini pia, hata Wizara nayo inapofanya uhakiki wa utekelezaji wa miradi, inapopata taarifa ya halmashauri A kutotekeleza bado inayo nafasi ya kuchukua hatua. Kwa hiyo uchukuaji hatua unaanzia kwenye Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Spika, ninataka kutumia nafasi hii kuyaagiza Mabaraza ya Madiwani na pia, Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa kuhakikisha kuwa, wanasimamia halmashauri zote kwenye mkoa zitenge fedha hizi 20%, 40% mpaka 60% kulingana na ukubwa wa

halmashauri, ili ziende kutekeleza miradi ya maendeleo vijijini. Pia, naiagiza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inapofanya ufuatiliaji, ijiridhishe, moja kati ya ajenda ni kufuatilia upelekwaji wa fedha za maendeleo zilizotokana na mapato ya ndani ya halmashauri, ili wananchi waweze kupata maendeleo wanayohitaji, ili Waheshimiwa Madiwani na wao mapendekezo yao yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sisi tunapofanya ziara huko, tutafuatilia kama kunakuwa na halmashauri ambayo haijafanya utekelezaji huo, tunataka kujua sababu ni nini. Pale ambapo wanatutolea sababu ambazo haziridhishi tutachukua hatua kali dhidi ya halmashauri na watendaji ambao hawakutekeleza maagizo ya Baraza la Madiwani. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, swali lake litaulizwa, kwa niaba yake na Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 38

**Ujenzi wa Stendi ya Kisasa – Jiji la Arusha**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Stendi ya Kisasa katika Jiji la Arusha kupitia Mradi wa *TACTIC*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa katika Jiji la Arusha eneo la *Bondeni City* utatekelezwa kupitia mradi wa Uboreshaji Miundombinu ya Miji *''Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC)"* ambao unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Ujenzi wa stendi hii unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 24.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na usanifu wa kimazingira katika eneo la *Bondeni City*. Zabuni ya ujenzi wa stendi hii ilitangazwa tarehe 19 Januari, 2024 kupitia mfumo wa *NeST* na hatua iliyofikiwa ni ya upekuzi *(Due Diligence)* kwa makandarasi waliopendekezwa ili zabuni itolewe kwa mkandarasi atakayekidhi vigezo kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mpango uliopo tathmini ya mradi imefanyika na kukamilika Julai, 2024. Hatua ya kusaini mkataba itafanyika na ujenzi unatarajiwa kuanza ifikapo Januari, 2025. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naipongeza Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo kwa tathmini ambayo imefanyika, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, inajenga stendi kwenye Jiji la Arusha ambalo tunalitegemea kwenye Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza. Mheshimiwa Gambo anauliza ni lini Serikali, kwa sababu, ni miezi tisa imepita toka tenda itangazwe na tathmini zifanyike, itasaini mkataba huu, ili wananchi wa Arusha wawe na matumaini kwamba, stendi inaenda kujengwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni la wananchi wa Makete. Sisi wananchi wa Makete tunafahamu kwamba, tuna Barabara ya kutoka Njombe – Makete imefungua sana Jimbo la Makete kwa maana kwamba, tunahitaji stendi. Je, ipi kauli ya Serikali kuhusu kujenga stendi kwenye Mji wa Makete, pale Makete? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba, kuna uhitaji mkubwa wa stendi ya kisasa katika Jiji la Arusha eneo la *Bondeni City* na tayari Serikali imeshatangaza zabuni na imeshapata makandarasi ambao waliomba. Hatua iliyopo sasa ni ya kufanya uhakiki kwa maana ya *due diligence*. Naomba tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini kwamba, mpango wa Serikali ni kuanza ujenzi mapema iwezekanavyo Januari, 2025 na mkataba utasainiwa wakati wowote kati ya Novemba na Disemba, mwaka huu 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Makete, naomba kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu. Tumeshafanya ziara katika eneo la stendi ya Makete na wewe kama Mheshimiwa Mbunge umekuwa ukiwasemea wananchi wa Makete mara kwa mara kuhusiana na uhitaji wa stendi hiyo. Natumia nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Makete kuandaa andiko rasmi la maombi ya fedha, kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo, ili tuweze kuona namna ya kuweka kwenye bajeti ya mapato ya ndani, lakini pia, bajeti ya Serikali Kuu, kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya Makete. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Wilaya ya Mwanga ilishapeleka andiko maalum TAMISEMI, kwa ajili ya ujenzi wa stendi, likapokelewa na hati ya kumiliki ardhi imeshawasilishwa na halmashauri tayari imeshaandaa uwanja, kwa ajili ya kazi hiyo. Je, ni lini ujenzi wa stendi ya Mwanga utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Halmashauri ya Mwanga ilishawasilisha andiko la ombi la kujenga stendi katika eneo la Mwanga na tayari lilishawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Upembuzi yakinifu umekwishafanyika na ombi hilo limekwishawasilishwa Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kutafuta fedha, kwa ajili ya mradi huo. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge Tadayo kwamba, mara fedha hizi zikishapatikana tutahakikisha tunazipeleka, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ukipewa nafasi ya kuuliza swali, nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Miradi ya *TACTIC* katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, soko kuu, stendi kuu na barabara itaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Miradi ya *TACTIC* iko katika makundi matatu, kuna kundi la awamu ya kwanza *(Tier 1)*, kuna kundi la awamu ya pili na kundi la awamu ya tatu. Namhakikishia Mbunge kwamba, kundi la awamu ya kwanza tayari tumeshaanza utekelezaji, kundi la awamu ya pili zabuni zimeanza kutangazwa na kundi la awamu ya tatu zabuni zitaanza kutangazwa mapema Disemba, mwaka huu 2024. kwa hiyo, Halmashauri ya Mji wa Ifakara ni miongoni mwa miji ambayo tayari taratibu za utangazaji wa zabuni zinaendelea na wakati wowote tutaanza utekelezaji wa mradi ule mwaka ujao 2025. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga stendi za mabasi Nyegezi pamoja na Nyamongoro

katika Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela, lakini stendi zile hazitumiki kama inavyopaswa kutokana na wenye mabasi kutozingatia utaratibu wa kituo cha kuanzia. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na matumizi ya stendi hizo mbili? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ujenzi wa stendi katika miji yetu una dhamira ya kusogeza huduma kwa wananchi, lakini pia kuboresha huduma hizo kwa wananchi. Ni maelekezo ya Serikali kwamba, stendi zinapojengwa ni lazima zitumike ipasavyo. Maeneo ambayo yanatakiwa kutumika, kwa ajili ya *parking* ya mabasi itumike, lakini pia, maeneo ambayo yatakuwa kwa ajili ya huduma nyingine yatumike kama mpango wa stendi ulivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuwasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri za Jiji la Mwanza kwa maana ya Nyamagana, Ilemela, Manispaa na halmashauri nyingine zote kote nchini, kuhakikisha wanazingatia na kusimamia matumizi sahihi ya stendi zote kwa kadri ya mpango ili wananchi waweze kupata huduma bora kama inavyotarajiwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ni lini ujenzi wa stendi ya Manispaa ya Shinyanga utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Manispaa ya Shinyanga ni moja ya manispaa ambazo ziko kwenye mpango wa *TACTIC* na mipango hii ya *TACTIC* inaendelea kutekelezwa. Nakuhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, awamu ya Manispaa ya Shinyanga itakapofika tutahakikisha pia, stendi hiyo inajengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na haya naona wote mlikuwa mnajiuliza kusimama. Mheshimiwa Minza Mjika.

Na. 39

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Hunyari – Bunda**

**MHE. MINZA S. MJIKA K.n.y. MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Afya Hunyari utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kituo cha Afya Hunyari kilipokea shilingi milioni 500 kutoka Serikali Kuu na kujenga jengo la kutolea huduma za nje, jengo la maabara, jengo la wazazi na jengo la kufulia, ambapo majengo haya yamekamilika na yanatumika. Aidha, ujenzi wa jengo la upasuaji upo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmmshaurri ya Bunda itatenga shilingi milioni 60 katika mwaka wa fedha 2025/2026, kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la upasuaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali linalofuata la kwanza; je, ni lini sasa jengo hilo litakamilika kwa sababu, wananchi wa kata hiyo wanahangaika sana. Matibabu ni shida wanaenda mpaka hospitali ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kituo cha Zagayu ambacho kiko Wilayani Itilima hakina jengo la maabara; je, ni lini Serikali itajenga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba, katika Kituo hiki cha Afya cha Hunyari bado jengo la upasuaji halijakamilika, liko takribani 85% ya utekelezaji na kiasi cha shilingi 60,000,000/= zinahitajika kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa jengo hili kukamilika mapema na ndiyo maana katika mwaka ujao wa fedha, tutatenga shilingi milioni 60 ili mapema robo ya kwanza ya mwaka wa fedha ujao jengo hili likamilike kwa ajili ya kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa Hunyali.

Mheshimiwa Spika, pili, zahanati ya Zagayo katika Halmashauri ya Itilima ni kweli haina jengo la maabara na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum mara kwa mara wamekuwa wakifuatilia na tayari tumeweka kwenye mpango kwa ajili ya kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo la maabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zakaria Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya Murray katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu kama ilivyoahidiwa na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Charles Mahera?  Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mpango wa kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika Kata zetu. Nimwombe tu Mheshimiwa Zacharia kwamba, kwa sababu hiyo ni ahadi iliyotolewa maana yake

inakidhi vigezo, tunaendelea na taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kwenda kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kiponzero ambacho kipo katika Jimbo la Kalenga kina majengo lakini kuna eneo ambalo watu huwa wanawahudumia wagonjwa ni chakavu sana. Ni lini Serikali itakwenda kujenga na kuwapelekea gari la wagonjwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza vituo vyote vya afya ambavyo vina majengo chakavu, Serikali imeshaandaa mpango mkakati wa ukarabati wa vituo hivyo kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba, Kituo cha Afya cha Kiponzero ni moja ya vituo ambavyo ni vikongwe na tutahakikisha kwamba tunakarabati majengo ambayo ni chakavu na yanahitaji kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imekwishapeleka magari ya wagonjwa zaidi ya 562 ndani ya mwaka mmoja, ikiwemo katika Halmashauri ya Iringa Vijijini na Jimbo la Kalenga limepata, tutaendelea kupeleka magari kwa sababu tuna uhakika kwamba bado hayatoshelezi kwa kadri ambavyo yataendelea kununuliwa tutapeleka pia katika Halmashauri hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha shilingi milioni 250 kwa ajili ya Kituo cha Afya Gidas Jimbo la Babati Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Gidas katika Halmashauri ya Babati na Jimbo la Babati Vijijini ilipelekewa shilingi milioni 250 katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na ni kituo ambacho kimeingizwa kwenye mpango wa vituo 14 ambavyo vinahitaji kupewa milioni 250 kwa ajili ya ukamilishaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya Kiloleni Wilaya ya Busega hakina wodi za kulaza wagonjwa; je, ni lini Serikali itajenga wodi hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Kituo cha Afya cha Kiloleni bado hakina wodi za kulaza wagonjwa, lakini hiyo inaenda sambamba na vituo vya afya vingi ambavyo vimejengwa kwa awamu ya kwanza. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, ujenzi wa vituo hivi vya afya unakwenda kwa awamu. Tulianza na majengo ya awamu ya kwanza, majengo matano yamekamilika tunatoa huduma, tutakwenda na awamu ya pili kwa ajili ya kujenga wodi na baadhi ya miundombinu muhimu ili vituo hivyo vifanye kazi ipasavyo ikiwemo Kituo cha Afya cha Kiloleni. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mbunge nimekuona lakini umesimama baadaye sana, kwa hiyo inabidi hii ikupite.

Tunaendelea na Wizara ya ya Nishati, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Umeme Jazilishi Maeneo ya Miji yenye Sura ya Vijiji**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, lini ahadi ya umeme jazilishi itatekelezwa kwenye Miji yenye sura za Vijiji kama Ugele, Mosi, Cargrielo, Machinjio, Ulonge, Mtalagala na Msisina?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kupeleka umeme katika maeneo ya vijijini yakiwemo maeneo ya miji yenye sura za vijiji. Aidha, kwa maeneo ya Ugele, Mosi, Cargrielo, Machinjio, Ulonge, Mtalagala na Msisina yaliyopo katika Jimbo la Iringa Mjini, Serikali itayapelekea umeme kupitia mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 15 kwa kila Jimbo kwa maeneo ya Ugele, Mosi, Ulonge, Mtalagala na Msisina. Aidha, maeneo ya Cargoelo na Machinjio yatapatiwa umeme na *TANESCO* kupitia miradi yake ya ndani ya kusogeza miundombinu ya umeme kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nishukuru kwamba, umeme umeendelea kwenda na *TANESCO* wameshapeleka maeneo ambayo Serikali imeshasema, kwa hiyo nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine ilikuwa tunaomba sana, tumejitahidi sana *TANESCO* wametusaidia sana kutoa majiko ya gesi, lakini tulisahau watu wenye ulemavu waliopo ndani ya Manispaa ya Iringa. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri kama anaweza kutupatia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa moyo wake mzuri wa kuwakumbuka watu wenye ulemavu, nimepokea ombi lake na nitalifanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itaanza kupeleka umeme mkubwa kwenye vitongoji ambavyo havijapitiwa na umeme mkubwa na hivyo kuvifanya vikose sifa ya kuwemo kwenye miradi yoyote ya maendeleo ya kupeleka umeme vijijini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye mradi huu wa vitongoji 15 kwa kila Jimbo, ni mradi jazilizi. Unapeleka umeme kwenye vitongoji ambavyo tayari kuna miundombinu. Kuanzia mwezi Desemba, mwaka huu tunakuja na mradi mwingine wa vitongoji ambao utahusisha kujenga *MV-Line* na *LV-Line* na kwenye mradi huu tumeboresha zaidi na tutakuwa na transfoma zenye ukubwa wa *kVA* 50, 100 na 200 kulingana na ukubwa wa kitongoji.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, maeneo ya vitongoji ambayo hayajanufaika na mradi yatanufaika na mradi unaokuja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Uhitaji wa Geti la Kuingia Watalii Wilayani Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka Geti la kuingia Watalii kwenye hifadhi ya Mwalimu Nyerere kwa upande wa Wilaya ya Liwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa shughuli za utalii zinafunguka katika ukanda wa kusini, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali upande wa Kusini mwa Tanzania ikiwemo kujenga mageti, ukarabati wa viwanja vya ndege, ujenzi wa barabara ndani ya hifadhi. Aidha, ujenzi mkubwa wa miundombinu unaendelea katika eneo la Mtemere, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uwanja wa ndege, geti la kuingia watalii, nyumba za wageni na ujenzi wa malazi kwenye kambi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha miundombinu hiyo, Serikali itajielekeza katika kujenga geti la kuingia Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa upande wa Wilaya ya Liwale ili kuimarisha shughuli za utalii katika ukanda wa Liwale sambamba na kukuza uchumi wa wananchi kwani uwepo wa geti hili utavutia uwekezaji katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hivyo nitoe rai kwa wananchi wa Liwale kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuhifadhi rasilimali za nchi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia matumaini. Sambamba na uhitaji wa geti hili kwa ajili ya kuingilia watalii, vilevile tuna uhitaji mkubwa sana wa kuboresha uwanja wa ndege wa Liwale ambao huko mwanzo ulikuwa unatumika

mara nyingi sana na watu wa Hifadhi ya Mwalimu Nyerere pamoja na *Selous Game reserve*. Nataka kujua, ni lini Serikali itakwenda kuboresha uwanja huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ipo barabara ya ulinzi inayotuunganisha sisi na Wilaya ya Ulanga, Mkoa wa Morogoro inayoanzia Kijiji cha Ngapata kuelekea Ulanga. Je, nini mkakati wa Serikali wa kuboresha barabara hii, pamoja na kwamba ni barabara ya ulinzi kwa wananchi wa mikoa hii miwili waweze kunufaika nayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Serikali inaangalia kwa jicho makini sana uendelezaji wa utalii Kusini na tumeshafanya tathmini ya maeneo ya viwanja vya ndege na ndani ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere kwa upande wa Liwale kuna uwanja wa ndege eneo la Kibaoni, mikakati yetu ni kuboresha uwanja ule. Vilevile, kwenye hii barabara ya ulinzi ni barabara muhimu sana na kwa sasa tunachofanya, kuna kazi ya kukarabati barabara karibu kilomita 400 ndani ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, kwa barabara hii tulishapeleka fedha kupitia mpango wa UVIKO tukaiboresha, tulichobakiza ni kuimarisha barabara hii kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo hayapitiki wakati wa mvua tunajipanga kuweka vivuko ili barabara hii iweze kupitika wakati wote, kwa sababu shughuli ya utalii wa hija unafanyika kwa miguu, tunaweka jitihada sasa za kuweka ulinzi kuhakikisha kipindi chote ambapo wananchi watapita kwenye eneo lile wasiweze kudhuriwa na wanyama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza, moja kwa moja kwenye swali.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, ujenzi wa geti litakalotumiwa na watu maarufu au *VIP route* kuupanda Mlima Kilimanjaro katika Kijiji cha Kidia uko katika hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha tulipitisha hapa fedha karibu milioni 120. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kazi hiyo sasa ya kukarabati kwa kiwango cha changarawe barabara hii inaendelea. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, kwenye yale maeneo ya Mti Mrefu eneo lile lenye maporomoko liweze kutumika vizuri kama kivutio cha utalii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga geti katika Mbuga ya Udzungwa kwenye Kijiji cha Udekwa kwa kuwa 80% ya mbuga hii ipo Wilaya ya Kilolo, lakini hakuna geti hata moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kazi tunayofanya kupitia mradi wa *REGROW* ni kujenga miundombinu muhimu katika hifadhi hii. Mara baada ya kazi zinazoendelea sasa ikiwepo ujenzi wa viwanja vya ndege, itakapokamilika basi tutaingia kwenye awamu nyingine ya kuboresha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi. Barabara ya kuingia Hifadhi ya Tarangire kutoka Mji wa Babati yenye takribani kilometa 22, imekuwa na uhitaji mkubwa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyotembelea Mji wa Babati…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi itatujengea barabara hiyo yenye thamani ya takribani bilioni 18. Naomba nifahamu ni lini ujenzi huu utaanza kutoka Mji wa Babati kwenda kwenye Geti la Tarangire?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kumjibu Mheshimiwa Gekul swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumejielekeza kwenye ujenzi wa geti lile linaloingia Tarangire, kazi hii itakapokamilika basi tutajielekeza kwenye eneo hilo aliloliona.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Kuwahisha Pembejeo na Mbegu za Ruzuku ya Mahindi Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahisha pembejeo na mbegu za ruzuku ya mahindi kabla ya kipindi cha masika Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Katika msimu wa kilimo wa 2024/2025, Serikali inatekeleza mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora *(certified seeds)* kwa wakulima kwa kutumia

mfumo maalum wa kidigiti ili kupunguza mianya ya udanganyifu. Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu ya matumizi ya mfumo kwa wazalishaji, waagizaji na mawakala wa mbegu nchini ambapo hadi sasa Mawakala 13 wamesajiliwa katika Halmashauri ya Mbulu Vijijini kwa ajili ya kuuza mbegu za ruzuku. Mpango huu wa ruzuku unatekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara ukiwemo Mkoa wa Manyara. Pia, Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania *(TOSCI)* inaendelea kutoa lebo za udhibiti ubora kwa wazalishaji na waagizaji wa mbegu ili mbegu ziendelee kusambazwa na kuuzwa kwa wakulima katika mpango wa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mpango wa ruzuku ya mbolea imesambaza jumla ya tani 74.35 za aina mbalimbali za mbolea kwa mawakala waliopo Halmashauri ya Mbulu Vijijini kwa ajili ya msimu wa kilimo 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatey Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEY G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu na kwamba tutapelekewa ruzuku hizo. Swali la kwanza; je, mvua zimeanza kunyesha Mbulu Vijijini ni lini hizo mbegu zitapelekwa Jimbo la Mbulu Vijijini ili wananchi wakapanda na kupata mazao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nashukuru umeeleza kwamba tani 75 za mbolea zitapelekwa Mbulu. Je, ni tani ngapi za mahindi zitapelekwa Jimbo la Mbulu Vijijini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba, nimeshazungumza na watu wa *TOSCI* na wamesema ndani ya wiki moja watakuwa wamemaliza kazi zote na mbegu zitaanzwa kusambazwa kwa wakulima wote kabla ya msimu ambao umeshaanza sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upande wa mahindi, mawakala walioko Mbulu Vijijini ambao tumeshazungumza nao na ambao

wako *certified* kwa ajili ya ruzuku, wana tani zisizopungua 250 za mbegu za mahindi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, makampuni mengi hawajakamilisha taratibu za kutoa mbegu kwa namna ya ruzuku. Je, ni lini kauli ya Serikali kwa mawakala wadogo ambao mbegu zimethibitishwa kuendelea kuwahudumia wakulima mbegu wawauzie kwa bei elekezi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatey Massay ni kwamba, ndani ya wiki moja *TOSCI* watakuwa wameshamaliza shughuli hiyo na mawakala wadogo wataenda kuchukua mbegu kwa mawakala wakuu kwa ajii ya kusambaza kwa wakulima wote nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nyanda za juu kusini ndio msimu wetu wa kilimo umeanza. Ni kwa kiwango gani mbegu za ruzuku zimekwenda kwa ajili ya kuwasaidia wakulima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba usambazaji ambao *TOSCI* wanasimamia, unapelekwa kwa mawakala wote wakiwemo katika nyanda za juu kusini na ndani ya wiki hii jambo hilo litakuwa limeshakamilika. Kwa hiyo, nitampa orodha katika mikoa yote ya nyanda za juu kusini kwa kiwango ambacho kinatakiwa baada ya Bunge. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjin,i sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Kasi Ndogo ya Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Mwamkulu – Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu kasi ndogo ya Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Mwamkulu – Mpanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilianza utekelezaji wa Mradi wa Umwagiliaji Mwamkulu. Utekelezaji wa mradi huu ulisuasua katika hatua za awali kutokana na kuchelewa kwa malipo ya awali *(Advance payment)* ya mkandarasi. Kwa sasa malipo hayo yameshakamilika na kazi ya ujenzi inaendelea, na utekelezaji wake umefikia 50%.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali inayo taarifa kuwa kasi bado ni ndogo na kusuasua kwa awali kumerejea tena?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa msimu wa mvua umeanza na wananchi wanalitegemea bonde hilo kupitia skimu ya kienyeji. Je, Serikali inasema nini kwa maana ya kuwasaidia wakulima hawa wakati mradi huu bado haujaanza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwanza mkandarasi bado yupo ndani ya muda kwa sababu kukamilika kwa mradi huu unatarajiwa kukamilika kufikia mwezi Aprili, 2025. Tumeshapeleka fedha awamu hii na imeshalipwa ndani ya wiki moja iliyopita na tumeshapeleka maombi mengine

Wizara ya Fedha kwa ajili ya kumwongezea fedha ili amalize kwa wakati na hatujaongeza muda kwa ajili ya kukamilika kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hawa wakulima ambao wanaendelea kutumia, huwa mara nyingi tunawaruhusu wakati wa msimu kama huu wa mvua, maana yake wakulima waendelee kutumia, lakini bila kuathiri ile miundombinu ambayo mkandarasi anaitengeneza. Kwa hiyo, hali ilivyo kwa sasa ni hivyo na ndiyo hata hii tathmini ambayo tumeitoa, tumeifuatilia katika Jimbo lake. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze Mbunge wa Kigoma Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Mkandarasi Mshauri wa Daraja la Malagarasi Chini Kumaliza Kazi**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Mkandarasi Mshauri wa Daraja la Malagarasi Chini, Kijiji cha Ilagala atamaliza kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Lowa – Malagarasi lenye urefu wa mita 200 ambalo lipo katika Barabara ya Simbo – Ilagala – Kalya yenye urefu wa kilomita 234 imekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia ili kupata fedha kwa ajili ya ujenzi. Mara baada ya majadiliano kukamilika zabuni ya ujenzi itatangazwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri yanayotia matumaini, lakini ninaomba niulize swali moja la nyongeza. Je, ni lini Serikali inajipanga kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema kwenye jibu la msingi, barabara hii ina urefu wa kilomita 234. Kutokana na hali ya mvua ambayo imejitokeza Serikali imeona ni vyema kwanza iweze kulijenga daraja hili ambalo lilikuwa ni kikwazo kikubwa sana; na kama nilivyosema tunategemea kulijenga mapema sana. Kwa barabara hii ambayo inaambaaambaa na ziwa tulichokubaliana ni kuhakikisha kwamba maeneo yote yale korofi yaweze kujengwa kwa kiwango cha lami ama kwa zege kwanza wakati tunatafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia usanifu na baadaye iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilituahidi wakati wa Bunge la Mwezi Septemba kwamba mshauri elekezi atakuwa amesaini mkataba kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa Barabara ya Kahama – Nyang'hwale – Busisi. Je, mshauri elekezi huyo amekwishasaini mkataba huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zote za manunuzi zimeshakamilika na mhandisi mshauri ameshapatikana na mkataba huo umeshapelekwa kwa *AG* kwa ajili ya *vetting*. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama nimewaona; narejea tena nenda moja kwa moja kwenye swali bila historia,

historia, Mheshimiwa Naibu Waziri anaijua tayari. Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujua, je, ni lini Madaraja ya Kalebe na Kyanyabasa Bukoba Vijijini ambayo tuliambiwa yatajengwa hivi karibuni yataanza kujengwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kama tulivyosema kwenye taarifa ni kwamba madaraja yote ambayo yaliyopata changamoto kubwa kipindi cha mvua yatajengwa. Miongoni mwa madaraja yatakayojengwa ni pamoja na haya madaraja mawili, Daraja la Kalebe na Kyanyabasa. Hivi tunavyoongea daraja moja tayari mkandarasi amekwishasaini na lingine tuko kwenye hatua za mwisho za majadiliano. Kwa hiyo, madaraja hayo yatajengwa kwa kipindi tunachokianza sasa hivi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Daraja la Munguri ambalo linaunganisha Hanang na Kondoa litaanza kujengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, daraja hili lilikuwa limekwishakamilika kufanyiwa usanifu, lakini baada ya mvua limeongezeka takriban mara mbili. Kwa hiyo kinachofanyika sasa hivi ni kulifanyia usanifu upya ili liweze kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya Mbande – Msongola itakamilika?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la msingi linahusu madaraja, sasa naona tukimwona Mheshimiwa Naibu Waziri wa

Ujenzi hapa tunataka kumuuliza maswali yote. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali la Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, mkandarasi yuko *site* na kwa kweli nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pengine kama kuna changamoto itakuwa ni kumsukuma na kumsimamia ili kipande hicho kiweze kukamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, imetoa *commitment* ya kuanza ujenzi wa Barabara ya Kolandoto kwenda Kishapu yenye urefu wa kilomita 63 kwa kiwango cha lami; na kilomita 20 ndizo zitakazoanza katika ujenzi wa mwaka huu. Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi huu? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tuliahidi kuanza kujenga kwa awamu na kibali kimekwishatolewa. Kwa hiyo taratibu zitakazofuata ni kuanza kuandaa zabuni, *I mean* makabrasha ya zabuni ya ujenzi kwa ile ahadi ambayo tumeitoa kwenye kitabu chetu cha bajeti. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilikusudia kujenga Barabara ya Masasi – Nachingwea kwa kiwango cha lami na mkandarasi aliyepatikana hakufanya kazi hiyo na Serikali ilitoa ahadi kwamba inatafuta fedha. Je, fedha hizo zimekwishapatikana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii aliyoitaja ni kweli kwamba tulikuwa tumeahidi kuijenga na mkandarasi alikwishapatikana; kama sijakosea ni Barabara ya Masasi – Nachingwea kwenda Liwale. Ni kwamba ilikuwa kwenye *EPC+F* na tulisema kwamba tunafanya mapitio na hiyo barabara

tutaijenga kwa awamu. Taarifa tutakuja kuitoa rasmi ni kiasi gani tutaanza kuijenga barabara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, je, Daraja la Mto Luwegu kwenye Barabara ya kutoka Mtonya kwenda Mgombasi ambalo liliathirika na mvua na niliripoti hapa, lipo kwenye *list* ya madaraja yatakayokuja kutengenezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge tuweze kupitia madaraja maana ni madaraja yanayogharimu takriban bilioni 800. Kwa hiyo nitapitia ili tuone kama hilo daraja la watu wa Mkoa wa Ruvuma ni kati ya madaraja ambayo waliona yaingie kwenye utaratibu huo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya Utegi – Shirati – Kirongwe itaanza ujenzi wa kiwango cha lami? Nashukuru sana

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii tumekwishaitengea fedha na kinachofanyika sasa hivi ni maandalizi tu ya kukamilisha taratibu ili tuweze kuitangaza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Ujenzi wa Barabara ya Njianne, Kipatimu, Nandete hadi Nyamwage**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya lami kutoka Kijiji cha Njianne – Kipatimu – Nandete hadi Nyamwage utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Barabara ya Njianne – Kipatimu – Nandete – Nyamwage imekamilisha usanifu wa kipande korofi cha barabara hii chenye urefu wa kilomita 10 kuanzia Njianne – Chumo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja sita ya kudumu na baadaye iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Sehemu ya barabara hii iliyobaki ya kuanzia Chumo – Kipatimu – Nandete – Nyamwage itafanyiwa usanifu ili kujengwa kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuletea katika Mkoa wetu wa Lindi jumla ya shilingi bilioni 140 kwa ajili ya marekebisho ya madaraja yaliyoharibiwa na mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya, yakiwemo haya sita ya Barabara ya Njianne – Kipatimu.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali ilipanga katika mwaka wa fedha uliopita kujenga mita 700 katika Kijiji cha Kipatimu kwa kiwango cha lami. Je, ni lini ujenzi huu utaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika bajeti iliyopita tuliahidiwa kujengewa kilometa 10 katika Barabara ya Nangurukuru – Liwale kwa kiwango cha lami. Je, ni lini kazi hiyo itaanza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kupongeza jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya kwa kurejesha na kujenga madaraja ya kudumu baada ya kuathirika kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza, mita 700 zilikuwa zinajengwa eneo la Kipatimu. Ilikuwa ianze kujengwa mwezi Desemba mwaka jana na kwa bahati mbaya sana madaraja anayoyaelezea yalikuwa yamekatika na hivyo hakukuwa na namna yoyote ya kuweza kufika kwenye eneo la ujenzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba, mradi ule haujafa, tutakwenda kukamilisha kujenga hizo mita 700 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilomita 10 kibali kimekwishatolewa, muda wowote tutatangaza na tutajenga maeneo ambayo tunaamini katika Barabara ya Nangurukuru – Liwale ni maeneo korofi na hizo kilomita 10 kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niulize swali la nyongeza. Giza limeendelea kutanda na matumaini ya Watanzania watumiaji wa Barabara ya Kutoka Kibirashi – Chemba – Kwa Mtoro mpaka Singida yameendelea kupotea. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na hatima ya ujenzi wa barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge na wananchi ambao anawawakilisha kwamba giza lisitande bali waone nuru mbele. Ninafahamu kwamba barabara hii ilikuwa kwenye *EPC+F* na tunavyoongea sasa hivi Mheshimiwa Rais alishaunda kamati ya namna ya kujenga barabara hizi. Kama nilivyosema, kwamba barabara hizi zitajengwa na tutatoa utaratibu wa namna ya kujenga barabara hizi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, je, kuna kikwazo gani kinachosababisha kushindwa kumtangaza mkandarasi wa Barabara ya Mlandizi hadi Ruvu *Station* yenye urefu wa kilomita 23 ilihali kazi hii ilikwishatangazwa na waombaji walikwishaomba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara ikishatangazwa lazima ipitiwe. Kwa hiyo kama kuna changamoto yoyote tutaiangalia ili tuone kitu gani kimekwamisha. Nimwombe Mbunge baada ya hapa tuweze kuonana ili tuone ni kitu ambacho kitakuwa kimekwamisha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Barabara ya kutoka Kibaoni – Bunazi – Kagera *Sugar* yenye urefu wa kilomita 25 itajengwa; ambapo ni mwaka mmoja umepita tangu mkandarasi aliposaini mkataba akisubiri *advance?* Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Wizara tayari tumeshaomba malipo ya awali kwa mkandarasi ili aweze kuijenga hiyo barabara. Mara tutakapomlipa basi kazi hiyo itaanza mara moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana Serikali kwa Ujenzi wa Daraja la Chakwale. Je, ni lini Barabara ya Gairo mpaka Kilindi itajengwa kwa kiwango cha lami ikiwa ni ahadi ya viongozi wa kitaifa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Gairo ambayo inaanzia Ngilori na inapita kwenye madaraja hayo kwanza changamoto kubwa ilikuwa ni hayo Madaraja ya Nguyami na Chakwale ambayo tayari mkandarasi amekwishapatikana na hivyo wanaanza kuyajenga. Baada ya hapo tutasanifu hiyo barabara ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Mapitio na Maboresho ya Sera ya Malezi ya Mwaka 1977**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya mapitio na maboresho ya Sera ya Malezi ya mwaka 1977 ikizingatiwa wakati huo hakukuwa na utandawazi kama ilivyo sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawahi kuandaa Sera ya Malezi ya Mwaka 1977, badala yake iliandaa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 1996 ambayo ilifanyiwa mapitio na kuja na Toleo la Pili la Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008. Sera hii ndiyo inayotumika hadi sasa kutoa maelekezo kuhusu upatikanaji wa haki na ulinzi wa mtoto. Hata hivyo, Serikali imefanya tathmini ya awali ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 na kubaini kuwa ipo haja ya kufanya mapitio na kuboresha Sera hiyo ili kukidhi mahitaji ya sasa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, naridhishwa kwa kiasi kikubwa sana na namna ambavyo Serikali inatekeleza ama inaweka mazingira mazuri ya watoto katika nchi yetu. Hata hivyo, ninaomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ikiwa Serikali bado haijandaa Sera hii, je, hawaoni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuwa na Sera ya Taifa ya Watoto na Vijana Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa vile Chama Cha Mapinduzi tayari kina Sera nzuri sana kwa ajili ya malezi kwa watoto na vijana wa Taifa letu. Je, Serikali iko tayari itakapokuwa inaona inafaa kutushirikisha Umoja wa Wazazi Tanzania, Jumuiya ya Chama Cha Mapinduzi ambao ndio wasimamizi wa suala la malezi ili tuweze kutoa mchango wetu na kuwa na jambo zuri katika Taifa letu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba tunatunga sera za malezi na makuzi kwa ajili ya Watoto. Hivi juzi tu tumepitisha Sera ya Ulinzi wa Mtoto kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Serikali inalinda watoto na kuwa salama. Sera ambayo tumepitisha ni makosa ya kimtandao, Sheria ya Mtoto, Sura Na. 13, lakini siyo Sera ya Mtoto. Kwa hivyo Serikali ina

wajibu na tunaendelea kuhakikisha kwamba mtoto anapata haki zake na kuwa salama na amani. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kama nilivyosema Serikali itaendelea kutunga sera ambazo zitawasaidia na kuwalinda watoto wetu. Itakapokuwa tayari tutawashirikisha wote, ikiwa pamoja na Jumuiya ya Wazazi. Kwa vile Mheshimiwa Najma ni mjumbe wa Jumuiya ya Wazazi ana haki na yeye kuhakikisha anatoa maoni yake katika kutunga sera hizi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Uzalishaji wa Madini ya *Niobium***

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, lini uzalishaji wa Madini ya *Niobium* na Kiwanda cha *Farroniobium* utaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uchimbaji wa Madini ya *Niobium* katika eneo la *Panda Hill,* Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya unamilikiwa na Kampuni ya *Panda Hill Tanzania Limited (PHTL)* ambayo ina leseni tatu za uchimbaji wa kati wa madini *(mining licence)* kwa ajili ya kuzalisha mazao mbalimbali ya madini. Moja ya mazao ya madini ya *niobium* baada ya kuyachakata ni *ferroniobium.* Zao hili hutumika kwenye injini za ndege na *rockets,* mitambo ya uchorongaji ya utafiti wa mafuta *(oil rigs),* mabomba ya gesi na mafuta, pamoja na utengenezaji

wa magari kutokana na sifa ya kuzuia mitambo husika kushika kutu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura 123, wamiliki wa leseni za kati na kubwa za uchimbaji madini wamepewa sharti la kutoa hisa huru na zisizofifishwa na zisizopungua 16% kwa Serikali. Kutokana na uwepo wa takwa hilo la kisheria, Serikali ilianza majadiliano na Kampuni ya Panda *Hill* kwa lengo la kusaini Mkataba wa Makubaliano utakaowawezesha Serikali kupata umiliki wa hisa hizo kwenye mradi huo; ikiwa ni pamoja na manufaa mengine ya kiuchumi. Majadiliano hayo yanaendelea na yapo katika hatua nzuri. Aidha, Serikali iko mbioni kukamilisha majadiliano hayo sambamba na kukamilisha taratibu za ulipaji fidia wananchi wa eneo husika ili kuwezesha shughuli za uchimbaji na ujenzi wa kiwanda cha *ferroniobium* kuanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Sasa kutokana na utayari wa wawekezaji kutimiza masharti yote ambayo wanatakiwa kuyatimiza ikiwemo uwekezaji wa dola milioni 250 kama *FDI*. Je, ni kwa haraka kiasi gani Serikali itahakikisha kuwa hawa wawekezaji wanapata leseni yao ya *EPZ* ili waanze kujenga kiwanda ambacho kitakuwa ni cha kwanza Tanzania na cha nne duniani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa sababu kuna eneo ambalo lina wananchi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, sasa ni lini wako tayari kuingia mkataba na huyu mwekezaji ili aweze kuanza kazi mara moja? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Oran Njeza, kwa kuleta swali hili muhimu la mradi huu wa madini muhimu ambayo na sisi kama Taifa tunayahitaji kwa ajili ya kukuza uchumi wetu. Ninaomba kujibu maswali yake mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kumjulisha kwamba, majadiliano yanayoendelea ili kufikia kuwekeana sahihi kwenye huo mkataba unaitwa *Framework Agreement* yanaendelea na kesho watakutana Arusha kwa sababu ya kumalizia vipengele vya muundo wa makubaliano hayo ambayo inajumuisha vitu vitatu vya msingi:

(i) Muundo wa jinsi Serikali itakavyoshiriki katika uzalishaji wa hayo madini (uchimbaji madini) wenyewe;

(ii) Muundo wa jinsi Serikali itakavyoshiriki katika kiwanda hicho cha uchakataji, itakavyopata hizo hisa zake;

(iii) Uundaji wa kampuni tanzu kwa takwa la kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo basi, watakapokuwa wamemalizia hilo na tuombe Mungu kesho hatua ya majadiliano hiyo iweze aidha kufikia mwisho au kukaribia mwisho, waweze sasa kusaini huo mkataba. Hapo ndipo sasa wataweza kwanza watahamisha gereza lililopo pale, watafidia watu na shughuli za kuanzisha eneo la *EPZ* ambalo lilikuwa kwenye *framework* inayojadiliwa, litaweza kuanzishwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na Serikali kuwapatia majibu. Nitaleta matangazo yaliyo hapa mezani kisha tutaendelea na ratiba yetu. Tutaanza na tangazo linalohusu wageni waliofika asubuhi hii Bungeni.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika; hawa ni wageni watatu kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Magonjwa ya Moyo *(JKCI),* waliopo katika Kituo chetu cha Afya hapa Bungeni ambao wanaendelea kutoa huduma kwa ajili yetu.

Wapo Dkt. Jimmy Ernest ambaye ni Daktari Bingwa tiba ya pua, koo na sikio; Dkt. Lorna Kasyanju, ambaye ni Daktari Bingwa wa magonjwa ya Ngozi na Dkt. Emil Richard, ambaye ni Daktari

Bingwa wa Magonjwa ya Mifupa. Karibuni sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni sehemu ya madaktari ambao wanaendelea kutoa huduma pale kwenye Kituo chetu cha Afya. Kwa hiyo, tuendelee kwenda hapo kutazama afya zetu.

Tunao wageni mbalimbali, wageni wenu Waheshimiwa Wabunge. Tunaanza na Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, akishughulikia afya. Wapo Wanafunzi 25 na Walimu wanne kutoka Shule ya *Mother of Mercy* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Haya, watoto wameruhusiwa jamani ni wadogo, kwa hiyo kusimama wote kwa pamoja kidogo inakuwa mtihani, lakini tumewaona watoto wetu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Haya, tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; hawa ni Wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Kusini Unguja, Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, ambao ni wanafunzi 130 na Walimu 14 kutoka Shule ya Msingi *Joyland* kutoka Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa George Mwenisongole, ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Kata ya Magamba, Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Haya tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ambao ni watoto wake kutoka Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ambaye ni Katibu wake kutoka Mkoa wa Mara. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 46 na walimu saba kutoka Kituo cha *Ametech Training Center* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 48 na Walimu watano wa Shule ya Sekondari Chikole kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania. Anawatangazia kwamba, leo Saa saba Mchana, kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Spika uliopo Ghorofa ya Tano, Jengo la Utawala. Katika kikao hicho nami nitakuwepo. Waheshimiwa Wabunge Wanawake mnakaribishwa sana. *(Makofi)*

Haya, baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023;**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji**

**ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wangependa kuendelea kuchangia hoja hizi tatu za Kamati.

Tutaanza na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hoja zilizo mbele yetu. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali anayoiongoza kwa kuonyesha nia ya dhati ya kupunguza hizi hoja za CAG zinazotokana na uzembe, wizi na matumizi mabaya ya fedha za Watanzania. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani sote ni mashahidi, katika ziara mbalimbali za Mheshimiwa Waziri Mkuu huko mikoani, tumeona ni namna gani amekuwa na nia thabiti ya kuhakikisha fedha za Watanzania zinabaki kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kidogo na tupeane uzoefu na mwanga wa kuona ni namna gani sasa hizi hoja zinaenda kwisha. Ninadhani sote ni mashahidi, tunaona huu wizi unaoendelea na huu uzembe ambao kila ikija Ripoti ya CAG Bungeni imekuwa kama ni wimbo. Fedha hazijatumika inavyopaswa, fedha hazionekani zilipokwenda na mambo mengine ya kizembe ambayo yamekuwa yakilisababishia Taifa hasara.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida kujadili mambo haya na tukiona kwamba imekuwa kama ni utamaduni. Tangu sijawa Mbunge, mpaka nimekuwa Mbunge, zoezi hili linaendelea, tunakuja hapa tunajadili, tumbua huyu, fukuza huyu,

shughulikia huyu, lakini kila Ripoti ya *CAG* inaposomwa, inakuwa na mambo yale yale yanayohusisha wizi na uzembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, ninadhani umefika wakati wa sisi wenyewe kujitafakari. Kufikiria kwa undani kwamba, ni nani anayezembea, anayeiba na anayetumia vibaya fedha zetu? Haya yote yanafanywa na watumishi tuliowaajiri Serikalini. Serikali inasimamiwa na viongozi wetu Mawaziri. Wapo watu wanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ninadhani ipo shida kubwa kwenye namna tunavyoajiri watu wetu. Kuanzia mwanzo tunavyopata wafanyakazi, tumekuwa tukilalamikia utaratibu wa ajira. Ninadhani tukiangalia kwa ndani mawazo ya wananchi na watu wanaotaka kuajiriwa, wengi wanaamini ajira bila *connection* haipatikani. Ndiyo maana sisi Wabunge ni mashahidi, kila Mbunge kwenye Jimbo lake ana meseji lukuki za kuombwa kusaidia watu wapate ajira.

Mheshimiwa Spika, watu wanaoajiriwa kwa kuamini *connection* ndiyo imewapa ajira, wanapoingia ofisini, wanaenda kufanya kazi kwa *connection* hizo hizo. Kwa hiyo, mwisho wa siku tunapata hasara ya fedha zetu. Ninadhani ipo haja kubwa ya kuangalia mfumo tunaotumia kupata Wakuu wa Mashirika yetu ya Umma, tunavyopata Wakurugenzi wa Halmashauri zetu na Makatibu Tawala. Je, hawa watu tunaowapata ni lazima tufike wakati tujiulize, tunahitaji Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kazi gani? Anahitajika mtu mwenye sifa zipi akawe Mkurugenzi wa Halmashauri au tunaweka tu mtu kujaza ile nafasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tujifunze kwenye benki. Tunaweza tukatoa mfano wa benki zetu nyingi nchini. Wanapohitaji Meneja wa Tawi la Kwimba, nafasi ya ajira ya Meneja inatangazwa ndani ya wafanyakazi wenye sifa. Wanaomba wafanyakazi wenye sifa ndani ya benki. Wanafanyiwa *interview,* wanapatikana watu bora wa kuwa mameneja ndani ya utaratibu.

Mheshimiwa Spika, sisi tunachukua mtu ambaye ajira yake ya kwanza ni ukurugenzi; akawe Mkurugenzi aongoze Halmashauri ya Tandahimba iliyojaa wazoefu wakuu wa idara.

Anakuja, akifika pale yule Mkurugenzi anakuwa ni mwanafunzi wa wakuu wa idara. Kwa hiyo, wakuu wa idara badala ya kusimamia fedha zetu na maendeleo yetu, wanapata kazi ya kufundisha Mkurugenzi. Sasa, itategemea atakuwa mwanafunzi mzuri au mbovu, atakuwa na walimu wazuri au wabovu, atafundishwa vitu vizuri au vibovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi akikutana na walimu wabovu, akafundishwa vitu vibovu na yeye akawa mbovu, lazima fedha zetu ziibiwe. Hatuwezi kuendelea hivi, yaani ukurugenzi iwe ni kazi ya kujifunzia. Ni lazima Tume ya Mipango na Serikali mjipange vizuri. Hili jambo nyinyi wenyewe mnaliona. Nyinyi wenyewe Mawaziri mnazunguka huko, Mheshimiwa Waziri Mkuu unafanya ziara, unakutana na wezi huko.

Mheshimiwa Spika, hao watu wametengeneza utaratibu wa wizi kwa sababu ajira ni za *connection*. TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri Mkuu wale watu uliwakuta wanakomba fedha zetu kule, wanazileta kwa wakubwa TAMISEMI, hiyo ni *connection* tu ya wizi ambayo inatokana na mfumo mbovu wa ajira kwa sababu ili apate u-*DT* anatakiwa awe karibu na watu waliopo TAMISEMI na wale watu wanaompa u-*DT* ndiyo wanaomwambia aibe zile fedha. Sasa, anaachaje kuiba wakati anautaka u-*DT*?

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku mfumo wetu wa kupata watumishi tusipoubadilisha, tukawa tunachukua watu akaongoze shirika kubwa kama *TTCL,* anashindwa kushindana na *Tigo* ambayo imepanga, anashindwa kushindana na *ZANTEL* ambayo imepanga; *TTCL* ina majengo na rasilimali kila sehemu. Hii ni kwa sababu tunaweka watu ambao hawana *vision* na uwezo wa kutupeleka mbele na badala yake wakifika pale wanafanya kazi ya mazoea, fedha yetu inaendelea kuibiwa, *business as usual.*

Mheshimiwa Spika, ninataka kulishauri Bunge lako, tuishauri Serikali. Upatikanaji wa wakuu wa taasisi, wakurugenzi na viongozi mbalimbali upatikane kwa utaratibu ambao utatupatia watu bora na siyo watu wa kwenda kujaza nafasi. Kutoka hapo tunaweza tukapata mambo mazuri ya kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, ninadhani tuna shida ya mipango pia. Tunaposimama kila siku watu wameiba na wamezembea, ninadhani tushukuru Serikali kwa kuweka Tume ya Mipango. Ninadhani tunakuwa na Wizara ambayo inashughulika na mipango moja kwa moja, lakini wanayo kazi kubwa ya kufanya. Waziri wa Mipango na Tume ya Mipango kuna kazi kubwa sana ya kufanya. Aina ya miradi ambayo Serikali yetu inaitekeleza ninadhani tunatakiwa tufikirie miradi yenye vipaumbele itakayoweza kutukuzia uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tuna miradi ambayo inawekwa, ukijiuliza kwa nini mradi huu wameuacha, kwa nini wameweka huu, kwa nini vipaumbele vinatolewa kwenye eneo hili na siyo hili? Ninadhani kuna kazi kubwa sana ya kupanga. Ninapenda kushauri kwa mifano, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Sumve na katika Jimbo hilo kuna barabara ambayo nimekuwa nikiizungumzia sana, Barabara ya kutoka Magu – Ngudu – Hungumalwa. Kama kweli tupo *serious* na mipango, barabara hii ikitengenezwa kwa kiwango cha lami inapunguza umbali wa mtu anayetoka Shinyanga anaenda Nairobi kwa zaidi ya kilomita 66. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini Serikali kuendelea kupuuzia ujenzi wa barabara hii, inawaongezea wananchi zaidi ya kilomita 66 za kusafiri. Kwa hiyo, haya na yenyewe ni matumizi mabovu ya fedha za umma. Hii nayo ni hoja sema siyo hoja ambayo inakaguliwa, lakini ukiiangalia ni hoja ya msingi anayotakiwa kuja nayo *CAG*. Tunatakiwa tuangalie miradi yenye tija ipewe kipaumbele. Hatuwezi tu kuwa tunafanya miradi kwa sababu imesemekana ifanyike, lakini tunaacha miradi ya kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo shida moja Serikalini. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji. Kwenye Kamati ya Maji, idara na taasisi zilizopo kwenye Wizara ya Maji zinadai Idara za Serikali bilioni za fedha. Umekuwa ni utaratibu wa kawaida Serikali kutokulipana fedha. Magereza halipi maji, *TANESCO* halipi maji na Maji hamlipi *TANESCO*. Sasa, ninafikiri kuna sababu ya msingi tuje kama Serikali tukubaliane kwamba, suala la Serikali kulipana fedha limetushinda; kwa sababu kwa nini kila mmoja halipi?

Imekuwa ni utaratibu kila siku tunakuja kusumbuana humu, yanaletwa madeni. Huyu hajalipa, huyu hajafanya hiki, lakini tunajua kabisa na bajeti zao tunazipitisha hapa. Kila taasisi inapitishiwa bajeti ya maji na umeme. Hizo fedha wanapeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hizo fedha wakipitishiwa hazitumiki kwenye maji, basi tuache kuzipitisha. Kwa nini tuwe tunakaa watu wazima humu, wanakuja kutuambia wanahitaji shilingi bilioni 400 kwa ajili ya maji, tunawapitishia halafu wanaenda kuitumia kununua magari. Kwa hiyo, ninadhani ipo haja ya msingi kabisa ya kutoka na Azimio la kwamba, Taasisi za Serikali na mamlaka zinapopitishiwa bajeti ya huduma za maji na umeme na huduma nyingine zilipie kwa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja za Kamati zote na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ili nichangie hoja ambazo zipo mezani kwetu. Hoja ambayo ipo mezani kwetu ni Taarifa tatu za Kamati zetu za *PAC, LAAC* na *PIC*.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niwapongeze Wenyenviti wa Kamati hizi kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa hizi. Pili, niwapongeze Wajumbe wa Kamati hizi kwa jinsi walivyochambua kwa kina Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuja na taarifa hizi tatu ambazo zina takwimu za kutosha na taarifa ambazo zinajieleza wazi. Hongereni sana Wajumbe wa Kamati hizi tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utaanza na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)*. Kama nilivyoanza kutangulia kusema, ukisoma taarifa ya Kamati kwa kweli ni taarifa ambayo imekamilika, ina takwimu na imenyooka. Hongereni sana wana-*LAAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa sababu taarifa ya *LAAC* imesema kuna ongezeko la hati ambazo ni za kuridhisha. Taarifa iliyopita tulikuwa na hati 170 na hii inaonesha tuna hati 181 kati ya halmashauri 184. Kwa hiyo, kuna ongezeko, niipongeze Serikali kwa usimamizi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kupungua vilevile kwa hati zisizoridhisha, katika taarifa iliyopita tulikuwa na hati 13, taarifa hii sasa inasema kwamba tuna halmashauri tatu tu zilizopata hati ambazo haziridhishi. Kwa hiyo, ina maana zimepungua kutoka 13 na zikabaki tatu, hii ni kwa sababu ya usimamizi mzuri na maelekezo mazuri ya Serikali. Hongereni sana Serikali kwa kuendelea kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresho hayo, lakini taarifa ya *LAAC* imeeleza maeneo mengi ambayo bado yana changamoto na eneo mojawapo ni usimamizi wa fedha za umma na matumizi ya Akaunti ya Amana. Hiki ni kitu ambacho kipo wazi kabisa kwenye miongozo ya matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa. Kuna ile *Local Authority Accounting Manual* na *Local Authority Financial Memorandum*; zote zinaelezea vizuri matumizi ya Akaunti hii ya Amana. Ni kwamba, inawekwa amana kwa ajili ya malipo ya hawa ambao wameweka amana, lakini matokeo yake sasa, halmashauri wanafanya ni akaunti ya kimbilio.

Mheshimiwa Spika, likitokea lolote wanakimbilia kwenye Akaunti ya Amana na ikitokea sasa mwenye amana anakwenda kudai fedha zake, inakuwa zile fedha zimeshatumika. Hii siyo sahihi, Kamati ya *LAAC* imeeleza vizuri madhara ya matumizi haya mabaya ya Akaunti ya Amana. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kwamba, Serikali itaendelea kuzisimamia halmashauri na kuzielekeza kwa matumizi sahihi kulingana na miongozo iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Kamati ya *LAAC* imebainisha halmashauri kutolipa madeni ambayo wanadaiwa na imeelezea waziwazi madeni ya makundi mawili; kuna deni la wazabuni na deni la watumishi. Watumishi wasipolipwa stahiki zao kwa wakati, wanapunguza *morale* ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli tunawasingizia watumishi wezi, siyo waadailifu, lakini wakati huo ni *carrot and stick.* Lazima tuwape motisha hawa watumishi, anapostahili kupata mshahara wake apate kwa wakati, anaposafiri apate stahili zake, anapoumwa apate fedha za matibabu. Kweli utamdai uwajibikaji, lakini kama stahili zake za msingi hazipati, tunaweza kumkamua ng'ombe ambaye hatumlishi vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa Kamati ya *LAAC* imeelezea vizuri athari na bahati mbaya sana halmashauri ambazo zimetajwa nyingine zina vyanzo vingi vikubwa vya fedha. Mtumishi wa umma yeye anapotaka stahili zake, hajui fedha zinatoka Serikali Kuu au Mamlaka ya Serikali za Mitaa, anachotaka ni haki yake. Kwa hiyo, unakuta wakurugenzi wengine sasa imekuwa kama *fashion*, Mtumishi akidai anasema kwamba deni lako limeshahakikiwa, subiri Hazina, kitu ambacho siyo sahihi. Tumeona hapa Jiji la Dar es Salaam linadaiwa fedha nyingi na watumishi, jiji lina makusanyo mengi, kwa nini wasilipe watumishi? Huwezi kuwekeza kwenye mipango mingine wakati watumishi wako huwalipi. Kwa hiyo, ni muda sahihi halmashauri wajielekeze katika kutoa stahiki kwa watumishi wao ili watumishi nao wawe na *morale*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ya madeni ni ya wazabuni na inachekesha sana. Wajumbe wa Kamati wamesema hapa wakati wanachangia, halmashauri imeshapata huduma kwa mzabuni. Halafu ukimwambia kwa nini hulipi? Anasema vielelezo vyake havijakamilika. Wewe umekula chakula chake wakati wa semina, umeshakula tayari, unataka kielelezo gani? Umekula kuku, mayai, unasema hajaleta vielelezo, unataka akuletee nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mzunguko tu wa kutaka kumzungusha yule mzabuni na maskini, huyu ni mjasiriamali mdogo tu ambaye anapeleka ile huduma pale halmashauri. Unaambiwa vielelezo vyako lete, mara vimepotea lete vielelezo vingine. Kwa kweli, hapa hii siyo sahihi, tunaua mitaji ya wajasiriamali na halmashauri sifa yao kubwa ni kuhama! Wakishafilisi mfanyabiashara huyu wanahamisha huduma sasa wanapeleka sehemu nyingine. Kwa kweli, hatufanyi sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, iendelee kuzisimamia halmashauri kulipa madeni haya ya watumishi na madeni ya wazabuni. Nami ninakubaliana kabisa na mapendekezo ya Wizara kwamba, lazima hizi halmashauri zilipe madeni ya watumishi na madeni ya wazabuni, la sivyo hatua kali zichukuliwe kwa hawa wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili utahusu Taarifa ya *PAC*, hapa imeonesha ukurasa wa 16 kuna deni kubwa ambalo *TPDC* inaidai *TANESCO*. Takribani shilingi bilioni 713. Hii siyo sahihi kabisa na hili ni ongezeko la 23%, kwa sababu taarifa ya mwaka jana ilikuwa inadaiwa shilingi bilioni 579.

Mheshimiwa Spika, huu ni kama ule mchezo wa mtoto ndani ya nyumba; watoto wanakwenda shule, lakini mtoto mwingine anaficha sare na viatu vya mwenzie, halafu kesho anakuja kuripoti kwamba baba, fulani hajaenda shuleni. *TANESCO* na *TPDC* wapo Wizara moja, anaposhindwa kumlipa fedha *TPDC*, *TPDC* haita-*perform,* halafu leo ionekane kwamba *TPDC* hai-*perform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TPDC* kwa sasa ina majukumu mengi sana, tunaenda kwenye *clean energy* na hawa wana nafasi kubwa sana ya kufanya. Sasa hivi tunawaambia *TPDC* kasi yao ya usambazaji wa gesi asilia majumbani ni ya mwendo wa konokono. Ni kwa sababu ya fedha hizi ambazo hazilipwi, *TANESCO* wameshapata huduma na wateja wa *TANESCO* wanalipa, lakini wao kuwalipa *TPDC* hawawezi. Kwa hiyo, nami ninaungana na mapendekezo ya hii Kamati kwamba, *TANESCO* lazima isimamiwe ili ilipe hili deni kubwa na *TPDC* la shilingi bilioni 713, ili *TPDC* iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TPDC* wana kazi kubwa ya kufanya, kuna uchorongaji wa visima vipya vya gesi, kuna ulinzi wa Mkuza wa gesi kutoka Madimba mpaka Kinyerezi na mambo mengine mengi ambayo *TPDC* inatakiwa iyafanye, lakini wanakwamishwa na inaathiri hali ya kifedha ya shirika hili kwa sababu ya deni kubwa ambalo *TANESCO* hawawalipi *TPDC*. Kwa hiyo, ninaomba kama walivyopendekeza Kamati kwamba, Serikali lazima ije na mkakati ili *TANESCO* walipe deni hili kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kuzipongeza hizi Kamati tatu kwa taarifa nzuri na ushauri wangu kwa Serikali ni kuboresha kitengo cha mkaguzi wa ndani na udhibiti wa mifumo ya udhibiti wa ndani ili dosari kama hizi zisiendelee kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mezani. Ninaanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, ambaye ametupa uzima kwa siku ya leo tukawepo katika Bunge lako Tukufu. Pia, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyopambana katika Taifa letu ndani na nje kutuhakikishia kwamba tunapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipokupongeza wewe kwa jinsi ambavyo umetuwakilisha Kimataifa na ukaweza kuonyesha kwamba kwa kweli Watanzania tupo na umefanya vizuri sana na tunakupongeza kwa moyo wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati ya *LAAC* na Wenyeviti wote wawili ambao wameweza kuwasilisha ripoti vizuri ambayo tunaijadili leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nami ninaanza na eneo la makusanyo ya mapato ya Serikali kwa maana ya *TRA* na halmashauri zetu. Maeneo haya yamekuwa na udhaifu mkubwa sana katika kukusanya mapato na hii inaonekana katika ripoti ya *CAG* ambayo imeeleza kwamba, kwa mfano, *TRA* ilikuwa ikusanye kiasi cha shilingi trilioni 23.652, lakini ilishindwa ikawa imekusanya shilingi trilioni 22.583 na kushindwa kukusanya kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.069.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambazo zipo katika ukusanyaji wa mapato, siyo kwamba nchi hii haina fedha, nchi hii kuna fedha nyingi sana ambazo zingekusanywa kwa uaminifu na uadilifu mkubwa na kutanguliza uzalendo, ninaamini kwamba fedha zingekuwa nyingi kuliko hata hizo shilingi trilioni 23 ambazo zilikadiriwa kukusanywa.

Mheshimiwa Spika, katika taasisi yetu hii ya *TRA* kuna baadhi ya watu wachache ambao siyo waaminifu, waadilifu, siyo wazalendo. Kuna wengi wanafanya kazi vizuri, lakini kwa kweli wengine siyo waaminifu kiasi ambacho kinaikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia suala ambalo linaongoza katika maeneo haya ya ukusanyaji wa mapato, unaambiwa hata ving'amuzi havisomi kama mzigo uko ndani ya nchi au umeshatoka, ukiwa mpakani au ukiwa ndani ya nchi. Inaonyesha kwamba, hapo hatujui ni mifumo haisomani, ni mchezo wa wataalamu wetu au ni namna ambavyo hatujajiandaa vizuri kukabiliana na teknolojia ambayo itatuwezesha kukusanya mapato yetu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo linachangia kwa sehemu kubwa ukosefu wa mapato ni suala la ufisadi na rushwa. Katika sheria ya ukusanyaji wa mapato, kuna hili suala la kukadiria kwamba unatakiwa ulipe labda shilingi bilioni kadhaa au shilingi milioni kadhaa. Watumishi wa *TRA* wanapokaa mezani kujadiliana na mfanyabiashara, wanamzidishia kodi kubwa, kwa hiyo, inakuwa ni tishio kwake na kufika mahali sasa ambapo mfanyabiashara anaona ni bora nifanye *bargain* ya kutoa rushwa ili wanipunguzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanamwambia usipotupa kiasi fulani, labda shilingi milioni 300 au shilingi milioni 200, ni lazima utupe. Usipotupa sisi tutakuzidishia kodi zaidi. Haya maeneo yanatokana na sheria yetu ya kuruhusu mwanya wa kukaa mezani na kujadiliana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2023 niliomba Wizara ya Fedha ije na sheria itakayo-*fix* kwamba, kama mfanyabiashara analipa

kodi hii, basi sheria itamke wazi kinagaubaga kwamba anatakiwa alipe kodi kiasi hiki. Tukiendelea kuwaachia mwanya huo, ninaamini bado tutaendelea kulia kilio cha kutokukusanya mapato kwa sababu ya ukosefu wa uzalendo, uaminifu, uadilifu na uwajibikaji, ambao ni udhaifu wa baadhi yao katika taasisi hii ya *TRA,* halikadhali na katika halmashauri zetu ambazo na zenyewe zinashindwa kufikia malengo kadri ambavyo bajeti imekusudiwa kukusanywa.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa uhamasishaji wa walipakodi na uelewa mdogo; lazima sasa *TRA* ifike mahali hata itumie simu, *TV* na *message* ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaelewa dhamira ya Serikali kukusanya kodi ili iweze kuleta maendeleo, kwa sababu, kodi ikikusanywa kwa kiwango kinachotakiwa, basi maendeleo yatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limenisikitisha katika ripoti iliyotolewa na Kamati zetu hapa ni usuluhishi wa mashauri ya kikodi, ambao umeweza kuisababishia Serikali kushindwa kukusanya shilingi trilioni 10.489. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, trilioni 10, kesi haziishi, watu wamekaa, hizo *tribunals* hazimalizi kesi, hili ni tatizo. Kama tusipoliangalia litaendelea kutupa matatizo makubwa katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ijihoji na ijitathmini kwamba, lazima ije na sheria ambayo itaweka *limitation* ya kesi zote ambazo zinahusu masuala ya kikodi. Vinginevyo tunaanza kusema mashauri yanakaa pale kwenye hizo *Tribunals* hayaishi, kumbe kuna mchango mwingine ambao unaweza ukarudi kwa nyuma ikawa ni suala la rushwa na ufisadi unatengenezwa katika hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ilichukue hili kwa makini kabisa, ilete sheria ya kuhakikisha kwamba, kama kesi ni ya kodi iishe ndani ya mwezi mmoja au ndani ya miezi miwili, au miezi mitatu, *full stop*. Mambo ya kupeleka kesi ya kodi ya shilingi trilioni 10 kwa miaka miwili, mitatu, minne, huo ni ujanja ambao hauwezi kukataliwa kwamba hakuna jambo ndani. Ina maana kwamba *there is something behind the scene*, kwa sababu haiwezekani kesi kukaa muda mrefu. Hata Mahakama yeyewe inakuwa na

mwisho wa kesi zake, ikifika miezi tisa kesi inakuwa imefika mwisho. Sasa hii ya kwetu ambayo tunataka kupata kodi ambayo hatuwezi kuwa na mwisho, haiwezi kukubalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iweze kutuelewa kwamba tuna nia njema ya wao kukaa chini kwa sababu, bila kodi hakuna Serikali, hakuna maendeleo, hatuwezi kukaa humu ndani, Taifa haliwezi kusonga mbele, hakuna amani. Kwa hiyo, ninaomba suala hili tuliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la madeni ya wazabuni na watumishi; ninaomba sana, ninajua Serikali ina mambo mengi, lakini suala la madeni ya wazabuni, suala la madeni ya watumishi. Ninaomba watumishi waangaliwe kwa jicho la huruma kwa sababu ndiyo maana inasababisha hata mahali wanapoona jambo lolote wanajaribu kufanya mambo ambayo siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba madeni hayo ya wazabuni yalipwe, hasa hawa Mama Ntilie ambao wanadai, ambao wanatoa *service* kwenye halmashauri zetu na hawapewi fedha zao, hili siyo jambo zuri. Haina maana mtu unakula chakula cha mtu, umeshaweka tumboni, hata wakati mwingine umeshatoa kimeondoka, halafu baadaye anakufuata kiguu na njia mpaka soli inaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la uhamisho wa wakurugenzi na watumishi wengine, kwa maana ya wakuu wa taasisi. Tunaishauri Serikali, suala hili liangaliwe kwa umakini kwa sababu, kumhamisha mkurugenzi ndani ya miezi miwili yuko pale, ndani ya miezi mitatu yuko pale, ndani ya miezi minne yuko pale, hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inataka kutuambia kwamba ina jambo inalotaka kuficha dhidi ya ufanisi wa watumishi hawa? Kwa hiyo, ninaomba iangaliwe, lakini pia tuwe na watumishi ambao wana uzoefu wa kutosha, tusichukue mtu tu ni mtu kwa sababu ni rafiki yangu, ni shangazi yangu, ni mjomba wangu, ni wa rafiki yangu, hayo mambo katika Serikali hayafai.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji ufanisi, watu ambao wana uwezo, ambao wako *competent* ili waweze kuleta ufanisi katika Serikali na kuhudumia Watanzania na kuifanya Serikali iweze kung'ara kwa sababu ya watumishi walio bora, ambao siyo kwamba tumewachukua tu kwa sababu ya *undugunization*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu; nami ninaishukuru sana Serikali, kwa sababu, tulikuwa tunapiga kelele humu ndani kwamba watu wa miaka 35 – 45 ambayo ndiyo mwisho wa kuajiriwa Serikalini, ilikuwa nao waingizwe. Sasa, ninaishukuru Serikali na baadaye pia ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri anayehusika, atakapofika hapa kama ambavyo jana alijibu swali hili, kwamba sasa wananchi kuanzia miaka 18 – 45 wanastahili kupewa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia japo kidogo. Nami nitajikita kwenye Kamati ya *PAC* kwa maoni ambayo wao wameyatoa kwa ajili ya kuona namna gani tunaweza kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nikijaribu kushauri ndugu zetu wa Stendi ya Msamvu pale Morogoro ambapo *LAPF* walitoa fedha zaidi ya 74% na baadaye halmashauri ikatoa 26%, fedha zile hazijaweza kurudishwa, ina maana tunaendesha kwa hasara. Wakati wanaweka mpango wa kuendesha ile stendi, ilikuwa ni kusaidia miundombinu tuweze kuwa na stendi bora kusaidia wanaopitisha mabasi, lakini kuwasaidia wananchi waweze kupata sehemu sahihi ya kupata usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walipanga kwamba katika faida ambayo wanaipata, basi angalau shilingi bilioni 2.5 iwe

inarudishwa kwenye halmashauri na wenzetu wa *LAPF* waliikabidhi halmashauri kukusanya fedha zile, lakini fedha haziendi zaidi ya miaka 13, fedha hazifiki, hasara imeendelea kuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nijiulize, kwa nini watu binafsi wanafanya biashara vizuri na usimamizi unakuwa mzuri, inapokuja kwenye mambo ya kijumuiya ya Kiserikali, tunapata hasara? Hii inaonyesha jinsi gani ambavyo hatusimamii. Tuliopewa dhamana ya kusimamia watu wafanye kazi kwa uaminifu, wanafanya kazi vibaya na kusababisha Serikali yetu kupata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, haiwezekani kuniambia pesa zaidi zimewekwa pale bilioni za kutosha, halafu stendi haiingizi fedha. Kwa nini tunaanzisha miradi ambayo inaleta hasara? Kumbuka hii ni michango ya wafanyakazi, ambao wanatumia fedha zao, zimewekwa kwenye mifuko, mifuko inaenda kuendesha biashara ambazo zinaleta hasara. Mwisho wa siku inasababisha watumishi wanapostaafu wasipate fedha zao kwa wakati, kwa sababu kuna hela imelala sehemu haijafanyiwa kazi au imeibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inasema kwamba, kuna mashirika yamepeleka wakandarasi ambao hawana uzoefu. Hivi inakuwaje unatoa kazi kwa mkandarasi ambaye siyo mzoefu? Kamati inasema imekuja kugundua kwamba watu wanapewa tenda, anafanya kazi anaachia katikati kwa kutokuwa mzoefu. Nani awajibike? Kwa nini tusiwawajibishe hawa watu? Wizara iko wapi? Watu wazuri wa kufanya kazi hizo wapo, tatizo ni usimamizi, kwa sababu wale wasimamizi wanaosimamia ni wezi, ndiyo maana wizi unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mashirika ambayo yanategemea ruzuku kutoka Serikalini, mashirika yanapata fedha, lakini bado yanapata hasara. Hivi wewe unaletewa fedha na mzazi wako unapewe mtaji huu hapa, halafu ule mtaji unakatika hujapata faida, lakini watu binafsi wanafanya kazi kama unayofanya wewe lakini wanapata faida.

Mheshimiwa Spika, tuna mashirika kama Shirika la Wakala wa Mabasi ya *DART*; tunaona kabisa Wakala wa Umeme

*(TEMESA)*, Kamati imezungumzia, tunazungumzia hawa watu wa Nafaka na Mazao *(CPB)* wanaleta hasara na wanafanya kazi kidogo, yaani hakuna faida. Kwa nini tusubiri mpaka watu wa Mwenge wapite ndiyo waseme mradi huu ni mbaya au Mheshimiwa Waziri Mkuu, aende ndiyo aseme tunamtoa mtu huyu kwa nini? Kwa nini wanaosimamia na waliopewa dhamana wasiweze kuona kama kuna hasara na kuwatoa wanaohusika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Benki ya *TIB*, benki hii ilianzishwa kwa ajili ya kuleta faida na kuwezesha kupata mitaji, lakini benki hii imeingiza hasara zaidi ya shilingi bilioni tano, benki hii siku zote haifanyi kazi kwa ufanisi. Hii haiwezekani kabisa, *of course* Serikali hapo lazima ilaumiwe; wana mtaji wa shilingi bilioni 88 ijapokuwa mtaji wao unahitajika kufika shilingi bilioni 200, kwa hiyo wana hasara ya shilingi bilioni 127. Sasa usipompa mtaji pia huyu mtu hata kama unamlaumu mtaji hujampatia anawezaje kufanikisha kazi ambayo umempatia? Tumesema benki hii inasaidia mitaji, Serikali haijatoa mtaji. Ninafikiri kuna haja ya Serikali inapokuja kuhitimisha iweze kutueleza ni namna gani tunaanzisha vitu halafu tunashindwa kuviwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mingi sana ya maendeleo ambayo inaanzishwa, tuna mradi tunauanzisha, lakini hauanzi kwa wakati, ndiyo na mikataba tumesaini, lakini mwisho wa siku riba zinaongezeka. Leo hii tunalipa riba nyingi sana kwa sababu tumechelewesha kuendesha mradi au mkandarasi au mtu yeyote amefanya kazi, lakini anapoleta *certificate* yake hawamlipi kwa wakati riba inaongezeka na kuipa Serikali hasara. Ninadhani kuna haja yakubadilisha hii tabia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana kuna Mbunge mmoja amezungumza, kuna mkopo ambao tumepewa kule Biharamulo, mkandarasi amefanya 60%, halafu mwisho wa siku anakwambia amepata hasara. Hivi umepewa pesa za mdhamini, *donor* ametoa fedha halafu unaachia kazi katikati unasema kuna hasara. Hii haiendi sawa, hawa watu wawajibishwe wanajulikana wapo Tanzania, kwa nini walileta hasara? Kwa nini wasikamatwe? Kwa nini wasirudishe mali za Watanzania? Kwa sababu hata kama ni msaada tumepewa, lakini imepewa nchi, hajapewa mtu,

haijapewa wilaya, ni mali iliyopewa Taifa hili, kodi ya Watanzania, mali ya Watanzania, hawa watu wawajibishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nizungumzie suala la *REA*. Kuna hii miji midogo ambayo inahitaji umeme, leo hii umeme wa *REA* ni wa vijijini, lakini unakuta sehemu kwa mfano mji mdogo upo maeneo ya vijijini yaleyale, watu ni walewale, huyu analipa shilingi 27,000 kuungiwa umeme, huyu analipa shilingi laki tatu. Lazima tukae tena chini tutafakari kama Taifa watu waliopo vijijini wote wapate umeme bila ya kuwabagua tutakuwa Watanzania wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia wakurugenzi, mkurugenzi hata akiwa mgeni anakutana na *engineer* amekaa miaka 20 sehemu husika, huyu mtu ameshakuwa mbobezi, ameshakuwa mtu aliyezoea kukata kona na kuiba, leo hii pesa zinaenda kwenye halmashauri zinapotea kwa sababu maafisa mipango ni walewale, utabadilisha wakurugenzi kila siku. Kwa hiyo ni bora ubadilishe watu angalau ukikaa miaka 10 basi abadilishwe aende sehemu nyingine, tutawalaumu wakurugenzi, lakini wakati mwingine kuna wafanyakazi wanakaa sehemu moja kwa muda mrefu sana, tunaomba wasimamie hilo tuhakikishe tunabadilisha watu na tunawasimamia na wale waliokosea na wakaiba wachukuliwe hatua kali ili tuweze kubaki na halmashauri zilizo salama na safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja za Kamati zote zilizotoa ripoti mahali hapa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya ajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia taarifa zilizopo mbele yetu; Taarifa za *PIC, PAC* na *LAAC*. Kwanza nianze kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati yangu ya *PIC* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuandaa taarifa tukiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Vuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania tunayo mashirika 309 ambayo yanasimamiwa na Taifa letu. Mashirika hayo 309 yamegawanyika makundi mawili, makundi ya biashara na ambayo siyo ya biashara na katika makundi hayo yapo ambayo yanafanya vizuri na yapo ambayo pia hayafanyi vizuri. Baadhi ya mashirika baada ya kuchambua, Kamati imebaini changamoto zilizopo katika mashirika mbalimbali zikiwepo; mashirika kukosa mitaji ya kujiendesha, mashirika kuwa na madeni ya miaka mingi na kuna mashirika yanayofanya vizuri, lakini bado yanahitaji kupata fedha ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza na mashirika ambayo miaka mitatu mfululizo yamekuwa yakizalisha madeni. Shirika la kwanza ni *TTCL* (Shirika la Mawasiliano Tanzania); *TPC* (Shirika la Posta Tanzania); *NARCO* (Kampuni ya Ranchi ya Taifa); *TFRA* (Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania); na Bodi ya Mkonge. Mashirika haya yamekuwa na madeni miaka mitatu mfululizo, nini maana yake? Maana yake ni kwamba hata kujiendesha yenyewe imekuwa ni kwa kusuasua. Tukumbuke kwamba fedha zinazotolewa ni kodi za Watanzania na ili mashirika yafanye vizuri ni lazima yarejeshe gawio Serikalini kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea pia mashirika ambayo yana upungufu wa mitaji. *TTCL* lina upungufu wa mtaji, *MSD* (Bohari ya Madawa) pia ina upungufu wa mtaji na *TIB* (Benki ya Maendeleo) pia ina upungufu wa mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nitaongelea zaidi kuhusu *MSD*. Tunatambua kwamba afya ndiyo kila kitu kwa maisha ya binadamu, Shirika hili limekuwa likisuasua na kufanya hata halmashauri zetu zinashindwa kupata dawa kwa wakati. Niiombe Serikali kwa kupitia Msajili wa Hazina, ahakikishe kwamba anawezesha Shirika hili kupata mtaji wa kutosha ili liweze kufanya kazi kwa ufasaha na kuleta tija. Tunaamini kwamba kwa Bohari yetu ya Madawa ikiwa na dawa za kutosha halmashauri zetu zote nchini zitapata dawa na kwa wakati na hivyo zitaboresha pia afya za Watanzania. Hivyo niisisitize sana Serikali ihakikishe kwamba Shirika hili linasimama vizuri na kufanya kazi kwa ufanisi.

Pia Serikali iisimamie kwa ukaribu ili liweze kufanya kazi na kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea pia kuhusu benki mbili za Serikali. Tunazo benki za *TIB* na *TCB*, benki hizi ziliundwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinakwamua uchumi wa Watanzania. Wapo wafanyabiashara wanategemea kupata mikopo ili kuendesha biashara zao, lakini benki hizi zimekuwa zikisuasua. Niiombe Serikali kupitia Msajili wa Hazina isimamie vizuri benki hizi ili ziweze kufanya kazi na kujiendesha vizuri na hata kuweza kutoa gawio Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea vile vile jinsi mashirika yanavyosuasua. Yapo Mataifa ambayo yamefanya vizuri sana, ninasema Mataifa kwa sababu zipo nchi ambazo zimefanya vizuri katika kusimamia mashirika yao na yakafanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija. Nchi kama Kuwait, China, Singapore, Abu Dhabi, Ethiopia na Misri. Ukiangalia nchi hizi zimesimamia mashirika yao vizuri na zimeweza kuyafanya yafanye kazi vizuri na kuleta tija katika mataifa yao, hivyo na sisi Tanzania tujifunze kutoka kwa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na nchi, kwa kuniwezesha na kunipa uhai siku ya leo tena kusimama ndani ya Bunge Tukufu kuweza kuchangia hoja ambayo imeletwa na Wabunge wenzetu ambao ni Wanakamati wameichambua vizuri, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, shukrani za pili, nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kunipa *support* katika Wilaya yangu ya Mbogwe, hakika maendeleo yanayoonekana 100% yanatoka

Serikali Kuu ni mkono wake Mheshimiwa Rais, abarikiwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tupo na hoja ya Ripoti ya *CAG* pamoja na Kamati zilizokaa na nimezisoma kikamilifu sana. Ushauri wangu wa kwanza (namba moja kabisa) wote waliyoonekana na makosa wachukuliwe hatua haraka iwezekanavyo na ninashindwa kutumia lugha nzuri, sijui nitumie lugha gani ambayo itaeleweka vizuri ndani ya Bunge hili na jamii yote ya Kitanzania kwa sababu imekuwa sasa ni mazoea, watu kula pesa za watu imekuwa ni hali ya kawaida. Niwaombe Wabunge wenzangu tunapoishauri Serikali katika mambo haya tuwe wakali ili kuyakomesha ili Taifa letu liweze kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka nimejaribu kujumlisha hasara ambazo zimepatikana ni pesa nyingi sana naona aibu hata kuzitaja, lakini kwa harakaharaka tukiangalia tu watu ambao waliaminiwa na Serikali kwenye halmashauri kukusanya kwa *POS* kuna shilingi bilioni 5.6, hazijulikani ziko wapi, hizi ni bilioni. Uki-*calculate* kwa harakaharaka ni vituo vingapi vya afya vingejengwa kwenye nchi yetu, unaona kabisa kwamba tuna watu wa *design* gani wezi ambao wamekuwa sugu, lakini zipo shilingi bilioni 61 ukisoma katika ukurasa wa 15, haya ni mapato ambayo hayakukusanywa na penyewe unaweza ukasema tu hizi ni akili zinatumika, watu wanasema hawakukusanya lakini walikusanya. Kwa sababu sisi tunaishi huko kijijini na huwa tunalipa hizi kodi na ushahidi tunao, lakini hapa unaambiwa kwamba shilingi bilioni 61 hazionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mamlaka zinazohusika nashauri zichukue hatua haraka iwezekanavyo ili kusudi Taifa letu liweze kupiga hatua. Hakika Tanzania ni nchi tajiri, ukiangalia wizi uliofanyika huu kwa muda mfupi unaona kabisa trilioni ngapi ambazo zimepotea hapa na zingelikuwa zinasimamiwa ama ikitokea bahati zikakusanywa hizi pesa kwa bajeti ambayo tuliipitisha na shida tulizonazo kwenye majimbo hakika wananchi wetu wanaenda kubadilisha maisha kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 23 watu walipewa mashine, wengine walikuwa wanatoza ushuru kwenye mchanga, kwenye

mawe ya madini, kwenye mageti pale wakulima wanapotoka shambani ina maana walikuwa wanatozwa ushuru, lakini hapo unaambiwa hizi pesa hazionekani shilingi bilioni 6.17 ukurasa wa 23. Hapa kwa kweli mimi inanipa wasiwasi na wakati mgumu sana. Wakati mwingine unafikiria kwamba watu wanapoenda Chuo Kikuu wanaenda kufundishwa wizi ama? Mbunge yule aliyekuwa anasema kwamba huu wizi unafanyika ki-*connection*, kwa sababu mtu peke yake hawezi akaiba shilingi bilioni sita ila kama ni *connection* sawa. Kama huwa wanatuletea ripoti hizi kututega kwamba tusikilize wanasemaje sawa, acha tuseme kwa sababu kazi ya Mbunge ni kusema, kuishauri Serikali na kuisimamia, acha tuseme hata watuue.

Mheshimiwa Spika, hili halikubaliki mbinguni na duniani, hawa watu wanatakiwa wachukuliwe hatua haraka sana na Waheshimiwa Wabunge ikiwezekana tuongeze na sheria kabla mtu hajapelekwa Mahakamani apitishwe kwenye Jeshi la Sungusungu kwanza ale tope na viboko ili anapoenda Mahakamani aende amejipanga kwa sababu kwenda tu mtu amechomekea suti halafu anakwenda na gari lake kule Mahakamani ni kuzungumza tu na kuweka Mwanasheria nimekula shilingi bilioni sita nakupa wewe shilingi bilioni moja inakuwa ni rahisi sana. Kwa hiyo, bora wawe wanapitia kwanza Sungusungu kabla hatujapitisha sheria ile tuliyoipendekeza mwaka jana ile. Wawe wanapitia kwanza Sungusungu wanakula tope, wanapelekwa Mahakamani ili kusudi hii tabia isiwe inajirudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna shilingi bilioni 17, hizi ni pesa zilikuwa zinawalenga watu wenye ulemavu pamoja na wanawake na vijana. Kila Mbunge akifanya mikutano haya maswali huwa tunakutana nayo, hizi pesa zipo kisheria ambapo zinatakiwa ziwanufaishe akinamama pamoja na watu wenye ulemavu. Ripoti hapa inaonekana kwamba zimeliwa shilingi bilioni 17.60, pesa za mapato ya ndani zinazokusanywa na hizi halmashauri zilizopitiwa.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia hapa Kamati ya *LAAC* imepitia halmashauri 55 na ukiangalia mbaya zaidi ninaangalia kwenye majiji mpaka ninajiuliza hivi sisi wa kwenye miji midogo sijui tujifunzeje sasa? Ipo Kinondoni, Temeke, Ubungo, Kigamboni, Dar

es Salaam, *Hai DC*, *Siha DC* na Same. Unafikiria haya maovu kama yanatendeka huko, unaweza ukafikiria kwamba sisi ambao tunakaa kwenye halmashauri za vijijini tunakutana na mambo haya, ninakubaliana na Mbunge yule aliyesema kweli hii ni *connection* huwa inafanyika na ndiyo maana huwa tunahangaika sana. Mimi Mbogwe watanikoma na mpaka watatambua kwamba, kumbe wapo Wabunge mashine za kusaga na kukoboa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hili suala halikubaliki kabisa, mkulima analima shamba analipa mapato halafu pesa haiingii kwenye Mfuko wa Serikali wakati huo sisi bado tuna shida ya barabara. Ukiangalia kwenye shule zetu hakuna madawati, ukienda vitongoji vingine vinahitaji umeme, tukifuatilia mambo ya pesa wakati mwingine kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, unakuta pesa hakuna ya kupeleka miradi ya maendeleo huku mtu mwingine ana trilioni ameshikilia mkononi, haiwezekani. Hili watusaidie sana Watumishi wa Mungu wale wanaofanya maombi kuliombea Taifa letu, kuhakikisha kwamba wezi wanakwisha kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala la madeni kwa wazabuni. Kuna wafanyabiashara wanafilisika sasa hivi, wanakopa mikopo benki wanafanya biashara na Serikali, hawalipwi kwa wakati muafaka. Mfanyabiashara unapokopa Benki marejesho ni kila mwezi, unakuta umefanya na halmashauri haikulipi pesa zako, hii benki ambayo na yenyewe ninaamini ni mali ya Serikali haikusikilizi ukiwapelekea zile *document* kwamba Serikali imekukopa, matokeo yake wanakuja kukufilisi nyumba yako, kama ni kituo cha mafuta kama ni nini wanapitia, huku Serikali ilishakula kabisa. Inasemekana hapo watoa huduma ni bilioni zaidi ya 14,270, hapa nchini ambao wamekanyagwa na halmashauri zetu. Ushauri wangu ni kwamba wale wanaohusika na mambo haya wachukue hatua haraka ili kusudi wazabuni waache kuwa wanadhulumiwa nyumba zao pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, suala la madeni kwa watumishi sijui niseme lugha gani kwa Kisukuma huwa tunasema; "*Wagunana mbuli wagunana na nighumela,*" watumishi hapa wanadai shilingi bilioni 87 ambapo wameifanyia kazi Serikali wanataka walipwe hii

haki yao. Kwa hiyo wakati mwingine ukirudi huku unaweza ukasema kweli ni maelekezo kweli, hawa huwa wanatuma mawakala waibe ili kusudi kuziba madeni yao. Kwa hiyo, niwaombe sana wakubwa zangu wale mnaohusika, watumishi wanapokuwa wanafanya kazi zao na wao wapewe stahiki zao ili na sisi kama wasimamizi wa Serikali, kwa sababu sisi Wabunge tunabahatika kukaa na mwizi, kukaa na mwema, kwa kweli kuna siku moja nimekaa na watumishi na wakasema kabisa kwamba mimi nimehama kutoka wilaya fulani, niliambiwa nitalipwa, lakini mpaka sasa hivi sijalipwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake mtumishi ambaye ni Mtumishi wa Mungu analazimika kuiba kwa sababu, halipwi haki yake. Kwa hiyo, hii Wizara inayohusika na mambo hayo ikiwezekana wakae na kuona kwamba, ni kwa nini wanaiba namna hii jamani?

Mheshimiwa Spika, kama kuna hasara ambazo zimesababishwa na wananchi, Serikali ikae kati ya watumishi na hawa wadai. Sasa tufikie mwisho, hesabu zifanyike, huku tunadaiwa hizi shilingi bilioni 87, lakini huku tuna hasara ya shilingi trilioni hizi hapa. Madeni yaishe ili Ripoti ya *CAG* mwaka ujao iweze kueleweka, kuliko kuwa tunaleteana hasara za hivi bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu umeeleweka. Nipige mambo mawili kama utaniruhusu, tupo kwenye mwaka wa Uchaguzi; kwanza, nichukue hatua hii kuwapongeza sana wananchi wa Tanzania kwa uchaguzi mdogo wa kura za maoni ambao wameufanya mijini na vijijini. Hakika tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, haki imetendeka kwa sababu, kila nikipita mtaani kwenye vijiji vyangu kuna furaha, watu hawajakatwa majina. Awamu hii chaguo la wananchi ndilo limerudi hilo hilo. Naamini na mwaka kesho ni Uchaguzi Mkuu**.** *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mohamed Said.

**TAARIFA**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe Taarifa mchangiaji, Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe, anachangia vizuri sana, lakini Watanzania hawajafanya uchaguzi kwa wote, ni CCM ndio ambao wamefanya uchaguzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, una pokea Taarifa hiyo?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, siipokei Taarifa, labda tu nimpe Taarifa kwamba, huko uliko mimi nilianzia huko nikaona ujinga nikarudi huku niliko. Kwa hiyo, naomba niendelee na kuchangia. Watanzania mwaka huu wamefanya Uchaguzi kwenye vyama vyao, wamechagua vizuri. (*Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, nafikiri nia ya Mheshimiwa Mohamed Said ilikuwa ni kwamba, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakuwa tarehe 27 Novemba. Kilichofanyika sasa hivi ni kura za maoni ndani ya Chama Cha Mapinduzi. Ndicho alichokusudia kukwambia kwamba, kile unachokisifia kisifie kwa sura ya ndani ya Chama Cha Mapinduzi ili wananchi wasije wakafikiria ule ndio uchaguzi umeshapita. *(Makofi)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima yako, wewe ni Mheshimiwa Spika wa Kimataifa na Mheshimiwa Spika wetu mwaminifu, naipokea Taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kuchangia. Uchaguzi ni tarehe 27 Novemba, niwaombe Watanzania wote wenye machungu na nchi hii kwanza wajitokeze kwa wingi kuchukua fomu, wale walio waaminifu kwa sababu, Katiba yetu inasema ni kusoma na kuandika basi, biashara inaisha. Hakuna cha Daktari wala *PhD,* wachukue nafasi tufanye kazi kuhakikisha kwamba, nchi yetu tunaitoa kwenye wimbi la umaskini na kuipeleka sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2025 Watanzania kwa sababu, Mheshimiwa Rais huku anafanya vizuri na hata sisi Wabunge wote 99.9% tunafanya vizuri. Wakati mwingine haipo sababu ya kubadilisha viongozi, tuendelee tu kuaminiana ili kusudi tuendelee kuitumikia nchi yetu kuhakikisha kwamba, tunaitoa ilipo na kwenda sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni-*copy* sera ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, ndiyo maana nimepokea Taarifa yake jamaa yangu. Kwanza, maendeleo hayana chama, lazima tuamini hivyo. Kwa hiyo, cha msingi tuangalie viongozi ambao ni waaminifu tu na familia za wezi zinajulikana ndugu zangu, kama kuna sifa za watu wezi hakuna haja ya kuwapa mamlaka. Hata kama wakiwapa pesa, kuleni pesa zao, halafu chagueni viongozi ambao watatutoa hapa tulipo, hapa tupo pabaya sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia mjadala wa Taarifa za Kamati za Bunge za *PIC, PAC* na *LAAC*. Nataka nianze kwa kudokeza kwamba, taarifa hizi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinapaswa zichukuliwe kama mtu anayejitazama kwenye kioo. Kwa nini, niweke mfano huu wa mtu anayejitazama kwenye kioo?

Mheshimiwa Spika, lengo la kujitazama kwenye kioo ni kuona iwapo una dosari, basi dosari hiyo iweze kurekebishwa na pia, kama kuna uzuri wowote unaouona kwenye kioo hicho, basi maana yake uweze kuuendeleza. Haitapendeza kwamba, upo mbele ya kioo na unajiona una tongotongo, nywele hujachana vizuri, vishikizo havijafungwa vizuri, lakini bado ukatoka hivyo hivyo. Kwa vyovyote vile anayekuona huko nje ataona mvuto wako siyo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa dhana hii ya kujitazama kwenye kioo katika ripoti ambazo zipo mbele yetu inawahusu sana Wakuu

wa Taasisi, lakini pia na watu waliopewa dhamana ya kusimamia utendaji Serikalini. Kwa nini, niseme dhana hii inawahusu? Ni kwamba mkuu wa taasisi kwa nini, usimamie taasisi ambayo inatengeneza hasara mwaka hadi mwaka? Nawe mkuu wa taasisi kama una dhana ya kujitazama kwenye kioo huchukui hatua ya kunusuru hali hiyo? Taasisi hizi ambazo zinaonekana zinaendelea kutengeneza hasara huku zikisubiri ruzuku kutoka Serikalini zitaendelea na mwendo huo hadi lini?

Mheshimiwa Spika, kama tunahitaji kupiga hatua za haraka za maendeleo katika Taifa letu ni lazima dhana hii tuiangalie na tuifanyie kazi sana. Anayejitazama kwenye kioo atajirekebisha, lakini inapokuja kwamba, ni mkuu wa taasisi, yeye ile ni ajira yake kwa hiyo, ni lazima kama anatengeneza hasara au kama malengo ya taasisi hayafikiwi, basi wale walio juu yake, waliompa dhamana hiyo wanapaswa wamwajibishe. Katika hili ninatoa hoja ya kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na Tume ya Mipango ya Taifa inayo sababu ya kuhakikisha kwamba, mashirika yote ya Serikali ambayo yanaendelea kutengeneza hasara mwaka hadi mwaka yanapaswa kuangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, mfano, kama mtendaji amepewa miaka mitatu na ndani ya miaka hiyo mitatu hatoi matunda, ana sababu gani ya kuendelea kukaa katika nafasi? Maana yake ni kwamba, ubunifu haupo, lakini pia, amekosa mbinu ya kuleta tija katika taasisi husika. Kwa hiyo, sioni sababu ya kwa nini mtu aendelee kukaa katika nafasi yake kwa miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumempa mwaka wa kwanza, labda anajaribu kujenga miundombinu, labda anajaribu kutafuta mbinu mpya, labda anajaribu kutafuta ubunifu. Miaka mitatu ni muda wa kutosha, kama ni mtu wa kutoa matokeo anapaswa atoe matokeo. Kwa hiyo, kwa jinsi hiyo inaonekana kabisa kwamba, *management* hiyo ime-*fail* na mtu anapokuwa ame-*fail* katika *management,* basi asiwe na sababu ya kutolewa taasisi moja kwenda kupeleka mbinu zilizo-*fail* katika taasisi nyingine. Huo ni mfano wa *management. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, *management* inayo sehemu kubwa sana katika ufanisi wa taasisi husika, lakini

yawezekana kweli, kwamba, mtu amepewa *management* miaka mitatu hakuleta tija, akapewa mtu mwingine miaka mitatu pia, haikueleta tija. Lazima turudi kuangalia kwamba, yawezekana tatizo siyo mkuu wa taasisi au *manager* anayekabidhiwa taasisi husika. Yawezekana kabisa kwamba, tatizo lipo katika mifumo ya uendeshaji isiyozingatia maslahi mapana ya Taifa na yawezekana ni mifumo iliyowekwa ambayo maslahi yapo kibinafsi, inayoendekeza rushwa. Kwa jinsi hiyo, taasisi hii sasa tunaweza tukaondoa tatizo la *management,* badala yake tukaangalia mifumo ya uendeshaji ambayo yawezekana watu wameshaweka mifumo ambayo ni kwa maslahi yao binafsi. Kwa hiyo, mifumo ya jinsi hiyo iweze kufumuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo mifano Dhahiri, napenda kutoa mfano mmoja, mwaka 2020, Shirika letu la Madini la *STAMICO* lilikuwa lifutwe kwa sababu, lilikuwa limetengeneza hasara ya shilingi bilioni 60, lakini kitendo cha kuweka *management* mpya, ndani ya miaka mitatu shirika liliondoka katika orodha ya mashirika yanayopaswa kufutwa. Badala yake shirika likatengeneza faida kiasi kwamba, sasa hivi halichukui mshahara kutoka Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo inaonekana kabisa kwamba, kumbe wakati mwingine kuna sababu ya kutathmini sana ni nani *Manager* wa kumpa taasisi ya umma. Ni ukweli ulio wazi kwamba, *management* inayo tija kubwa katika kuendesha taasisi za umma. Kwa hiyo, tuangalie sana habari za *management*. Pia, kama *management* itakuwa imeshindwa tuangalie mifumo ya uendeshaji kama imewekwa kwa maslahi ya ubinafsi iweze kufumuliwa, ili hatimaye tuwe na mashirika ambayo yataleta tija, ili Taifa letu liendelee kupiga hatua ya maendeleo na mashirika mengi ya umma yatengeneze faida, yasiendelee kutegemea ruzuku na wala yasiishi kwa sababu tu yanapaswa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze kazi nzuri ya Tume ya Mipango pamoja na Msajili wa Hazina kwa jinsi ambavyo wameendelea kuyatazama kuona ni yapi yenye tija na yapi ambayo hayana tija, ili tusiwe na mashirika ambayo yanaendelea kuchota katika kile kidogo ambacho tunapaswa kukifanyia maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye hoja nyingine ambayo pia, Wabunge wengi wameiongelea, madeni miongoni mwa Taasisi za Serikali na Wizara dhidi ya Wizara nyingine. Katika taarifa zilizowekwa mezani ni dhahiri kwamba, utaona taasisi moja ya Serikali inaidai taasisi nyingine ya Serikali. Pia, ajabu na kweli, yule anayedai kutolipwa na yeye mwenyewe anadaiwa mahali fulani.

Mheshimiwa Spika, sasa taswira inayojengeka hapa ni kwamba, Wizara moja, taasisi moja, imeamua kwa makusudi kuikwamisha Wizara nyingine na taasisi nyingine ya Serikali. Kwa sababu, kama mimi ninakudai na fedha zile ni kwa ajili ya kuendeleza taasisi niliyokabidhiwa na wewe hunilipi, maana yake ni kwamba, umeamua kunikwamisha na hii ni Serikali ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mifano michache katika taarifa iliyopo Mezani ya *PAC*. Mfano mmoja uliotolewa ni kwamba, *TPDC* inaidai *TANESCO* deni linalofikia Shilingi za Kitanzania bilioni 713, *TANESCO* ikidaiwa na *TPDC*. Sasa deni hili limekuwa likikua mwaka hadi mwaka, lisiporatibiwa vizuri ni nani ajuaye kwamba, miaka michache ijayo, litafika shilingi trilioni nzima ya madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari za deni kama hili zinakwenda pande zote mbili. Kwa *TANESCO* anaendelea kupata riba na kwa sababu, anadaiwa atashindwa kuendeleza miundombinu mipya, lakini *TPDC* naye atashindwa kufanya uwekezaji mpya.

Mheshimiwa Spika, mfano, mwingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia tu huo mfano mwingine.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mfano, mwingine ni mamlaka za maji mjini zinadai Taasisi za Serikali deni ambalo mwaka huu wa fedha limefikia shilingi bilioni 45, lakini limekuwa kutoka shilingi bilioni 14 miaka mitatu iliyopita. Wakati mwingine mamlaka zinazodaiwa ni zile

ambazo unaogopa kuzidai, lakini haipaswi kuwa ndio dhamira ya kwamba, ninakupa huduma ya maji, halafu shilingi bilioni 45 zinakuwa deni kutoka Taasisi nyingine za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulienda Babati, kama Kamati ya Maji, shilingi bilioni 12 zilitengeneza mradi mkubwa wa kuhudumia mji mzima wa Babati. Hapa tuna shilingi bilioni 45 ambazo zinatengeneza miradi kama hiyo mitatu, lakini ni deni kutoka Taasisi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kama umewasha *mic*. Nimalizie kusema kwamba, ninapenda kuunga mkono hoja zote ambazo zimewekwa na kamati zetu. Tungetamani kwamba, ndani ya Serikali kwa sababu, wote tunapewa *OC,* huduma ya maji, huduma ya umeme tunatumia kwa ajili ya ufanisi wa taasisi zetu, tulipe madeni ili tuweke pia, kielelezo kizuri hata kwa yule raia. Raia anakatiwa maji, kwa nini yeye hakatiwi? Kwa sababu ni Taasisi ya Serikali? Si na yeye akatiwe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati tuliongelea habari ya mita janja kwamba, Wizara inataka kuleta mita janja. Ninapendekeza kwamba, zile mita janja ambazo unatumia kadiri unavyopata huduma zianze katika taasisi hizi sugu, maana zipo na nyingine, zile zinazoogopwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, atafuatiwa na, ama wewe ulitajwa kabla?

Haya. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay na Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nitaanza kwa kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuendelea kupiga miguu yote, kimsingi unatuheshimisha sana na unatu-*inspire* sana. Unapiga miguu yote *back-to-back;* Mbeya Mjini pale, hapa

Dodoma, lakini pamoja na Geneva na duniani huko kote. Kwa kweli, unaendelea kuonesha *you mean business.* Kwa hiyo, nikupongeze wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, niwapongeze Wajumbe wa Kamati tatu ambao wametoa taarifa zao kuhusiana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Kamati yetu ya Bunge ya *PIC,* Kamati yetu ya Bunge ya *PAC* pamoja na Kamati ya Bunge ya *LAAC*.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, ukisoma hizi taarifa kwa watu wanaojua kazi nzuri ukisoma unakuwa *excited.* Kuna *feeling* fulani unaipata unaona kabisa kwamba, hawa wamejitolea, wana uzalendo na wana ari ya kutumikia nchi yao. Taarifa zimeshiba kiasi kwamba, unashindwa kuelewa shida ni nini. Waheshimiwa Wabunge wenzetu wametuwakilisha sisi ambao hatupo kwenye Kamati hizo, lakini wamefanya kazi ambayo sisi wenyewe tunakubaliana kwamba, wenzetu wametuwakilisha vizuri. Kwa hiyo, niwapongeze sana pamoja na Wenyeviti wote ambao wamesimamia kazi hiyo kufanyika usiku na mchana. Tunajua wengine walikuwa wanakaa muda mrefu mpaka wanakesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza mchango wangu katika Taarifa ya Kamati ya *LAAC* kuhusiana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Pamoja na pongezi za jumla, nimpongeze Mheshimiwa Halima James Mdee, *one of the best MPs,* ambaye pia ni *Senior MP* kwenye hili Bunge. Kimsingi kuna watu kabisa ukitaka kuchangia lazima ukatafute michango ya nyuma ya Mheshimiwa Halima pamoja na *Hansard* za Bunge, ili kuku-*inform* kuna vitu ambavyo alivizungumza na kimsingi Uenyekiti wa hiyo Kamati wala hawajakosea kumpa, nimpongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia hiyo taarifa, pia, nimepitia Taarifa za *CAG* za miaka mitatu nyuma mfululizo tukiwa kwenye Bunge hili, lakini pia na taarifa za Kamati kwenye mambo kadhaa ambayo tumekuwa tukishauri. Mambo ni mengi ambayo yanaelezwa kwenye Taarifa za *CAG,* lakini wote tunayajua kwa sababu, wote tunayapitia na kuna namna yanatuudhi. Kuna

maudhi kwa sababu, nchi hii ni kubwa sana na Watanzania wana changamoto nyingi za huduma za kijamii, wana changamoto nyingi ambazo sisi tunaotokea vijijini huko tunajua. Sasa ukisoma taarifa unaona namna ambavyo kuna *gap* kubwa katika utendaji, kwa kweli zinaumiza na hata watu wetu huko wanatuuliza.

Mheshimiwa Spika, hoja zangu zitakuwa mbili na nafasi ikibaki nitachangia ya tatu. Nitachangia kwenye upande wa uwezo wa Halmashauri zetu katika kukusanya mapato, uwezo wa Watendaji wa Halmashauri zetu, pamoja na matumizi sahihi ya fedha za umma. Hoja ya pili, itakuwa katika mikopo ya 10% ya Halmashauri na nafasi ikibaki nitachangia hoja ya tatu, kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa ya *LAAC* na ukifuatilia mijadala ya Wabunge humu Bungeni, pamoja na taarifa za Kamati miaka mitatu nyuma, unaona namna ambavyo kuna hoja zinazungumzwa na Wabunge mfululizo, wakitoa *case study*, wakitoa na matukio halisi ambayo yanaripotiwa kwenye taarifa hizi namna ambavyo tuna changamoto katika Halmashauri zetu. Ni nyingi ambazo tukianza kutaja hapa kila *case study* katika kila Halmashauri utaona kwamba tunahitaji *reforms* za hali ya juu katika zile *4R's* za Mheshimiwa Rais, mwone namna ambavyo tunaweza tukashauri ili eneo kubwa ambalo zitafanyiwa *reforms,* Halmashauri zifanyiwe *reforms*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna hoja moja ya kufanya Wakurugenzi wa Halmashauri kuwa na mfumo maalum wa kuwapata. Siyo tu kwamba umeharibu Halmashauri 'A' umepelekwa Halmashauri 'Z', na kwamba kuna mchakato fulani ulifanyika huko na ikaonekana kwamba hebu mmpeni hiyo nafasi. Tuzichukulie Halmashauri zetu kama kampuni.

Mheshimiwa Spika, hivi Wabunge ambao ni wafanyabiashara au taasisi na makampuni binafsi ambao wanaendesha kampuni zao, hivi ukikabidhiwa kama Serikali inapeleka ruzuku pale na ukaambiwa hebu bangua bonge, hebu *brainstorm*, hebu chakata, hebu buni, hebu *create*, tafuta namna ambavyo tunaweza tuka-*maximize* hiyo ruzuku ambayo

tumekupa tunaweza tukatumia hicho kidogo ambacho sisi tunakupa, hebu ongeza akili yako, halafu hakikisha Halmashauri yako inatengeneza vyanzo vipya vya mapato, kuna shida kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna zile Halmashauri ambazo zimefanya vibaya sana. Napongeza Halmashauri yangu ya Ikungi, Mkurugenzi wetu anapambana, anajitahidi, yaani naweza nikasimama hapa kifua mbele, unaona namna ambavyo anatamani mambo yaende. Sasa watu wa mjini, watu wa Dar es Salaam ukiangalia huku mpaka unashindwa kuelewa huku mjini kuna nini? Kama kuna wezi zaidi huko, na ni kitu ambacho unashangaa! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ngoja niwaambie, kwa sababu tunasema tunataka tufanye *reforms* upande wa Halmashauri kwa sababu kuna watu wanatuangalia huko wanatuona sisi ni kama *jokers*. Hili neno ambalo huwa nalitumia, kwa sababu ukifuatilia michango ya humu ndani na taarifa tunazozitoa, yaani ni zile zile kila mwaka, tunaongea vilevile.

Mheshimiwa Spika, najiuliza, hivi ninyi kama mkitangaza ajira za Halmashauri za Wakurugenzi, watu wakaomba ajira, wakafanyiwa *vetting* na mtu akaja akakuelezea, eeh, tumekupa kiasi fulani, tunataka ufanye moja, mbili, tatu na tutakupima kwa moja, mbili, tatu na ukishidwa unatoka. Hata kama mnataka kuwaweka watu fulani ambao ni makada niseme, kwa sababu mwisho wa siku ndiyo hiyo inakuwa hoja *sometimes.* Wapo watu ambao wana uwezo, basi wapeni hao.

Mheshimiwa Spika, mtu akishajua kwamba *key performance indicators* ni moja, mbili, tatu, ata-*perform* na akishindwa maana yake una haki ya kumtoa kwa sababu kashindwa mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijana kwenye hii nchi, wengine jamani ni *graduates* wapo huko mitaani wana uwezo kiasi kwamba mtu anakwambia, yaani Halmashauri wanapewa kiasi hiki, mbona tunaweza tukafanya moja, mbili, tatu! Ukiwa *open minded* unaweza kuona namna ambavyo kuna *potential* kubwa kwa Watanzania, wanafikiri wana uwezo wa kubuni, akili zao

zinafanya kazi, Watanzania wamezaa watoto wenye uwezo, wanaona kama sisi tunatania kwa sababu tunafanya *business as usual. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kuna moja ya hotuba alizungumza kwamba anafikiri tuanze kutoa mikataba kwa watendaji. Nafikiri ni kitu kama hicho. Nilifurahi kwa sababu mamlaka inaanza kuzungumza hiyo lugha, nawaomba sana washauri wa Mheshimiwa Rais. Tunaomba katika eneo moja tu, maeneo mengine aache. Afanye *reforms* kwenye Halmashauri tu, tuwapime wale watu, tuwachague kwa uwezo wao, tuwape hizo nafasi, nafasi nyingine za uteuzi wapewe Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, hizi nyingine ambazo tunahitaji tupate mapato jamani, mimi natoka kijijini, wananchi wangu wa Kikio, Misughaa kule Singida Mashariki, Dung'unyi, Choda, Mkiwa na Ikungi wanahitaji hizo fedha ili tukapeleke vitendanishi na vifaatiba akina mama wajifungulie sehemu ambazo kuna mazingira mazuri ya hospitali.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa mazingira ya shule, walimu wa kutosha, vifaa vya kufundishia na kujifunzia shuleni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wengi wakizungumza kuwa kuna mabilioni ya fedha, sisi tuliopo kule kwa wananchi tukiona mabilioni ya fedha yanapigwa, wale watu wangu wa kule Mungaa hawawezi kunielewa. Ndiyo maana tunazungumza hivi. Tunaomba mfanye kweli *reforms* kwenye upande wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake ya *LAAC* wamezungumzia kuhusu 10% ya mikopo ya Halmashauri, na inasikitisha kwamba bado makusanyo marejesho ya zile shilingi bilioni 79.69 bado hazijarudi mpaka leo. Tunapanga kurudisha mikopo ya 10% ya Halmashauri, nami natamani iwe hivyo kwa sababu katika zile 4:4:2 kuna wananchi wangu kule nao watafaidika.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ni lazima tuwe na mikakati madhubuti ya kurudisha hizo fedha, kwa sababu haiwezekani

tukawa tunajipangia kufanyia 'A' tunafanya vitu vingine ambavyo siyo tulivyojipangia, halafu inakuwa ni kama unalima, nyuma majani yanaota. Kabla hatujaenda huko, kwanza tuone mikakati ambayo ina-*inform* kwamba zitarudije hizo ambazo hazijarudishwa mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, halafu watu wa Dar es Salaam mimi nawashangaa! Narudia tena, Dar es Salaam, Kinondoni, Ilala, Temeke, Kigamboni wanadaiwa. Yaani wanadai fedha nyingi, wanashindwa kukusanya; yaani watu wa mjini, sisi watu wa huku ambako hakuna hata *internet* kuna changamoto tunashidwa kuelewa ni nini shida? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba sana, kuna mapendekezo ambayo Kamati wametoa ambako tunakwenda sasa hivi kurudisha mikopo 10%. Kwanza ni jambo zuri, *especially* kipindi hiki tunachoelekea kwenye uchaguzi, tunajua haya mambo yanavyoenda, lakini kabla, kuna mambo ambayo wameyapendekeza pamoja na vigezo vya utoaji wa hii mikopo wameyaeleza pale, nami nayarudia kwamba, basi vile vigezo kabla ya kwenda huko tuhakikishe tumevifanyia kazi ili tuwe na tija. Bila hivyo, tunakuwa tu tumeitaja kwenye makabrasha huku, kuwa tunarudisha mikopo 10% lakini tutarudi tena hapa.

Mheshimiwa Spika, tufanye *piloting* jamani, sisi roho zinauma kwa sababu tunajua kwamba tuna *cake* ya Taifa ndogo na tunatamani tugawane. Mheshimiwa Rais anapambana sana kutafuta fedha nje, lakini sisi kama hatupambani humu ndani kuishi, yaani tunakuwa sijui tunafanya nini? Kwa kweli mimi wakati naomba hata Ubunge, hivi vitu ndivyo ambavyo nafikiri kwenye kuvifanya, kwa sababu mimi ni *Social Development Enthusiast,* natamani mambo yaende. Ifike hatua tulijadili moja, tuseme tutafanya moja, mbili, tatu; tumefanya tumemaliza, tunaenda sita, saba, nane, hivyo. Siyo kila siku tunarudi tu *business as usual.*

Mheshimiwa Spika, wengine tunahitaji sana utumishi kuliko hizo nafasi, yaani utumishi zaidi kwa watu, kwa sababu nataka siku nikikaa niseme nilifanyia nchi yangu moja, mbili, tatu. Kwa hiyo, naomba tusaidiane. Kwa bahati nzuri, Waheshimiwa

Wabunge kwenye hizi taarifa za *CAG* Bunge tunashirikiana sana, unaona kabisa watu wanaongea *sense* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa wivu mkubwa na Bunge lako, kwa sababu wewe pia ni Mbunge, na najua ungekuwa umekaa kwenye hivi viti, nawe ingekuwa humu kunawaka ukichangia, kwa sababu tunajua na wewe ni *brain* nzuri.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, kwa sababu naona hapa bado nina nafasi kidogo, nipo kwenye Kamati ya Elimu. Tumekuwa tunazungumza mara kadhaa, kuna Mfuko wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, tunaomba Mfuko wa Mikopo wa Elimu ya Juu uwe na *special vote* yake peke yake usiunganishwe kwenye Wizara ya Elimu ili ujiendeshe kama *revolving fund.*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi, pamoja na kwamba namba zime-*increase,* nitaongea zaidi tukienda huko kwamba tumeongeza namba ya kutoa mikopo, lakini bado ni 70% hatujafika 100%. Ikiwa *revolving fund* maana yake wanakuwa wanajua kabisa Serikali ikipeleka ruzuku kiasi fulani, ile ijiendeshe pale, wawe na uwezo wa kukusanya. Wanaweza kufanya *investment,* wakawekeza kwenye bondi, wakawekeza maeneo mbalimbali wao kama mfuko, itatusaidia kujipima na inawezekana ikawa mfano katika taasisi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamani naomba sana tusifanye nchi yetu kama shamba la bibi. Kuna watu huku watakuja kupiga mawe makaburi yetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja za Kamati zote tatu; *PIC*, *PAC* na *LAAC*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mheshimiwa Mohamed Said Issa ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Nianze kwa kuzipongeza Kamati hizi zote tatu; Kamati ya *PIC, PAC,* na *LAAC*. Pia nampongeza *CAG* kwa kweli kwa ripoti ambayo kimsingi ameiandika hapa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ripoti ya mwaka 2023 aliyoandika *CAG* na miaka mingine iliyopita, amejaribu kutusaidia kutuonesha maeneo ambayo kimsingi yana tatizo. *CAG* ni jicho na maneno waliyoyaeleza Wenyeviti wa Kamati hizi tatu zimeeleza kwa ufasaha sana na ukizingatia maeneo mengi ni Bunge letu, sasa tunatakiwa kulisimamia na kuona kwamba haya ambayo yanaonekana tumeyaeleza hapa yakasimamiwe na utekelezaji wake uje hapa ili nchi yetu ya Tanzania iende mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi? Nasema hivi kwa sababu ukiangalia Kamati ya *PIC* imeonesha mashirika haya 309 lakini mashirika machache yameonesha jinsi ambavyo yanaendeshwa kwa hasara. Mimi ni Mjumbe wa *PIC,* lakini pia ukiangalia mashirika haya, kimsingi yanaonesha hapa yanaendeshwa kwa hasara. Nini maana ya hasara? Nafikiri inafahamika.

Mheshimiwa Spika, nashauri, kwa mfano, *TTCL*, *TPDC*, *NARCO* na mashirika mengine ambayo yametajwa, ili nisichukuwe muda, nataka nioneshe tu jambo ambalo kwa kweli Kamati pia hairidhii kwa sababu moja kubwa. Hasara inayopatikana hapa ni kubwa kwa sababu mashirika mengine yanapewa ruzuku na Serikali. Sasa unapewa ruzuku halafu wewe huonyeshi faida. Maana yake ni kwamba unaliingizia Taifa hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri kwamba mamlaka zinazohusika na hawa viongozi wanaochaguliwa kuendesha mashirika haya ni vizuri ikaangalia kama kuna shida iliyopo hapa ya kiongozi, basi kifumo ibadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati tulileta mapendekezo ya hawa Wakurugenzi wanaochaguliwa kwenye mashirika kuyaongoza waje wakiwa wanakwenda kuomba kazi na wapewe kazi kutokana na historia yao ya kufanya vizuri katika maeneo fulani. Ukiangalia Kamati nyingi hizi, sitaki kubeza umri wa

mtu, lakini kwa kweli Wenyeviti wa Bodi za hizi Kamati pia sitaki kuwasema sana, lakini nieleweke tu, wengi wao wamestaafu kazi. Ssa mimi nahoji kidogo, huku kustaafu kazi ndiyo kunasababisha mambo haya? Inawezekana siyo, lakini hebu tupeleke watu ambao wanaweza kufikiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina shida ya kuonesha kwamba labda ukistaafu huwezi kazi, Hapana. Hebu tupeleke damu mpya kwenye maeneo haya tupate faida, kwa sababu ukiangalia kimsingi, napata shida nikisikia shirika kubwa limepewa fedha, lakini halifanyi vizuri. Kwa mfano, ukiangalia *TTCL,* nalipenda sana shirika hili na hata kule kwangu minara ipo kila mahali, lakini jambo moja tu dogo unashangaa wameshindwa. *TTCL* watu wengi wanalipenda lakini hata vocha kule kijijini mahali pa kuipata ni kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria, jambo dogo la vocha kupata kijijini imekuwa kazi, lakini vocha ya *Airtel* inaeleweka, Voda inaeleweka, lakini *TTCL* kwa Mtanzania wa kawaida ambaye hana *Airtel money,* kuipata *physically* haiwezekani, lakini utaona wenzetu wengine wanafanya kazi kibiashara. Kwa hiyo, ushauri wangu upo katika suala hili la mashirika ambayo kimsingi yanaleta hasara kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusemea eneo lingine la madeni. Yapo madeni yameoneshwa na *CAG,* ni fedha nyingi sana. Yapo madeni kwenye Serikali za Mitaa, lakini yapo madeni kwenye taasisi zetu za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, Mheshimiwa Rais amewahi kusema kwamba mifumo isomane. Ukiangalia madeni yanayotoka kwenye shirika hili la maji, ukiangalia madeni ya *TANESCO* kwenda kwenye maji, utadhani hawa ndugu zetu hawaelewani, lakini kimsingi ni mashirika haya ya kwetu na taasisi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hebu angalia, kwa mfano bili ya maji anatakiwa kulipa nani? Huyu wa maji, anatakiwa kumlipa *TANESCO*, *TANESCO* wanatakiwa nao wa-*link*. Sasa unakuta hapa

wangeelewana tu. Hii ni Serikali na wapo pamoja, waelewane ili baadaye wasitupe kazi ya sisi kuona tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano unaweza kukuta kuna mradi wa maji labda upo eneo 'A', wanadai wapelekewe maji labda kwa shilingi milioni 70, lakini inaonekana mradi unachelewa kwa sababu tu hiyo hela sasa haiendi kufanya kazi. Huyu anamdai yule, na yule anamdai huyu. Nadhani kuna sababu ya kuangalia kutunga sheria na kanuni zitakazowalazimisha hao ndugu kulipa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni mikopo hii ya 4:4:2. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ameiruhusu mikopo na ndugu zetu kule kijijini wanapata mikopo hii ya 4:4:2, hasa wanawake na walemavu.

Mheshimiwa Spika, nimefanya vikao vya wananchi kule vijijini, lakini nilikuwa najaribu kushawishi hata Wabunge wenzangu waelewe kwamba hii 4:4:2 ni nzuri, inafanya kazi vizuri na watu wanakopa na kurudisha bila riba, lakini kuna kundi tumelisahau.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali imeongeza ule umri wa vijana kwenda miaka 45. Sasa kuna mtu ana miaka 46, mwingine 50, nami naomba kabisa na Waheshimiwa Wabunge wanielewe. Tuongeze eneo lingine la wazee wapate mkopo huu kwa sababu ukiangalia, nini maana ya mkopo wa 4:4:2? Ni makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Sasa Halmashauri zote zinakusanya kodi, na pia unapokusanya, maana yake unakusanya kodi kwa kila mtu. Wanakusanya kwa mwanamke, kwa kijana, na pia kwa mwanaume. Sasa kwa nini tunamwacha huyu mwanaume tu ambaye ni mzee? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu kubwa ni kwamba tuanze kuelewana tu. Wazee wanaanza kutuuliza kijijini kule, inawezekana ukaona wazee wengi ni *pensionable*, ni kweli kuna wazee wengine ni *pensionable,* ni watumishi wa Serikali, wamekaa nyumbani, sasa hali yao imekuwa ni ya kulipwa mafao yao. Pia kuna wakulima wengine hawana mahali pa kuweza kukopa hiyo mikopo. Ni kwa nini nao tusiwawekee?

Mheshimiwa Spika, napendekeza siku moja Waziri aje aone sheria hiyo tuibadilishe hapa, tuweke mbili, au 3:3:2:2, au tuje tuanzie 4:4:4 au 4.4.4.2.2 yaani tuweke mtu ambaye ameenda umri hasa, mzee. Hali ya vijijini kwa watu wetu ni mbaya. Ukifika kwenye vikao vya hadhara, wanauliza, wazee mikopo yao vipi?

Mheshimiwa Spika, nadhani hii Kamati kwa namna yoyote itoe maelekezo tuone namna gani ya kufanya. Vile vile Serikali ione namna gani ya kuwaingiza hao wazee? Wapo wazee wanahitaji mikopo, nami naomba niseme kwa niaba yao kwamba, mami na wewe ni wazee watarajiwa, kwa hiyo, inawezekana kabisa tukawa wazee, lakini pia tukawa tunahitaji mikopo hii, kwa sababu mikopo hii ni mizuri, unarudisha bila riba. Kwa hiyo niliona niseme hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Halmashauri zimetajwa hapo ambazo hazifanyi vizuri, zimepata hati yenye mashaka, lakini pia hazikusanyi mapato. Nazishukuru sana Kamati zimeonesha hapa, hasa ile Kamati za kiuchunguzi ya *LAAC*. Halmashauri isiyokusanya na ina madeni nadhani tuiangalie. Hizi Halmashauri hasa za mijini ni maeneo ambayo tunatamani fedha zikusanywe zipeleke kwenye Mfuko Mkuu ili maendeleo yaende. Sasa usipokusanya maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za wenzetu, huwezi kuacha kodi. Kodi ni kitu cha kwanza, ndiyo inasaidia nchi na maeneo mengine ya miradi kuendelea. Kwa hiyo, nashauri, kwa kweli maeneo hayo tuwe makini na tuamue kuona kwamba maeneo haya hawa wachukuliwe hatua za kinidhamu. Hii inaonesha kwamba katika hali hii pia Serikali haipendezwi na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema haya? Nasema haya kwa sababu zipo Halmashauri za kijijini ukiziangalia, kwa mfano Halmashauri yangu ya Mbulu imekusanya zaidi ya 110%. Sasa kwa nini hizi za mjini zisikusanye na kuna mifumo na kila kitu? Halmashauri ya Mbulu ukiangalia mapato yake siyo mengi, lakini kwa jinsi ilivyopangiwa, tumekusanya zaidi ya 110%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina maana ya kuwakebehi hawa ndugu zangu wa mjini, hapana, nataka waone kama kukusanya mapato

ni suala la hakika na ni kazi ambayo imewekwa pale na Mkurugenzi na watu wake, waone namna gani ya kukusanya haya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati zote. Nimezisoma kwa makini sana, lakini nilikuwa nashauri, pamoja na haya, yapo maoni ya Kamati hizi tatu yaliyopita mwaka 2023, na maoni haya mengine hayakufanyiwa kazi. Sisi kama Bunge, tuone pia yale maoni ambayo hayakufanyiwa kazi, nini kinafanyika baada ya hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapa, ombi langu ni kwamba, kwa kuwa *CAG* kuna maeneo ameyasema mara nyingi na kila mwaka anasema hivi hivi, Serikali sasa ichukue hatua kali kwa maeneo yanaonekana yana ubadhirifu na maeneo ambayo yameonekana yana shida, lakini pia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, naona kengele imegongwa. Nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said Issa, na Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika ripoti hizi tatu ambazo zimewasilishwa na Wenyeviti wetu hapa wa *PAC*, *PIC* na *LAAC*.

Mheshimiwa Spika, napenda kujikita kwenye ripoti ya *LAAC* ambayo ni sehemu ya maisha yetu ya kila siku, pia kama wananchi, na sisi kama viongozi kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze na kipengele cha watumishi, hapa ambapo inaonyeshwa kwamba kuna takribani shilingi bilioni 11.42 haijalipwa kama malimbikizo kwa watumishi wetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumza, naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia, mama yetu ambaye ameweza kupunguza shilingi bilioni 42 kwenye malimbikizo haya ambayo ni sawasawa na 72% ya madeni ya watumishi ambayo yalikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtumishi kulipwa stahiki zake ni haki yake ya msingi kabisa. Kumekuwa na changamoto kubwa ya ulipaji wa malimbikizo kwenye baadhi ya halmashauri zetu ambapo mtumishi kulipwa stahiki yake inakuwa kama ni *favor*, yaani ni kitu cha upendeleo, kitu ambacho siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kufuatilia madeni haya yaliyobaki, unaweza ukakuta ni ya wale watumishi wa chini. Wale wote wa juu juu; Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo na Wakurugenzi, hawana madeni kwenye maeneo haya. Chanzo cha madeni haya ni pamoja na ajira mpya, uhamisho, kupandishwa madaraja, kukaimu nafasi za ukuu wa idara na nyongeza za mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite kwenye eneo la kukaimu nafasi za ukuu wa idara. Ripoti hii imeonyesha nafasi za Wakuu wa Idara, wengi wanakaimu kwenye baadhi ya halmashauri, lakini kuna halmashauri ambazo zimeshakaimisha wakuu wa idara wengi na hadi leo hawajalipwa stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ifikie hatua Serikali iwe na *standards* za kwamba mtu akidai kwa muda fulani anatakiwa alipwe. Yaani isizidi muda fulani mtu akawa anaidai tu Serikali wakati wote. Kwa hiyo, naomba kwa wale wakuu wa idara ambao hawajalipwa fedha zao za kukaimu, wakati mwingine Serikali upande wa utumishi wanawaachia halmashauri, wanakaimisha, halafu mtumishi anapoenda kudai, wao wanasema kwamba ulikaimishwa na halmashauri, sisi huku juu hatukutambui, kwa hiyo, waambie halmashauri wakulipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaratibu wa kukaimishwa tunaomba uendelee kuzingatiwa na usizidi ule ukomo wa muda

wa kukaimu kwa mtumishi yeyote. Kwa hiyo, hilo nilitaka nichangie kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia, nataka nizungumzie kwenye makato ya kisheria kutokuwasilishwa kwa taasisi husika kwa wakati. Tunaona kuna deni ambalo lipo kwa baadhi ya halmashauri, ambalo ni shilingi bilioni 306.09 ambazo halmashauri zinadaiwa na mifuko ya *PSSSF, NHIF*, malipo ya kodi, Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ndani ya deni hili, deni halisi ni shilingi bilioni 4.013 peke yake, ambalo hii shilingi bilioni 4.013 ndiyo imesababisha kupata riba ya shilingi bilioni 32.075. Sasa nawaza ni riba ya kiwango gani hii inayoweza kuzalishwa kutoka kwenye shilingi bilioni nne? Ni asilimia ngapi ya riba ambazo hizi halmashauri zetu zinapaswa kulipa kwa kila faini inayokuwa imepigwa kwa ucheleweshaji wa fedha hizi? Katika hali halisi, unaona kabisa hakuna uwiano wa riba na deni kwenye hizi halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali inapokuwa inalipa mishahara, mimi nafahamu inalipa mshahara kwa stahiki ya mtumishi pamoja na makato yake ambayo halmashauri inatakiwa ichukue sehemu ya hizo fedha ipeleke kwenye mifuko. Kwa hiyo, uzembe unaotokea wa kutokulipa haya makato kwenye taasisi husika ni kosa la mtumishi ambaye huenda amebadilisha matumizi ya hizi fedha au amezembea kutokupeleka kwa wakati au sifahamu ni changamoto gani nyingine inaweza ikawa imemkumba. Kwa kosa hili, mzigo tunabeba sisi wenye halmashauri zetu. Unaponiambia mimi halmashauri nikalipe fedha hizi zote, unanionea mimi mwananchi.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili, kosa la mtumishi ambaye hapeleki fedha kwa wakati, naomba lifungamanishwe na mtumishi mwenyewe. Sisi halmashauri kuwekewa mzigo kama huu inakuwa siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia kwenye Halmashauri ya *Shinyanga DC*, unaambiwa walishindwa kupeleka shilingi milioni 238, wakapata faini ya shilingi bilioni 45.714. Najaribu

kuwianisha, kwanza kwa vile mimi siyo mwenyeji wa Shinyanga, lakini najaribu tu kupata picha kwamba hiyo Halmashauri ya Shinyanga ina kipato gani cha kuweza kulipa fedha yote hii? Hili deni linavyoendelea kuwepo kule, linamnyima haki mtumishi ambaye alipaswa alipwe mafao yake kwa wakati. Je, Halmashauri hii ya Shinyanga italipa hizi fedha? Je, inazo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natamani kuwe na uhalisia wa madeni ambayo tunaletewa hapa kwenye ripoti, kwamba, deni hili kwa halmashauri hii litalipika au linapaswa kuondolewa. Kwa hiyo, hili pia niliona kwamba siyo sawa kwa baadhi ya halmashauri zetu. Huu mzigo wa wananchi, sisi kwa kweli nikiwa kama sehemu ya wananchi, naomba Serikali yetu iweze kutazama kwa uzuri ili kupungumza mzigo usio wa lazima kwa wananchi kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningependa kukiongelea ni kuhusiana na miradi kutokukamilika kwa wakati. Serikali inapokuwa inabuni miradi, nadhani inakuwa imejipanga kulingana na *flow* ya fedha yake itaenda vipi? Kama hawana mpango wa *flow* ya fedha ya kupeleka kwenye miradi hii, bora wasianzishe huo mradi.

Mheshimiwa Spika, sioni umuhimu wa Serikali kuanzisha mradi ambao utachukua miaka 10 ilhali wangeweza kuanzisha miradi michache ambayo kwa fedha hiyo hiyo ndogo aliyonayo ikaisha na hiyo miradi ikaanza kufanya kazi kwa wakati na ikaingiza fedha ya kuzalisha mradi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye halmashauri zetu huko kuna miradi mingi ambayo imekwama. Ukiangalia kinachokuja kutokea ni kwamba matumizi ya fedha unakuta wakati mwingine yanabadilishwa. Kwenye ripoti hii tumeonyeshwa kwamba kuna fedha shilingi bilioni 7.73 ya miradi ya maendeleo ilibadilishwa matumizi. Sasa unawaza kwamba, kama fedha ilikuja kwa kazi fulani inakuwaje Mkurugenzi awe na ujasiri wa kubadilisha fedha ya miradi ya maendeleo ya wananchi kwenda kwenye matumizi mengine?

Mheshimiwa Spika, sijawahi kuona fedha ya *OC* ikibadilishwa kwenda kwenye maendeleo. Kwa hiyo, ifikie hatua kama Bunge tuwe wakali kwa watu wanaobadilisha fedha zetu za maendeleo kwenda kwenye matumizi mengineyo kwa sababu wanakuwa na bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiukweli kumekuwa na baadhi ya Wakurugenzi ambao ni wabinafsi sana. Wao wanapokuja pale wanawaza kujilimbikizia fedha. Kwa hiyo, fedha yoyote inayokuja kwenye halmashauri, wanaangalia namna ya kuifanyia utaratibu waweze kuitumia wao kama wao. Kwa hiyo, naomba pia kuwepo na adhabu ya Mkurugenzi au mtumishi ambaye anashindwa kupeleka fedha ya maendeleo kwenye miradi yetu ya maendeleo ili miradi iweze kuisha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pia, kumekuwepo na wizi. Nasema, mimi sio muumini wa *Force Account*, kwa sababu gani? Watu wananunua bidhaa, zinabaki zinazagaa, mwisho kila mtu anaanza kujichukulia kidogo kidogo. Kumekuwa na baadhi ya maeneo tunaona kabisa *cement* iliyonunuliwa inaganda, *cement* inayonunuliwa labda mwingine mifuko mingine anachepusha. Kwa hiyo, vitu kama hivyo inakuwa siyo sawa kwa miradi yetu. Ndiyo maana unakuta inakwama, inashindwa kutekelezwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, kumekuwa na usimamizi usio toshelevu. *Imagine* Mkurugenzi anakuwa na miradi mingapi kwenye halmashauri, ambaye huyo anakuwa na Wakuu wake wa Idara, ambao wanasimamia hiyo miradi mingapi kwa ufanisi; na je, hao watu wana huo utaalam wa usimamizi wa miradi hiyo? Kwa hiyo, unakuta wale wasimamizi wa miradi wanaopaswa kusimamia, hawafanyi kazi yao sawasawa. Kwa hiyo, hilo la usimamizi wa miradi, niseme nalo halijakaa sawa, na watusaidie kuweka watu wenye utaalam wa kusimamia miradi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho zaidi niongelee kwenye mikopo ya wanawake ambayo nayo imekuwa changamoto. Tunaomba kuwe na idara au kitengo maalum cha utoaji wa mikopo. Huwezi ukampa fedha Afisa Maendeleo ya jamii useme

akazikopeshe, aifuatilie na aweze kukusanya, siyo kweli. Hizi fedha zinazopotea takribani shilingi bilioni 79 ambazo hazijarudi, ni kwa sababu waliopewa dhamana ya kutoa mikopo siyo wataalam wa hiyo idara. Kwa hiyo, naomba kuwepo na wataalam au kitengo maalum chenye wataalam wa utoaji wa mikopo kwenye halmashauri zetu, nadhani tunaweza tukafanya vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Said Issa. Atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja ambazo zipo Mezani.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuzipongeza ripoti hizi tatu za Kamati zetu ya *PAC, PIC* na *LAAC*. Kwa kweli nimesoma zote na nimeona kwamba wamefanya kazi nzuri. Wamefanya kazi ya Bunge, sasa kilichobakia ni sisi Waheshimiwa Wabunge kuongeza tu kidogo maneno ili mwisho twende na maazimio ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, sitaki nielezee yote yaliyomo kwenye mchanganuo wa Kamati hizi, ama ripoti ya *CAG,* ila nitatoa tu mfano, na sitaki hata nichukue muda mwingi.

Mheshimiwa Spika, nimesoma hapa katika Ripoti ya *PAC*, nimeona kwa upande wa *TRA CAG,* aligundua miamala 238 ambayo haikupita katika mifumo. Hii tena ipo kwenye sehemu za *border* tu siyo kwenye bandari. Ni *border* tu, kama vile Kasumulu, Rusumo, Mutukula na sehemu nyingine. Sasa kama tunachezea chezea fedha hizi za Serikali ambazo wananchi wanalipa ili wapate huduma muhimu, tutafika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunasema kwamba nchi yetu inakusanya, lakini kuna watu wanasema wakipewa ile bandari tu, wanaweza wakahudumia Afrika nzima. Sasa kwa nini sisi tunalichezea hili, kwamba hatuyafanyii kazi haya maneno? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili lazima sisi kama Bunge tuje na maazimio makali. Nimeona hapa, kwa mfano kwenye uingizaji wa mafuta yale ya *transit* ambayo yanakwenda nchi za nje, lita 1,100,000 hazikutoka nchini, lakini pia zinaonekana zimefanyiwa *process za custom*. Hii kwa mwezi mmoja tu hasara iliyopatikana fedha hizi ni shilingi 9,296,000,000 yaani inamaanisha kwa mwaka mmoja ni zaidi ya shilingi bilioni 111. Fedha hizi zingekwenda kwenye vituo vyetu vya afya na kwenye shule, tusingekuwa na shida ya kulalamika kwamba watoto hadi leo wanakaa chini. Lazima mwisho wa mjadala huu maazimio yetu yawe makali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia alipoulizwa Kamishna wa *TRA* alisema, wanakiri kwamba tisa walikuwa na shida, na hatua alizozichukua ni kuwabadilisha. Sasa tujiulize, ni hasara kiasi gani waliweka? Au adhabu yao ni kuwabadilisha tu! Tunapenda kujua, kama Bunge, wamechukuliwa hatua gani za ziada ili iwe ni funzo kwa wafanyakazi wengine ambao wanafanya vitendo kama hivi? Kazi isiwe ni kuwabadilisha tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine wamesema kwamba, wataongeza miundombinu. Hili nalipongeza kwa sababu kila siku nchi yetu inakua, na kwa hiyo, miundombinu inahitaji kuongezwa; hilo nalipongeza.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Mfuko wa Mikopo ya Watumishi wa Umma. Huu mfuko nikiuangalia, sijui hata lengo lake kwa sababu umekuja kuweka hasara hapa ya shilingi 7,280,000,000. Kwa nini? Fedha zimekwenda, lakini hazina marejesho. Fedha ambazo ni shilingi 5,702,000,000 zilishaanza kurudishwa, lakini huku kwenye mfuko hazijafika, hazionekani. *CAG* ameonesha hivyo. Fedha ambazo zilikuwa hazitakiwi kurudishwa, bado muda wake, ni shilingi bilioni mbili tu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili hivi mantiki yake ni nini? Kama nia ni kuwasaidia wafanyakazi wa mashirika ya umma, benki zetu zipo hapa. Sisi Wabunge pia tunakopa. Mbona tunakwenda kule. Kwa nini hatuna mfuko huu? Ni kwa sababu ya nia njema. Benki zina uwezo mzuri wa kuratibu.

Mheshimiwa Spika, tunajiongezea kazi kama Serikali kuzipeleka fedha kule na zinapotea. Benki zinao uwezo wa kuratibu. Mimi ninashauri mfuko huu ufutwe ili wanaotaka kukopa kwenye mashirika ya umma waende kule benki na wao wakaone kwamba fedha hizi zina ufuatiliaji mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Bodi ya Utalii. Bodi ya Utalii imekuwa ikikusanya fedha kwa kutumia mfumo wa kawaida wa *manual* bila kutumia mfumo sahihi wa Serikali. Sasa sijui nani atakwenda kujithibitishia? Ikiwa Wakurugenzi wa Halmashauri wao wamewaajiri wale wafanyakazi kwenye masoko na wanatumia mifumo, Bodi ya Utalii kweli inashindwa kufanya jambo hili?

Mheshimiwa Spika, walipoulizwa na Kamati yetu walisema kwamba sasa watawasiliana na watu wa TEHAMA ili kutengeneza mifumo. Yaani mpaka leo! Tujiulize, hii mifumo yetu ya TEHAMA imeanza lini na mpaka leo hawajajiunga? Hili ni jambo la makusudi. Mwenyekiti wetu wa Kamati hii ambaye ameshughulikia hili aje na maazimio makali kuhusiana na suala hili ili lisijirudie tena, na mwakani watatueleza hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada yah apo, niende kwenye suala la *NHIF*. Nimeona hapa kwenye Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyopo Dodoma, kuna hasara ya shilingi 3,266,000,000 kwa kukataliwa maombi yao ya huduma ambazo wamezitoa kule. Jambo hili linaakisi nini? Hospitali zetu zile za binafsi ambazo zinatoa huduma, hii imetolewa hospitali ya Serikali tu, sasa kama ya Serikali imekataliwa, je, zile za binafsi ni ngapi zimekataliwa?

Mheshimiwa Spika, naamini kwa changamoto hii, ziko zaidi ya mabilioni na matrilioni ambayo hospitali zimekataliwa. Kwa hiyo, inaonesha *NHIF* hawana mfumo sahihi wa kutoa huduma hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri *NHIF* wasituletee *disaster,* mpaka hospitali zetu nyingine zinakataa kutoa huduma. Tulisikia hapa hospitali zilikataa kutoa huduma na Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wengine wamelalamikia sana suala hili. Sasa ni kwa nini *NHIF* wanafanya hivi? Sijui wameshindwa wapi?

Mheshimiwa Spika, nafikiri nimalizie kwa kusemea mashirika na bodi zetu zinazofanya vibaya. Sisi kama Bunge tunadharaulika sana kwa sababu tumeishia kusema tu. Tunapofika mitaani huko tunaambiwa, sasa nyie kazi yenu ni kusema tu, hamfanyi lolote.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Bunge ni kushauri, kusimamia na kuwajibisha. Sasa hii ya mwisho, hii ya kuiwajibisha Serikali, tumeisahau kabisa. Naamini kwamba hatujawatendea haki wananchi, au tuifute kama tunataka kufanya kazi nzuri, kwa sababu hawa Wenyeviti wa Bodi wanakuja na Mawaziri hapa kwenye Kamati zetu, tunawahoji na ripoti zao zinakuwa zimesainiwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna Mheshimiwa Waziri anashindwa kusimamia taasisi iliyo chini yake, basi na wao tuwawajibishe. Hakuna haja ya kusema sijui nani, sijui Mwenyekiti wa Bodi aliyechini yake; mtoto akiwa na tabia nzuri, basi anasifiwa mzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri wetu, mumsaidie Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais hawezi kufika huku. Mumsaidie ili nchi yetu iwe salama na amani, na wananchi wasiwe na changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, hayupo. Sasa namwita Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mheshimiwa Prof. Alexander Kitila Mkumbo, ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kipekee kabisa naomba nitumie nafasi hii binafsi kukupongeza kwa ile hotuba nzuri kule Geneva ambayo iliwakosha Watanzania wengi kwa namna ambavyo ulikuwa umewajibu wale wenzetu na hususan mimi binafsi nilikoshwa na yale majibu uliyompa yule Mheshimiwa Mbunge wa Ukraine. Hongera sana na ulipamba vichwa vingi vya Habari hapa nchini kwetu, tulifurahishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza niunge mkono hoja zote za Kamati ambazo zipo Mezani; Kamati ya *LAAC*, Kamati ya *PIC* nimeshawahi kuhudumu huko na sasa hivi mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika yake. Niungane na wenzangu wote kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti pamoja na Wajumbe wenzangu kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kutoka kwenye Taarifa ya Kamati yetu na kwenye Taarifa ya *CAG* nitaongea kwenye upande mmoja tu wa wakusanya kodi *TRA*. Nchi yoyote haiwezi kujiendesha pasipo kuwa na makusanyo mazuri ya kodi. Kabla sijaendelea kwenye mchango wangu, naomba niwa-*quote* wanafalsafa wachache huko duniani kwa maneno machache ambayo waliongea kuhusiana na kodi.

Mheshimiwa Spika, Mwanafalsafa wa kwanza anasema *"Governance have only one source of income taxes"*, mwingine anasema *"Having a lower tax simpler, fairer and flatter tax system is something that can drive gross",* lakini wa mwisho anasema *"Paying tax is not punishment, it is a responsibility,"* yaani kulipa kodi siyo adhabu, ni wajibu.

Mheshimiwa Spika, kauli hii inakuwa na maana kama tu wajibu huu utakuwa umeenda sawa. Wajibu huu usiwe kuna watu unawaumiza na kuna watu unawapendelea. Huu wajibu unapotea, hata wale ambao walikuwa wana moyo wa kutaka kulipa kodi unapungua. Ndipo hapa huyu mwingine anasema, "*Having a lower tax, simpler, fairer tax system is something that can drive gross.*"

Mheshimiwa Spika, kwenye Taarifa ya Kamati yetu na ile ambayo ilitoka kwa *CAG*, watu wa Mamlaka ya Mapato *(Tanzania Revenue Authority)* mwaka wa fedha 2022/2023 walikuwa wamekadiriwa kukusanya kodi ya shilingi 23,652,000,000,000 lakini wakakusanya shilingi 22,583,000,000. Hawakuweza kufikia lengo, wakawa wana pungufu ya shilingi 1,069,000,000,000, hivyo kupungua kwa 4.5%, walijitahidi walisogea sogea.

Mheshimiwa Spika, kutoka kwenye Kamati yetu, upo upungufu ambao tuliuona ambao *CAG* alipotuletea taarifa kwamba mambo hayo yalisababisha kushindwa kufikia hilo lengo, pamoja na changamoto nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge hili tulilonalo ni Bunge la kuishauri Serikali kwenye vyanzo vipya vya mapato, vipo baadhi ya vyanzo ambavyo nimeshakuja kuvishauri hapa, na Serikali tunaona bado hawajavitekeleza. *TRA* kwa kujituma huko huko kukusanya kodi kwa wananchi, zipo nyakati tofauti ambapo wananchi wa kawaida, wafanyabiashara wa kawaida na wenye mitaji ya kawaida wamekuwa wakilalamika kwamba wanawekewa lundo la kodi nyingi. Pia kodi hizo zinakuwa ni za kiwango cha juu sana, wakati mwingine kulinganisha na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri, nitolee mfano kwa wafanyabiashara wa kule kwetu Tunduma mpakani kwetu. Wafanyabiashara wengi ambao wapo Tunduma wamehamia nchi ya Zambia. Ukiwauliza sababu ya kukimbia kwenda nchi ya Zambia kufanya biashara na wakati huo tunaoenda kununua bidhaa zao ni sisi wenyewe Watanzania, lakini kodi wanalipa upande wa Zambia, wanasema kwamba wakija *OSHA* kukukagua atakuja na Polisi, wakija watu wa leseni ya biashara watakuja na Polisi, wakija watu wa *TRA* wanakuja na Polisi, lakini utakuta mfanyabiashara huyu anafanya labda biashara yenye thamani ya shilingi milioni nne, analipa tu kodi kwa mwaka, kila kitu *OSHA*, usafi, leseni za biashara shilingi 120,000, lakini ukija kwetu lundo na lukuki ya kodi.

Mheshimiwa Spika, vipo vyanzo vizuri ambavyo *TRA* ingeamua kuvisimamia wangeweza kukusanya kodi kikamilifu bila hata kuwabugudhi wafanyabiashara wadogo. Miongoni mwa dosari ambazo *CAG* anasema, kulikuwa na dosari katika mfumo wa ving'amuzi vya kieletroniki wakati wa kuthibitisha bidhaa zinazotoka nchini na kwenda nchi jirani. Akafafanua sehemu hizo, na katika hoja hii *CAG* alibaini miamala 238 ikijumuisha miamala 95 katika mpaka wa Mtukula; miamala 22 katika Mpaka wa Rusumo na miamala 121 katika mpaka wa Tunduma.

Mheshimiwa Spika, maana yake wapo baadhi ya watu ambao wao wakiingiza mizigo hapa nchini kwetu wakifika tu pale Nakonde, Isaka ambayo ni kama kilomita 30, 40 kwenda upande wa Zambia wanarudisha bidhaa wanakuja kuuza nchini kwetu, wanakwepa kodi. Ukweli watu ambao wanafanya biashara za Kimataifa ni watu ambao wana mitaji mikubwa. Kwa hiyo, unaweza ukaona, *TRA* kwa nini hawaweki nguvu kwenye eneo hili, na ndipo mahali ambapo kuna pesa nyingi?

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa mfano ukiangalia katika miamala shuku 238, Mpaka wa Tunduma tu ndiyo una zaidi ya 50%; na 121 kwa ving'amuzi ambayo haikufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimeshawahi kutoa wazo hapa Bungeni kwamba Mpaka wa Tunduma unabeba nchi nyingi; Zambia, *DRC*, Malawi, Zimbabwe na nchi nyingine. Tuongezewe mpaka mwingine ili kupunguza urasimu ambao upo kwenye geti la Tunduma. Sisi tunaamini kwamba magari machache yakipita pale yakisimamiwa kikamilifu hata hawa watu ambao wanafikiria wangeweza ku-*temper* na kufanya hayo mambo, tunaamini labda wangeweza kuonwa kwa sababu kungekuwa kuna *transparent*.

Mheshimiwa Spika, kama *TRA* wakipeleka nguvu huku mipakani hawatasumbuana na wafanyabiashara wadogo wadogo wenye mitaji ya shilingi milioni moja au mbili. Iweje nguvu nyingi wanapeleka kwa wafanyabiashara wadogo? Hawa wafanyabiashara wakubwa ambao wanarudisha bidhaa nchini bila kulipa kodi mbona wameachwa?

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, *CAG* alibaini uwepo wa bakaa wa lita za mafuta 1,105,466. Kama tunavyojua, nchi nyingi ambazo zimeendelea ni zile ambazo zinafanya biashara ya mafuta. Vivyo hivyo hata wafanyabiashara wengi waliopo hapa Tanzania ambao wanafanya biashara za mafuta ni wale ambao wana mitaji mikubwa. Maana kama kuna mafuta ambayo ilibidi yatoke nje ya nchi yetu yalipiwe kodi, lakini yakaondoka yakaendelea kubaki hapa nchi kwetu, ni nani aliyesababisha

mafuta haya yaendelee kubaki hapa nchini? Kwa nini watu hawa hawakulipa kodi?

Mheshimiwa Spika, hizi ni zile tu ambazo *GAG* amezitambua kwa sababu *CAG* naye pia ni binadamu. Inawezekana zipo lita zaidi ya hizi. Inawezekana zipo hata lita milioni saba hajaweza kufanikiwa kuzitambua kwa sababu anafanya kazi na watu. Inawezekana kuna mahali pia walimzidi ujanja.

Mheshimiwa Spika, wito wangu ni kuwaomba watu wa *TRA* waelekeze nguvu zaidi kwenye vyanzo vikubwa hivyo ambavyo ndiyo vitafanya waweze kukusanya mapato kikamilifu na kuweza kufikia malengo ambayo walikuwa wamewekewa. Pia, wanapokusanya kodi kwa wafanyabiashara wakubwa na vile vyanzo vikubwa ambavyo tunavijua ni vya kimkakati vinafanya wafanyabiashara wadogo wadogo wasiumie.

Mheshimiwa Spika, pia, wanapopita malengo katika kukusanya kodi ambazo wamewekewa, wanaifanya nchi yetu tuweze kukamilisha miradi mingi sana ambayo tumejiwekea kimaendeleo. *As we are speaking now,* yapo baadhi ya maeneo vijijini hakuna zahanati na vituo vya afya. Kwa hiyo, kama wangeweza kufikia lengo, kwa mfano hili la shilingi trilioni moja lingeweza kujenga zahanati nyingi. Zingeweza kujenga vituo vya afya na zingeweza kusaidia kupeleka madawa hospitali mahali ambapo bima haziwezi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuendelee kuwaomba watu wa *TRA* wapeleke nguvu mahali ambapo kodi kubwa zikikusanywa zitasaidia kuliko kukimbizana na wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, katika ripoti nyingi ambazo tulizipitia kwenye taasisi mbalimbali kwa ujumla kama ambavyo na watu wa *LAAC* pia wameongea, yapo mashirika mengi na taasisi nyingi za umma ambazo zinadaiana wao kwa wao. Kwa hiyo, kusababisha taasisi mojawapo ya kiserikali kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu wanaidai taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama tunasema Serikali inasomana, ni pamoja na kila mtu kumlipa mwenzake ili mwenzake aweze kutekeleza vizuri ile bajeti ambayo tulimpitishia hapa Bungeni. Kama taasisi nyingine inaidai Taasisi ya Serikali, eti kwa sababu ni Serikali kwa Serikali wanadaiana, taasisi nyingine haiwezi kutekeleza majukumu yake. Mbona wananchi wa kawaida wakiwa wanadaiwa wanachukuliwa hatua? Kwa nini taasisi nyingine yenyewe ihodhi fedha za wenzao na taasisi nyingine ishindwe kutekeleza majukumu?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia hoja iliyopo Mezani ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa hesabu za *GAG* zilizoishia Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyingi na za dhati kwa Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge kwa kazi nzuri anayoifanya yeye pamoja na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hakika wamefanya kazi hii kwa umakini wa hali ya juu sana mpaka usiku wa manane katika jukumu lao la kuchambua taarifa za halmashauri zetu na kuishauri Serikali na kuisimamia ili tuweze kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa hoja nyingi sana na muhimu ambazo wamezitoa wakati wa kuchangia Taarifa hii ya *LAAC*. Niwahakikishie tu kwamba kazi yetu sisi kama Serikali ni kuchukua hoja hizi, kuzifanyia kazi kwa manufaa ya wananchi wenzetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukitazama kwa kina, pamoja na kwamba bado kuna upungufu mwingi katika halmashauri zetu katika usimamizi wa fedha za Serikali, lakini ukiangalia mtiririko na *trend* nzima ya namna ambavyo upungufu huu umeendelea kubainishwa kwenye Taarifa ya *CAG* utaona kuna *improvement* kubwa sana kwa maana ya kupungua kwa hoja za matumizi mabaya ya fedha ya Serikali, na pia kwa maana ya kuongezeka kwa Hati Safi katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii, na kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ameendelea kusimamia Serikali hii, na pia kutuelekeza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa yetu kuendelea kuboresha upungufu ambao unabainishwa na *CAG*.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuchangia katika hoja chache ambazo zimeainishwa na Kamati yetu, lakini pia zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Nikianza na hoja ya ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali imeweka kipaumbele kuhakikisha kwamba halmashauri zetu zinaendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Hii inaziwezesha halmashari kupunguza utegemezi wao kwa fedha ya Serikali Kuu, lakini pia kuwezesha halmashauri kutatua changamoto mbalimbali za wananchi kwa kuongeza uwezo wa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, zipo halmashauri ambazo hazikupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwenye halmashauri. Sisi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kusimamia halmashauri zote kuhakikisha zile ambazo zinatakiwa kupeleka fedha 20% kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinapeleka na 40%, 60%, 70% zote zinapeleka kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha Halmashauri zote ambazo hazijapeleka fedha hizi kwenye miradi ya maendeleo, tunaendelea kuchukua hatua stahiki za kinidhamu ili kuhakikisha

kwamba fedha hizi zinafika kwenye miradi hiyo na kutekeleza miradi iliyokusudiwa kadri ya maelekezo na mwongozo wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba halmashauri zetu zote zinapeleka fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyopangwa na miongozo ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya 10%, ni kweli kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja tulisimamisha huduma za mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ni kupitia sheria yenyewe, kuifanyia maboresho lakini pia kupitia kanuni mbalimbali zinazosimamia mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tumeshakamilisha hatua zote kwa maana ya sheria, kanuni na taratibu zinazoendelea ni kufanya mafunzo kwa Kamati zote za mikopo ya 10% ngazi ya mikoa, ngazi ya halmashauri, ngazi ya kata na ngazi za vijiji. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaondokana na changamoto ya fedha ambazo zimekuwa hazirejeshwi ambazo zinakopeshwa kwa vikundi vya wajasiriamali katika miaka iliyopita na kwenda kuhakikisha kwamba ufanisi wa marejesho ya fedha unaendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la 10% katika Hesabu za CAG zilizoishia Juni, 2023, jumla ya shilingi bilioni 79 zilikuwa hazijarejeshwa. Naomba nitumie nafasi hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba mpaka kufikia tarehe 30 Oktoba mwaka huu 2024 jumla ya shilingi bilioni 27 tayari zimesharejeshwa na jitihada za kuendelea kurejesha fedha ambazo zinabakia zinaendelea. Kwa hiyo, tutahakikisha fedha zote ambazo hazijarejeshwa zinarejeshwa na Serikali tumeshaainisha vikundi vyote vinavyodaiwa na tumeshaviweka kwenye *database* ya kufuatilia kila kikundi kuhakikisha kwamba fedha hizo zinarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wanahusika katika kutoa mikopo kwa vikundi hewa, sheria zitachukuliwa dhidi yao

na tutahakikisha tunakomesha utaratibu wa kuwa na vikundi hewa katika maeneo ya mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ulipaji wa madeni, ni kweli kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinadaiwa madeni mbalimbali. Yapo madeni ya watumishi, lakini pia yapo madeni ya wazabuni. Naomba nitumie nafasi hii niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kwanza, katika kipindi hiki cha miaka mitatu cha Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, madeni mengi sana ya watumishi yamelipwa.

Mheshimiwa Spika, watumishi wetu wa kada mbalimbali katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wamelipwa madeni yao kwa kiasi kikubwa sana. Pia, bado kuna madeni ambayo yanaendelea kufanyiwa tathmini, kuhakikiwa kwa ajili ya kuendelea kulipa kwa watumishi wetu. Kwa hiyo, suala hili ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wetu wanalipwa madeni yao kwa kadri wanavyostahili. Vile vile ni muhimu kwa Serikali kujiridhisha kwa kufanya tathmini na uhakiki ili madeni yawe ni halisia na Serikali iweze kuwalipa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo madeni ya wazabuni yameendelea kulipwa, na tunahakikisha tunaweka mpango mkakati wa kulipa madeni yote ya nyuma. Pia, tumeweka mpango wa kuzuia madeni mapya katika halmashauri zetu, na katika kila bajeti tumeelekeza halmashauri zetu kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea maoni yao, ushauri wao na mapendekezo ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kulipa madeni ya wazabuni.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba wazabuni wetu ni Watanzania wenzetu, wanakopa katika benki mbalimbali, wanahudumia halmashauri zetu, hivyo, ni haki yao kulipwa kwa wakati na ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha kwamba tunawalipa kwa wakati. Suala hili tutaendelea kulifanyia kazi na

tutaendelea kuhakikisha kwamba tunazuia uzalishaji wa madeni mengine katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusiana na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani katika halmashauri zetu. Tumeweka mpango na tumeweka *Key Performance Indicators* kwa halmashauri zetu kuhakikisha kwamba kila mwaka wa fedha wanabuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani, wanavisimamia na wanakusanya kwa ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya *CAG* iliyowasilishwa na Kamati yetu, tumeona kuna halmashauri ambazo hazizidi 10 ambazo hazikukusanya zaidi ya 10% ya mapato yake ya ndani. Hali hii inaonyesha ongezeko la ufanisi ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita na miaka miwili, mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Spika, miaka iliyopita halmashauri zaidi ya 30% zilikuwa hazijafikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 tunaona tumepunguza sana idadi ya halmashauri ambazo hazikufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuendelea kuzijengea uwezo halmashauri, kuwezesha makusanyo ya mapato ya ndani ili kuweza kutumia fedha hizo kwa ajili ya kuboresha miradi ya maendeleo, kuhudumia wananchi, kutatua kero mbalimbali na kupunguza utegemezi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wake kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumepokea maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, pamoja na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge. Kazi yetu ni kwenda kuyatekeleza, na katika eneo hili tutahakikisha tunatekeleza maeneo hayo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia niongezee kwenye eneo la 10%. Kulikuwa na wazo kwamba tuanze na halmashauri 10 peke yake. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, katika

utaratibu mpya, tumeweka halmashauri 10 zitakwenda kwa utaratibu wa *pilot* kwa maana ya kwenda na mabenki; halmashauri 174 zitakwenda na utaratibu wa 10% ulioboreshwa.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie kwamba tutakwenda kusimamia vizuri kwa sababu mfumo umewekwa vizuri, na tumeanzisha mfumo wa kielektroniki wa *Ten Percent Loan Management Formation System* ambao unatambua mapungufu mapema kabla hali haijawa mbaya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii nami kukushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pia tunakushukuru na kukupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya hapa Bungeni, pia katika kutuwakilisha kwenye Umoja wa Mabunge. Tumethibitisha kule kwamba moja ya sifa yako ni kupenda usawa wa Wabunge wote hapa ndani, lakini pia umethibitisha kwamba unapenda usawa wa Wajumbe wote wa *IPU* bila kujali anatoka wapi. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tunawapongeza sana wenzetu wa Kamati zetu mbili, nami nakiri kwamba nimeshiriki kwenye moja ya Kamati, siyo kama Waziri, lakini kama Mwenyekiti wa Bodi ya moja ya shirika ambalo lilishughulikiwa kule. Nithibitishe kwamba Kamati zako ni makini sana. Jinsi wanavyohoji, nami nilifika pale wakasahau kabisa kama ni Mbunge mwenzao, waliniweka kitimoto cha kutosha. Zinafanya kazi nzuri sana hizi Kamati zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kupongeza taasisi na mashirika yetu ya umma kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kama ambavyo Kamati imebainisha. Ukweli ni kwamba taswira ya Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kiasi kikubwa sana inajengwa na taswira ya kazi ambazo taasisi na

mashirika ya umma yanafanya. Kwa hiyo, tusisahau hilo kwamba wanafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nieleeze tu kwamba, kama ambavyo Kamati imebainisha, Serikali inafanya mageuzi makubwa katika uendeshaji wa mashirika ya umma, na mageuzi hayo yako katika maeneo mbalimbali, lakini moja ni kuwezesha mashirika ya umma ambayo yanatakiwa kufanya biashara yapate mitaji stahiki, na pia kuboresha menejimenti zao kama ambavyo Kamati imeeleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uchambuzi wa haya mashirika yote ya umma na tunabainisha kwamba yapo mashirika ya umma ambayo majukumu yao yameshapitwa na wakati, ama kwa sababu majukumu hayo kwa sasa hayafanywi na Serikali, ama majukumu hayo kwa sasa yanaweza yakafanywa vizuri zaidi na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, yapo mashirika ya umma ambayo majukumu yao yanafanana sana na kuingiliana miongoni mwao. Kwa kuzingatia hilo, Serikali inachukua hatua ama mashirika haya kuyaunganisha yale ambayo majukumu yao yanafanana na kuingiliana, na tayari taasisi kadhaa Serikali imechukua hatua ya kuziunganisha na tumeshaandaa Miswada ya Sheria, muda ukifika tutawasilisha hapa kwa ajili hiyo ili Bunge lako lijadili na likiona inafaa, liweze kuchukua hatua stahiki za kutunga sheria ambazo zinahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, yapo mashirika ya umma ambayo Serikali imeshapendekeza kwa mujibu wa sheria zao yafutwe. Kwa hiyo, na yenyewe Waheshimiwa Mawaziri wa sekta husika watawasilisha hapa mashirika ya umma ambayo tunadhani kwamba yamepitwa na wakati kwa maana ya majukumu yao waweze kuchukua hatua ya kufutwa.

Mheshimiwa Spika, ni mchakato mgumu, kama ambavyo Kamati imebainisha na imeona, hakuna mtu ambaye angependa kufutwa wala hakuna mtu ambaye angependa kuunganishwa, lakini Mheshimiwa Rais ameshachukua hatua hizo na sisi kama

Serikali tunaenda kutekeleza, na muda ukifika tutawasilisha Miswada hapa Bungeni kwa ajili ya hatua hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, niseme kwamba siyo kila shirika la umma linapaswa kuleta faida, na siyo kila shirika la umma linapaswa kufanya biashara kwa sababu wakati mwingine mijadala yetu hapa ni kana kwamba mashirika yote haya 309 ni mashirika ambayo yanapaswa kuleta faida ya fedha, Hapana! Mashirika haya yanapimwa kwa tija tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, yapo mashirika ya umma ambayo kwa asili yao yanapswa kufanya biashara na kwa kweli yanatengeneza faida, lakini yapo mashirika ya umma ambayo yanapaswa kufanya biashara, lakini hayajaanza kutengeneza faida kwa sababu yako katika hatua mbalimbali za kujiendeleza na kujijenga. Kwa mfano, likiwemo shirika letu la ndege *ATCL*. Kwa hiyo, katika mchakato ambao tunafanya haya, kwa sasa haishangazi kwamba halijaanza kutengeneza faida kubwa kwa sababu ni mchakato.

Mheshimiwa Spika, yapo mashirika ya umma ambayo yanatengeneza hasara kwa sababu ama ya ufanisi wao ni mdogo, ama kwa sababu kazi ambazo yanafanya, yanapaswa kufanya vizuri zaidi na sekta binafsi. Mashirika haya, Serikali haitasita kuyafuta, kwa sababu kama limetengenezwa kwa ajili ya kufanya biashara na halifanyi biashara linatengeneza hasara, maana yake hiyo kazi inaweza kufanywa vizuri zaidi na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, *category* ya nne, yapo mashirika ambayo yanatoa huduma, na kutokana na huduma zao yanaenda kujiendesha, kwa hiyo, hayatengenezi faida, hayatengenezi hasara, lakini kwa huduma yao wanapata tozo ambayo inayawezesha kujiendesha. Hayo ni mashirika ambayo hatutarajii yadaiwe gawio. Haya yanaweza yakatoa mchango 15%, lakini siyo gawio kwa maana ya kutoka kwenye faida yao. Hilo na lenyewe lazima tulielewe.

Mheshimiwa Spika, yapo mashirika ambayo yanatoa huduma na katika huduma zao hayawezi kuzalisha chochote, na

kwa hiyo lazima dola ibebe gharama zake. Kwa hiyo, tukiona katika taarifa zetu mashirika ya namna hii, tusiseme kwamba yanatengeneza hasara, hapana. Ni kwa sababu kwa asili yao faida yao ambayo wanazalisha siyo fedha, faida yao ni huduma wanazozitoa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukiangalia, taasisi ambazo zinafanya utafiti, taasisi ambazo zinatoa *training* kwa maana ya elimu, hizi hutarajii tuone kwamba zinatoa faida, au baadhi ya taasisi ambazo ni za kutoa huduma za afya. Kwa hiyo, na lenyewe lazima tuwe nalo.

Mheshimiwa Spika, *category* ya mwisho ya sita ni mashirika mbayo yanafanya urekebu, kwa maana ya hizi *Regulatory Boards*. Hizi ni taasisi ambazo kwa asili yake zinatengeneza mazingira ya biashara. Kwa hiyo, hazitengenezi faida yoyote isipokuwa wahakikishe kwamba wanaweka mazingira mazuri kwa ajili ya biashara kufanyika na uwekezaji kufanyika. Kwa hiyo, na yenyewe haya hatutarajii yatoe gawio. Yanaweza yakatoa mchango lakini hatutarajii kuona faida kwa maana ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu Waheshimiwa Wabunge tukaelewa mgawanyiko wa mashirika haya ili tutakapoyadai faida tuyadai katika maeneo ambayo yanahusika.

Mheshimiwa Spika, pia, tunashukuru kwamba Kamati imetambua baadhi ya mafanikio ambayo mashirika ya umma imefanya, ikiwemo ile michango ambayo inatoa, na mapato siyo ya kikodi yameweza kuongezeka kwa 19%. Kwa hiyo, hili tunashukuru, lakini tunapokea ushauri wa Kamati hususan kwa mashirika ambayo yalipaswa kutoa gawio, lakini yameshindwa kutoa gawio, Kamati imeelekeza vizuri kwamba tuweze kufanya uchambuzi na tuone mashirika haya. Yapo mashirika takribani 33 ambayo yametoa gawio vizuri ambayo ni mashirika tisa peke yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho tunaahidi hapa sisi kama Serikali kwamba tutafanyia kazi maelekezo na ushauri wa Kamati kwamba mashirika 63 ambayo yanatengeneza mapato

makubwa kuliko ruzuku wanayopokea, lakini bado wanapokea ruzuku. Nadhani, hii ni hoja ya msingi sana kwamba mashirika haya yanatengeneza mapato makubwa kuliko hata ruzuku ambayo wanapokea. Sasa wanapokea ruzuku ya nini? Nadhani sisi tunapokea ushauri huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelekeza tukafanye uchambuzi. Tutafanya uchambuzi na tutaona namna ya kwenda nayo mbele. Pia wametoa ushauri mzuri kwamba mashirika haya yanayofanya biashara yapatiwe uhuru wa kiuendeshaji ikiwemo uhuru wa kuajiri. Tayari Msajili wa Hazina anafanya mawasiliano ya karibu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kwa kweli mashirika ambayo tumesema yafanye biashara, lazima yajiendeshe kwa mtindo wa kibiashara duniani kwa maana ya *corporate identity*. Sasa tukitaka yajiendeshe kama idara ya Serikali ya kawaida, inaweza ikawa changamoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mawasiliano yanafanyika kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na Ofisi yetu ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuona namna gani uhuru huu unapatikana ili tuweze kupokea tu kwao. Tuwape malengo na *target,* nao waje watupe malengo yale ambayo tumewawekea, lakini tuwape nafasi ya kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, tumeyapitia maazimio 14 ya Kamati yetu ya *PIC* na sisi kama Serikali kwa kweli maazimio haya hatuna changamoto nayo, tunaaihidi kuyapokea na kuyafanyia kazi, na tuseme kwamba tutakuwa sehemu ya maazimio hayo kwa sababu ni maazimio mazuri na tukiyafanyia kazi, tutaendesha vizuri mashirika ya umma hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia. Kwanza napongeza Kamati zetu zote ambazo zimewasilisha taarifa na kama

alivyotangulia kusema kaka yangu Mheshimiwa Prof. Kitila kwa niaba ya Wizara na kwa niaba ya Serikali, tunapokea mapendekezo hayo na hatuna shida nayo. Kimsingi mapendekezo hayo yapo ambayo ni *work on progress* ambayo tayari Serikali imeanza kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ninaanza na jambo la kwanza ambalo limetolewa pendekezo kuhusu uboreshaji wa utendaji kazi wa taasisi yetu ya ukaguzi wa ndani. Pendekezo hili ni jambo jema, kazi imeshaanza na tutaendelea kuboresha kama ambavyo mapendekezo ya Bunge lako Tukufu yalivyokuja.

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo tumeyafanyia kazi ni eneo la muundo, tulikuwa na muundo wa Ofisi yetu ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani ambayo katika maeneo mengi ilikuwa ina-*compromise* utendaji wa kazi. Sasa jambo la muundo limeshafanyiwa kazi, kwa sasa Ofisi yetu ya Mkaguzi wa Ndani ina *vote* yake, na hii inarahisisha mpangilio wa utekelezaji wa majukumu yake. Ndiyo maana kwa sasa tunaona baadhi ya miradi na ukiunganisha na nyongeza ya bajeti inaweza kufanya ukaguzi wa miradi ikiwa inaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilinunua tarakilishi mpakato *(laptop)* ambazo zimepelekwa kwa watumishi ikiwa ni sehemu ya kujengea uwezo sambamba na mafunzo ya kuanza kukagua mifumo kwa sababu kwa kiwango kikubwa kaguzi nyingi zilizokuwa zikifanyika zilikuwa zinahusisha masuala ya kiuhasibu.

Mheshimiwa Spika, katika jambo lingine ambalo limejadiliwa lilikuwa linahusisha utekelezaji wa kazi wa majukumu wa *TRAB* na *TRAT*. Tayari tulikamilisha mapengo yaliyokuwepo katika masuala ya uteuzi yakihusisha kutengeneza bodi pamoja na timu za wataalamu katika mikoa ili kuweza kukamilisha *column* ili waweze kufanya kazi ipasavyo, na siyo hivyo tu, pia tulirekebisha kanuni kuruhusu wataalamu wale kuweza kutumika katika maeneo tofauti.

Mheshimiwa Spika, ni kwa vile kazi zilikuwa kubwa sana ambazo zilishakuwa na *backlog* kubwa na zinahitaji kufanyika

kwa ufanisi bila kuonea watu na bila kupoteza mapato ya Serikali. Kwa hiyo, hayo ndiyo yamekuwa yakifanyika na kazi inaendelea vizuri. Mwezi mmoja uliopita tulikaa na timu hizo zote kuweza kupokea hizo taarifa, na tulikaa pamoja na Mamlaka ya Mapato na tukaona kazi inayoendelea na tunaamini siku siyo nyingi tutatoa taarifa ya kazi zikiwa zimeshakamilika zile ambazo zilikuwa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TRA,* kuna maboresho mengi yamefanyika. Utakumbuka katika miaka miwili au mitatu iliyopita, *TRA* inajenga mfumo wa forodha na inajenga mfumo wa kodi za ndani. Mifumo yote hii iko katika hatua nzuri ambapo kwa taarifa tulizozipata mfumo wa forodha ambao unahusisha ujenzi wa *TANCIS* uko katika hatua za mwisho unatarajiwa *by* Januari, 2025 uanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu utakapoanza kufanya kazi utakuwa umeunganishwa pamoja na mifumo mingine ikiwemo mpaka *weight bridge* zetu na hivyo itatusaidia hata magari ambayo yanabeba mizigo ambayo yamepita katika barabara zetu kuweza kuonesha kwamba hayajashusha mzigo wowote njiani kwa sababu uzito ulioonekana mwanzoni na unaoendelea utakuwa huo huo. Kwa hiyo, hili litaenda kutibu hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge, wengi wameongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kodi za ndani utaenda kuondoa malalamiko makubwa ambayo yalikuwa yamejitokeza hasa ya ukadiriaji kwa sababu tukishajenga mfumo, tutapunguza hii ya kukadiriana, kwa kushauriana ambayo katika maeneo mengi inakuwa na makosa ya kibinadamu. Hii ni upande wa mifumo ambayo kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala na masuala ya utawala, utakumbuka Mheshimiwa Rais ameunda Tume ambayo tayari inaendelea kufanya kazi yake, hii inaenda kufanya *review* ya utaratibu wetu wa utozaji wa kodi, viwango vya kodi na utaratibu wa utawala wa masuala ya kikodi. Tume hii imejaa watu wenye weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hilo kubwa ambalo litaenda kutengeneza taswira mpya katika masuala haya ya kikodi. Pia, siku siyo nyingi, wiki kama mbili zilizopita aliizindua tume hii, na inatarajiwa mpaka ifikapo mwaka 2025 ndani ya miezi sita itakuwa imekamilisha kazi hii, na tuna uhakika itaenda kutengeneza kitu ambacho kitakuwa mwarobaini wa matatizo mengi ambayo yalikuwa yanaleta malalamiko katika masuala ya kikodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa benki zetu kama michango ilivyotolewa, *TIB* pamoja na *TADB,* benki hizi zote Serikali imekuwa ikiweka mitaji kuweza kuhakikisha kwamba zinakuwa na ufanisi katika ufanyaji kazi wao. Kwa *TADB* wameendelea kupokea mtaji, kwa *TIB* kazi inayoendelea kwa sasa ni uhakiki wa madeni.

Mheshimiwa Spika, tulishakaa na taasisi yenyewe na pia tumekaa na taasisi ambazo zinaidai hii taasisi yetu. Unafanyika uhakiki na tayari Serikali ilishaandaa mpango ambao itautekeleza wa namna ya ku-*clear* madeni yale na kuifanya benki yetu hii iwe na mtaji, pamoja na ukwasi wa kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liliongelewa, lilikuwa linahusisha mtiririko wa fedha. Kazi inaendelea vizuri. Ni mtiririko wa fedha kwenye miradi, lakini pia mtirirko wa fedha kwenye uwezeshaji wa kuwalipa wakandarasi wetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika Bunge lililopita, tulikuwa na madeni makubwa katika maeneo mengi. Tulikuwa na madeni makubwa kwenye *refund*, tulikuwa na madeni makubwa kwa wakandarasi na tulikuwa na madeni makubwa kwa watoa huduma. Kazi hii imeendelea kuyapunguza na kuhakikisha kwamba hatutengenezi madeni mapya. Kwa hiyo, ni kazi ambayo ni endelevu, isingeweza kufanyika ndani ya siku moja au wiki moja, lakini kazi kubwa sana imeshafanyika kwa sababu tulikuwa tunatenga zaidi ya shilingi bilioni 600 kwa ajili ya kulipa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ambayo inaendelea ni ya kuhakikisha kwamba mtiririko wa fedha kwenye miradi, hasa ya wakandarasi wa ndani, fedha zinatoka kwa wakati na kuhakikisha hatulimbikizi.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine kubwa ambayo imefanyika ambayo kwa kiwango kikubwa na yenyewe ilikuwa inasababisha tufinyanefinyane katika maeneo mengine, ilikuwa ni ukamilishwaji wa miradi ya kimkakati ambayo ilishafikia hatua za kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya mradi mkubwa ambao ni fahari ya Watanzania ni Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tumefinyanafinyana, tumejifungafunga mkanda kwa nguvu za Watanzania tumeweza kuukamilisha na sasa ni zaidi ya 99% na tayari *Megawatts* zimeshaingia kwenye utekelezaji. Sasa hatua ambayo Serikali inaweka jitihada, ni kuongeza nguvu katika kukamilisha utaratibu wa *transmission* ili kuweza kuhakikisha umeme ule unakwenda katika maeneo ambayo unahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lilikuwa ni daraja la kihistoria, Daraja la Magufuli pale Kigongo Busisi, na lenyewe liko zaidi ya 99%, nadhani na lenyewe linaelekea kwenye ukamilishwaji. Nilimwona Waziri wa Sekta akikagua, lakini pia nilimwona Mheshimiwa Rais akikagua. Ni mradi ambao na wenyewe ni fahari ya Watanzania. Tumefungafunga mkanda, lakini ni mradi ambao tunaweza tukauonesha, mradi wa kifahari kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ambao na wenyewe tulifungafunga mkanda na pengine sehemu nyingine ukachelewesha mtiririko kidogo ilikuwa ni ukamilishwaji wa *Lot* ya kwanza na *Lot* ya pili ya reli yetu ya kisasa ambayo Jumanne, tarehe 29 Oktoba, 2024, Mawaziri tulikuwa tunakutana na *delegation* ya wenzetu waliotoka Marekani. Hatukutaka kuwaonesha ubaya, tukawaambia reli hii inakaribiana na za Marekani. Wao wenyewe wakasema, hata sisi Marekani hatuna reli kama hii, labda mtaje viwango vya Ulaya. Kwa hiyo, ni reli ambayo ni fahari ya Watanzania na tayari imeshaanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshuka usiku, nikalala Dar es Salaam na asubuhi nimeshafika hapa kwa kutumia reli ya kisasa ya *SGR*. Kwa hiyo, tulikuwa tunabananabanana ndani ya Serikali kuweza kukamailisha, na sasa *Lot* nyingine zinaendelea, ambapo niliongea na Waziri wa Sekta akasema ya Isaka – Mwanza ndani ya miezi kadhaa baada ya kupata fedha za mwisho itaweza kukamilika na hapa katikati ujenzi unaendelea na *Lot* nyingine zitaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli kuna baadhi ya maeneo yanaweza yakawa yameathirika, lakini yaliathirika kwa utaratibu wa kufunga mkanda, tukamilishe yale maeneo ambayo tunaamini yakikamilika yataleta tija kwa Watanzania. Hili ni jambo la kuchagua vipaumbele tu katika kutekeleza miradi ambayo imekaribia kuleta tija iweze kukamilika na tuendelee na ile ambayo itakuwa inahitaji ukamilishwaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lile ambalo linahusisha makusanyo ya Mamlaka ya Mapato, kama nilivyosema, kwa kazi hii ambayo inafanyika ya kujenga mifumo na ile ya kufanya *review* ya utaratibu wa utawala wetu wa kikodi, tunaamini tutaenda kuziba mapengo yale yaliyokuwa yanajitokeza ambayo yameibua hoja kama ambavyo mapendekezo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wa viwango kabisa kabisa na niwaombe Watanzania waendelee kuwaunga mkono Wabunge wetu, waendelee kumuunga mkono Rais wetu na waendelee kuiunga mkono Serikali kwa sababu kazi zinaonekana na mnaona jinsi ambavyo hata hizi hoja zimeendelea kupungua na Serikali inaendelea kuchukua hatua pale ambapo bado hoja zinahitajika kushughulikiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kikao chetu hiki cha leo kwa sehemu ya kwanza, lakini kabla sijasitisha shughuli za Bunge, yapo matangazo mawili hapa.

Tangazo la kwanza ni la wageni ambao wameingia baada ya tangazo letu la awali. Hawa ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanachama 37 ambao ni *Dodoma Legends* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wetu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho tarehe 01 Novemba, 2024 kutakuwa na semina kuhusu Rasimu ya Awali ya Dira ya Taifa 2050 itakayotolewa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Lengo la semina hiyo ni kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge ili muweze kutoa ushauri na maoni kwa ajili ya kuboresha dira hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, semina hii itaanza kesho saa saba mchana, na tutafanya hivyo baada ya kusitisha shughuli za Bunge kesho. Ni muhimu sana Wabunge wote kuhudhuria, ndiyo maana wengine walikuwa na safari za kikazi ambazo Bunge imebidi tuzizuie ili tushiriki sote kwenye zoezi hili la kutazama wenzetu wamefikia wapi, na mawazo gani tungetaka tuongeze ili nasi tuwe sehemu ya kutengeneza dira hii ambayo italipeleka Taifa letu mbele, tunaamini hivyo kwa miaka 25 ijayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka leo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023;**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano lakini upande wa wachangiaji tulikuwa tumemaliza kabla hatujasitisha Bunge. Kwa hiyo, watoa hoja wataanza kuhitimisha hoja, kisha Bunge litafanya maamuzi.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)*. Namwona Mheshimiwa Joseph Kakunda akija kuhitimisha kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)*, kwanza naomba nikushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kusimamia majadiliano haya kwa siku tatu hizi kwa umahiri na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda pia kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali

Kuu na Mashirika ya Umma kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa michango yao kwa hoja hii muhimu inayohusu uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Michango yao imetolewa kwa weledi na uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yetu. Kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati, tumeipokea na kuithamini michango hiyo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 24, ambapo Waheshimiwa Wabunge 22 walichangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wawili walichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo yalichangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, nitatoa msisitizo kwa baadhi ya maeneo kama ambavyo mapendekezo ya Kamati yalivyotolewa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika maeneo makuu sita kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza wamechangia katika usimamizi wa makusanyo na mapato ya Serikali. Wabunge ambao wamechangia katika eneo hilo ni Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Venant Daudi Protas, Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Noah Saputu, Mheshimiwa Mohamed Issa na Mheshimiwa Condester Sichalwe.

Mheshimiwa Spika, kama taarifa ya Kamati ilivyofafanua, makusanyo ya kodi Tanzania Bara kwa mwaka husika yalikuwa shilingi trilioni 22.583 sawa na 95.5% ya bajeti ya shilingi trilioni 23.652. Hivyo, Serikali haikukusanya shilingi trilioni 1.06.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia kuhusu upungufu uliosababisha kutofikiwa malengo ya ukusanyaji wa kodi, ambapo wamesisitiza mashauri ya kodi yafanyiwe kazi kwa wakati ili fedha zinazoshikiliwa kwenye Mahakama za Rufani za Kodi zimalizike. Ushauri huu umesisitizwa pia katika mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhakikisha inafanya doria za mara kwa mara ili kuhakiki ving'amuzi vinavyofungwa kwenye mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi ili kudhibiti udanganyifu. Pendekezo hili pia lipo katika Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazopendekezwa na Kamati zitasaidia katika kuboresha uwiano wa pato la Taifa kwa kodi zinazokusanywa. Uwiano mkubwa wa kodi kwa pato la Taifa huashiria kuwa sehemu kubwa ya pato la Taifa inakusanywa kama kodi. Kinyume chake, uwiano mdogo wa kodi kwa pato la Taifa huashiria kuwa sehemu ndogo ya pato la Taifa imekusanywa kama kodi. Kwa sasa uwiano wetu wa kodi kwa pato la Taifa ni 12%, kiwango ambacho bado ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili ndiyo maana Kamati ilisisitiza sana usimikaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato; kusafisha taarifa kwenye mifumo *(Data Cleaning)* ili kuwa na taarifa sahihi wakati wote; kutambua na kusajili idadi halisi ya walipakodi; kutambua kila aina ya kodi na kiasi kinachotakiwa kulipwa na kinachoweza kukusanywa; vilevile, kuhuisha kanzidata ya walipakodi yenye uhalisia; na mwisho, *TRA* kuandaa hesabu kila mwaka kwa kutumia mfumo wa *Revenue Statement and Financial Statement* ili kuondoa uwezekano mkubwa wa kuwa na makosa ambayo huathiri taswira halisi *(fair view)* ya vitabu vya hesabu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli katika eneo hili nawapongeza sana na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa weledi mkubwa na kwamba walikuwa na ufahamu wa kutosha wakati walivyokuwa wakitoa michango yao.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni eneo la kukataliwa kwa madai yaliyowasilishwa na Hospitali ya Benjamin Mkapa katika Mfuko wa Bima ya Afya. Waliochangia katika eneo hili ni Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii Waheshimiwa Wabunge wameutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuboresha mifumo yake ili kuhakikisha kwamba madai yanayoletwa na watoa huduma yanahakikiwa kwa wakati. Hii itasaidia mfuko kupata malipo stahiki, lakini pia watoa huduma kuwa na uwezo wa kuendelea kutoa huduma bila kikwazo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi bilioni tatu zilizokataliwa na *NHIF* kwa Hospitali moja tu ya Benjamin Mkapa ni kiasi kikubwa. Hivyo, mapendekezo ya Kamati yanatakiwa yafanyiwe kazi ili kuepusha kadhia hii. Pia Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia kwenye eneo hili kama nilivyowataja, wamesisitiza kwamba, kama hospitali moja imekuwa na takwimu hiyo maana yake ni kwamba ukijumlisha matatizo ya aina hii kwenye hospitali nyingi (hospitali za binafsi na za Serikali) basi tatizo litakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, inatakiwa lifanyiwe kazi kama ambavyo Kamati imependekeza katika maazimio.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia ni Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Wabunge ambao wamechangia katika eneo hili ni Mheshimiwa Simon Songe, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Nusrat Hanje.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge katika hoja hii wamebainisha changamoto za msingi kama ifuatavyo: -

(a) Bodi kutokuwa na fedha za kugharamia mikopo kwa wanafunzi 77,401 waliohitaji mikopo ya shilingi bilioni 198.9; kati ya hiyo miaka kuanzia 2015 hadi 2021; na

(b) Upungufu katika mifumo ya kikokotoo cha upimaji wa kiwango cha uhitaji wa mikopo na upungufu katika

urejeshaji wa mikopo iliyotolewa, ambapo hadi sasa takribani kiasi cha shilingi trilioni 2.2 haijarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, michango mingi ya Wabunge imesisitiza umuhimu wa kuwa na mfuko wa mikopo ya ufadhili wa elimu ya juu ili kutatua changamoto za ugharamiaji wa elimu ya juu. Ikumbukwe kwamba, ombwe la ugharamiaji wa elimu ya juu *(financing gap)* kwa miaka 10 ijayo, linaweza kufikia 32% kutoka 70% ya sasa. Pia, ni muhimu mapendekezo haya ya Kamati katika eneo hili yakazingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Waheshimiwa wamechangia kwa uhakika kabisa kwamba, zipo hatua ambazo zinatakiwa kuchukuliwa na Serikali pamoja na wadau wa sekta ya elimu ili kuhakikisha matatizo ya sasa ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu yanatatuliwa, hasa hili pendekezo kuu la kuanzisha mfuko maalum, unaweza ukawa na vyanzo vya mapato na hivi vyanzo vikawa na uhakika kabisa na vikaweza *ku-close* hiyo *financing gap* ili kuhakikisha kwamba, vijana wetu wengi zaidi wananufaika kwa kupata hii mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, nimeshuhudia na Wabunge wengi wameshuhudia kwamba wapo vijana wengi wamekuwa wakikatisha masomo kwa sababu ya kukosa mikopo hii ya elimu ya juu, na uhitaji ni mkubwa na mwingi. Kwa hiyo, tunavyokwenda mbele hivi, ni lazima tuwe na uhakika zaidi kwamba mfuko huu utaendelea kuhudumia vijana wetu kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia ni kuimarisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Wabunge waliochangia katika eneo hili ni Mheshimiwa Venant Daud Protas na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa sasa na jitihada za Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuvutia uwekezaji, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni muhimu sana, hasa katika usuluhishi wa kesi za madai ya kimikataba mara kunapojitokeza migogoro. Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza umuhimu wa kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika masuala ya kimkakati ya usuluhishi ambapo

maoni ya Waheshimiwa Wabunge ni sehemu ya mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika msisitizo, Mawakili wetu wa Tanzania wale waliopo katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambao ndio huwa wanakwenda kusimama katika Mahakama mbalimbali zikiwemo Mahakama za Usuluhishi ndani na nje ya nchi, wanahitaji elimu ya ziada ya kimkakati kuhusu masuala ya mikataba, kuhusu masuala ya sekta mbalimbali kama madini, kuhusu masuala ya kitaalamu kama ufundi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo ambalo limekuwa likizungumzwa na lililetwa kwenye maandishi, yule Mheshimiwa Mbunge alisema, "Ni muhimu kuanza kufikiria kwamba, *Degree* ya Sheria iwe *degree* ya pili." Yaani Mtu akisoma *Engineering*, basi akitaka *Masters,* asome Sheria ili awe na utaalamu wa Uhandisi na wa Sheria. Siyo kwamba kuondoa wanasheria, Hapana. Wanasheria wale wa kawaida wataendelea kuwepo kama wewe Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuwahitaji sana. Hata hivyo, Mbunge aliyependekeza kwamba Serikali ifikirie, ni muhimu sana kufikiria hivyo. Nadhani tutawapa wahusika kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tano ambalo lilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge, ni limbikizo la madai ya maji na madeni ya *TANESCO* kwa *TPDC*. Wabunge waliochangia kwenye eneo hili ni Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya, Mheshimiwa Emmanuel Kasalali Mageni, Mheshimiwa Noah Ole Saputu, Mheshimiwa Abdallah Chikota na Mheshimiwa Flatei Massay.

Mheshimiwa Spika, madeni haya ambayo yamekuwa yakikua na taasisi kwa taasisi zinadaiana. Taasisi ya Maji inaidai *TANESCO*, Taasisi ya Maji na yenyewe inadaiwa na *TANESCO, TPDC* inaidai *TANESCO* na taasisi mbalimbali. Madeni haya yamekuwa yanakwamisha ufanisi wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira na ufanisi wa taasisi hizo zinazodaiana kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama Kamati ilivyopendekeza, Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji, wanatakiwa kuandaa mkakati wa kulipa madeni haya. Kwa *TANESCO* na *TPDC* tunakubaliana na

maelezo ya Serikali kuwa deni limeanza kulipwa na hivyo mpango huo wa malipo uendelee ili kuacha kutengeneza deni kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita ambalo lilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na maazimio ya Bunge kwa ujumla. Wabunge waliochangia kwenye eneo hili ni Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwenye eneo hili wameonesha masikitiko kuhusu kutotekelezwa ama kasi ndogo ya utekelezaji wa mapendekezo ya maazimio ya Bunge. Bunge limekuwa likitoa maazimio kila mwaka kwenye masuala mahususi, lakini hoja hizo zimekuwa zikijirudia tena na isingependeza hoja moja inakuwa inajirudia kila mwaka. Kwa hiyo, hapo ndiyo masikitiko ya Wabunge wengi yalipo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika ngazi ya Kamati katika kipindi cha Agosti hadi Novemba, 2024 zilifika taasisi 31 zilizokuwa na jumla ya mapendekezo 104 ya Kamati na Maazimio ya Bunge. Hata hivyo, kati ya hayo, mapendekezo 60 sawa na 57.7% ndiyo ambayo yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, na mapendekezo 44 sawa na 42.3%, utekelezaji wake ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tungependa kusikia kwamba mapendekezo yote yametekelezwa kikamilifu, lakini kama ambavyo unaweza ukahisi kila wakati huwa kuna changamoto zinazotumika kama sababu za kuchelewa kwa utekelezaji. Kwa hiyo, upande wa Serikali tunawaomba waliangalie sana suala hili.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri waliochangia hoja hii. Mheshimiwa Waziri, Prof. Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waheshimiwa Mawaziri hao wamelieleza Bunge juhudi za uboreshaji zinazoendelea kutekelezwa na Serikali na mikakati

iliyopangwa kutekelezwa ili kuhakikisha kwamba mapendekezo ya Bunge yanatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa ujasiri huo wa kuahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba hatimaye sasa pengine mwaka 2025 tutaona utekelezaji wa 100% wa mapendekezo haya ambayo yamependekezwa. Hilo ni jambo ambalo litakuwa zuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida, tunategemea mwaka 2025 tupate taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na taarifa hizo zitawasilishwa kwenye Kamati na kisha Bungeni kama mrejesho.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye hoja, nirejee kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo hoja hii imejadiliwa kwa kina, weledi na ufanisi mkubwa. Ni imani yangu kuwa mapendekezo ya Kamati yatazingatiwa na kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi nilioutoa hapo juu, na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wameunga mkono mapendekezo ya Kamati, na hapa kuwa na pendekezo jipya, bali kulikuwa na ushauri mwingi kwa Serikali, naomba sasa nitoe hoja kwamba, Bunge sasa lipokee mapendekezo yote ya Taarifa ya Kamati kuhusu Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ili yawe Maazimio rasmi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Mheshimiwa Joseph Kakunda, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ninyi kuunga mkono hoja, sasa nitawahoji ili tufanye maamuzi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) Kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023 yaliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa uamuzi huu na kwa sababu hatukupata mapendekezo yoyote ambayo yalikuwa yanarekebisha mapendekezo ambayo yaliletwa na Kamati, maana yake sasa ni Bunge limeshaazimia na haya ndiyo maamuzi ya Bunge kwa Serikali.

Katika ngazi hii wakati Wabunge mbalimbali wakichangia kuna muda watu walisema, pengine tunajikita zaidi kwenye kuishauri Serikali na kutunga sheria na kuisimamia, pengine tunapungua hivi; lakini hii ndiyo kazi yetu ya kuisimamia Serikali kwa sababu, hiki tunachoiambia sasa, haya ni maagizo kwa Serikali.

Kwa hiyo, Serikali uzuri baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri walipata kuchangia hapa na mmesikia wakieleza kwamba, haya yote ambayo yamesemwa humu hakuna aliyetoa mabadiliko yoyote kwa mujibu wa kanuni zetu. Maana yake ni yale yote ambayo tumeazimia, wao wanayachukua kama maelekezo ya Bunge na kwenda kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, katika ngazi hii ndiyo tumefanya kazi yetu ya kuisimamia Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo mafupi, namwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC),* Mheshimiwa Halima James Mdee, aje ahitimishe hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii, kwanza kuwashukuru Wabunge wote waliochangia hoja yetu kwa weledi na uzalendo wa hali ya juu. Kwetu tuna matamanio kwamba, huu uzalendo na weledi ambao Wabunge wameonesha na kuwa na uchungu na nchi yetu kuhusiana na hizi taarifa, basi wenzetu wa upande wa Serikali wangekuwa na juhudi zaidi za kuhakikisha kwamba hizi hoja za kikaguzi zinafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sisi Wabunge wakongwe, na Mheshimiwa Simbachawene anajua, kipindi cha hoja kama hizi kipindi kile unakuta Mawaziri wote wamejaa hapa wakati tunahitimisha, kwa sababu hakuna mwenye uhakika wa kesho yake. Yaani haikuwa poa. Hizi taarifa zinaondoka na vichwa, lakini inawezekana wanaona tumelainika kidogo, kwa hiyo, wanachukulia *simple,* ndiyo maana tunafanya hitimisho kwa hesabu za Mkaguzi Mkuu ambaye anakagua fedha zote ambazo zimekusanywa na wananchi, Bunge likaidhinisha maeneo mbalimbali ambayo wamepewa fedha, wakaenda wakafanya matumizi, *then* anakuja kukagua kama kilichofanyika ni halisi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinamgusa kila Waziri, kila Idara na Taasisi ya Serikali. Sasa tuko hapa, ndiyo kama hivi, tukiwahesabu hapa hawafiki hata 10, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, nashukuru Wabunge waliochangia ni 31, kwa sababu ya muda sitaweza kuwataja majina, lakini nitatolea tu ufafanuzi zile hoja za jumla ambazo zimezungumzwa na wengi. Nyingine nisipozitolea ufafanuzi haimaanishi kwamba siyo nzito, lakini kwa sababu tumeshapitisha mazimio na maazimio mwishoni naamini yatapitishwa bila kuletewa mabadiliko, Serikali itaenda kusoma ili ijue nini kilichoazimiwa ili waende wakatekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiujumla, kabla sijaenda kwenye hoja moja moja, nilikuwa naomba na kwa sababu, Spika wetu ni kijana, ni Spika *smart,* ni mtu wa mabadiliko, unayependa nchi yako, kabla hatujamaliza muda wetu ambao tunamaliza mwakani, kwa sababu tuna Kamati yetu ya Kanuni, tuweze

kuingiza kwenye Kanuni za Bunge uwepo wa siku mahususi ambayo tutakuwa tunapewa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ambayo yanahusisha pia maelekezo yote ambayo yalitolewa na Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kiujumla.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo mmeona, sisi Kamati ya *LAAC* tumeweza kukutana na halmashauri 55 kati ya halmashauri 184, lakini ndani ya kile kitabu kikubwa kuna halmashauri 184 ambazo pia zina maelekezo ya *CAG* ambayo akiwa kama jicho la Bunge, alichokiona kile amekiona kwa niaba ya Bunge. Kwa hiyo, ninaamini tukiwa tuna kanuni hii Serikali itachukulia kwa uzito utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, na utekelezaji wa hoja zote zilizokuwa *raised* na *CAG.*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2023 wakati ambapo ulianzishwa utaratibu mzuri ambao tuliufanyia kazi mwezi Juni, 2023 Kamati ya *LAAC* kwenye Taarifa yetu ile ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, kuna maneno fulani tuliyasema, na ninaomba nirudie kuyanukuu kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Spika, tulisema, "Kamati imebaini kutokuwepo kwa utaratibu maalum kwa ajili ya kuratibu zoezi zima la utekelezaji wa Maazimio ya Bunge baina ya Taasisi za Serikali, hali inayosababisha vielelezo muhimu kushindwa kufikishwa kwa CAG kwa wakati, kwa ajili ya kuhakiki kinyume na Ibara ya 143(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na Kifungu cha 11(a) na (b) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma".

Mheshimiwa Spika, kwa sisi ambao umetupa dhamana ya kufanya kazi kwa niaba ya Bunge, na ambao tunakutana na hizi taasisi, tunaona wazi kabisa kuna dharau fulani kwa jicho la Bunge wakati wanaenda kukagua. Dharau hiyo inasababisha kwamba, vitu ambavyo vingeweza kutatuliwa ndani ya muda mfupi vinachukua muda mrefu sana kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, ninaamini tukiwa tuna kanuni ambayo inawaelekeza hawa jamaa namna ya kufanya kazi watajilazimisha kuji-*tune* kwenda na mdundo kwa sababu,

nilichojifunza pia, ni watumishi wengi wa umma wa nchi hii, siyo wote, kuna waadilifu sana, lakini walio wengi wanapenda kufuatiliwa hapo nyuma ndiyo wafanye jambo. Usipowafuatilia, hawafanyi. Sasa kama tumeshajua ndiyo *culture* ya Kitanzania ya utumishi wa umma, ndiyo tulivyo yaani, mmenielewa? Lazima tutengeneze mfumo wa kufukuzana hapo nyuma kama vile wanavyofukuza kuku wa kienyeji.

Mheshimiwa Spika, bila hivyo inakuwa *business as usual*. Watu mara nyingi wanafanya siyo kile wanachokitegemea, siyo kitu ambacho wao wanaki-*expect* ila wanacho ki-*inspect,* ndiyo *human nature*. Ukiwa na *inspection,* watafanya wakijua huyu atakuja atachungulia, lakini kama unatarajia kufika mbinguni halafu hapa duniani unaishi maisha yasiyoeleweka, Mbingu utaiona? Huwezi kuiona.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba tuwe na kanuni ili hawa watu wetu tuweze kuwaweka kwenye tanuru fulani, ili siku tukiona kwamba, maazimio hayajatekelezwa licha ya kwamba, tumewaweka kwenye tanuru, tuweze kuwala vichwa bila *excuse*. Ndiyo hali ilivyo, na ndiyo watu wetu hao. Huo ulikuwa ni utangulizi.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye hoja, naamini nina muda. La kwanza ni Mpango wa Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri. Kama Kamati, nimesikia maoni ya Wajumbe wengi. Kamati yetu tumesema kwamba, Serikali za Mitaa 184 zinategemea Serikali Kuu kwa 98.999% na ninashukuru Profesa yupo hapa.

Mheshimiwa Spika, ugatuaji wa madaraka, pamoja na mambo mengine ulikuwa unalenga halmashauri zetu ziwe na uwezo wa kujitegemea. Inawezekana isiwe kwa 100%, lakini kuwe kuna mchango wa vile vichwa ambavyo tunavishusha kule chini kusaidia nchi ipate mapato kiujumla wake. Nadhani *that was the spirit. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapokuwa na halmashauri 184 zinapata shilingi trilioni 7.60, maana TAMISEMI bajeti yao haizidi shilingi bilioni 80 kama Wizara. *TARURA* kama chombo ambacho kiko TAMISEMI hakizidi shilingi bilioni 700; hizi nyingine zote zinaenda kwenye

Halmashauri. Kwa hiyo, inaweza ikaja halmashauri leo imepata ruzuku ya maendeleo, ruzuku kwa mtindo wa *OC* ambayo inajumuisha mishahara na yale matumizi mengineyo, inapewa shilingi bilioni 40. Kwa mfano, unaweza ukakuta mishahara ni shilingi bilioni 30, pesa ya maendeleo ni shilingi bilioni 10, wao wamekusanya shilingi milioni 500, hawa wamekusanya shilingi milioni 700. Sasa unajiuliza kuna faida gani ya kuwa na *brains* ambazo tumezishusha kwenye halmashauri? Tunatarajia zitumie fursa za kiuchumi zilizopo pale, wawe wabunifu, ili waangalie wataongezaje mapato yao, ili mapato ya Kapu la Taifa yaongezeke, Serikali Kuu ikikata pesa zote zina-*collapse*, zote ni muflisi.

Mheshimiwa Spika, halmashauri 184 leo Serikali Kuu iseme hatupeleki mishahara, hatupeleki ruzuku, ni muflisi. Sasa kuna maana gani ya kuwa na halmashauri za namna hii? Mkurugenzi anakuja anajivunia, anakwambia kabisa tumepunguza mapato kwa sababu, sisi tunategemea kilimo. Kwa hiyo, mvua hazikunyesha. Tunamwuliza, sawa, unategemea kilimo, dunia ya sasa hivi tunategemea mvua? Kwani huna vyanzo vya maji kwenye maeneo yako? Viko vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa unajiuliza kwa nini kama unajua wewe unategemea mazao, una vyanzo vya maji vya kutosha ama kuna mvua inanyesha mpaka inatiririka inapotea, kwa nini ama msitengeneze mabwawa ama muwe na mfumo wa umwagiliaji ambao uko *simplified? They don't care* kwa sababu, akikaa miezi miwili anapelekwa kwingine, akikaa miezi miwili anapelekwa kwingine na hakuna *key performance indicators* ambazo amepewa na asipo-*perform* hafanywi chochote. *We have to change*. Hili tatizo ni halmashauri zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunaambiwa tuweke mipango, yaani unakaanao unajiuliza, kwani sisi ni Bunge ama sisi ni nani? Ndugu zangu tunaomba *mentality* hii ya kufikiria ndani ya *box* iishe. Maana kuna wakati mwingine unajiuliza, au jumuiya za kimataifa zinazotupa mikopo zinatu-*restrict,* kwa sababu inawezekanaje tunapiga na hii? Kumbe sisi tuna-*enjoy* kuwa maskini. Unajua *it is possible as well,* yaani una-*enjoy* kuwa maskini,

ukipata vile vimikopo nafuu *IMF* na *World Bank,* maisha yameenda.

Mheshimiwa Spika, kuna halmashauri nyingine tunawauliza, kwa nini hamkusanyi inavyotakiwa? Wanasema, tunaweza kukusanya. Tukienda Wizara ya Fedha wanatuambia kuna *sealing,* semeni mnaishia hapa, lakini kusanyeni nyingine. Ndiyo mnaleta uwizi. Umempangia bajeti ya shilingi bilioni 110, kumbe mnajua wanaweza kukusanya shilingi bilioni 150, ile shilingi bilioni 40 inakusanywa ya ziada haina matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini utanipa muda. Kuna halmashauri moja tulikutananayo, sikumbuki jina, imechoka tu, yenyewe hii shilingi bilioni 1.52 ni mapato. Kwa hiyo, wameenda wakaongeza shilingi milioni 500, hapo wana madeni ya watumishi. Tukawauliza hivi hii shilingi milioni 500 mmeifanyia nini? Tumenunua gari la Mkurugenzi? Gari la mkurugenzi halikuwepo kwenye zile *activities* ambazo zilikuwa *planned*. Hazikuwa *priority* kwa sababu, *sealing* yao ilikuwa inajulikana. Wamepata ziada, sasa nawaambia wewe unanunuaje gari la Mkurugenzi wakati unajua unadaiwa na watumishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua wanafanyeje? Wanatuomba msamaha. Wanatuomba radhi, yaani ndiyo kichaka cha watu kukimbilia. *We have to change*. Yaani natamani tuwe na viongozi ambao tuna uchungu na hizi fedha za umma kwa sababu, Serikali haina fedha. Hizi fedha tunadunduliza walipakodi wadogo, wakubwa na wa kati. Tuwe na uchungu kama pesa yetu ya mfukoni, yaani nataka tufike pale siku moja nitoke hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hati za ukaguzi ni hoja imezungumzwa na nitaizungumza kidogo. Ni kweli tumepanda kidogo, mwaka 2021/2022 zilikuwa hati 170 za kuridhisha, 13 zenye shaka, na hati moja chafu. Mwaka 2022/2023 ambayo ni sasa, halmashauri 184, 183 hati zinaridhisha, moja hati isiyoridhisha, ni vizuri kabisa, lakini nyie mnajua kwamba hati inatoka kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kunapokuwa na ushahidi kuwa hesabu za halmashauri zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu, yaani wanapimwa tu, je,

viwango vya kimataifa vya uandaaji hesabu mme-*meet standard, principle,* yaani *only that,* lakini ndiyo kigezo kwamba, tumepiga hatua, Hapana. Ni watu wamejifunza tu kuandaa kwa viwango vya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusije tukakaa tunajidanganya eti ooh, sijui hamna! Ndiyo maana ningekuwa na saa tano ya kusoma Taarifa ya Kamati, yako ambayo umetupa *page* 100 matatizo ni yale yale. Kwa hiyo, madudu yapo, upigaji upo, ila tu wameweza kuandaa hesabu kwa *standard* za Kimataifa, yaani *balance sheet,* nashukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa wale Waheshimiwa mliokuwa mnasema kwamba mambo ni mazuri, mambo siyo mazuri. Nenda kasome Ripoti ya *CAG* ndiyo utajua mambo ni yale yale, ila watu wameweza ku-*meet standard* za uandaaji wa hesabu, lakini huku mashimo yapo, ndiyo maana mnalia hapa. Ndiyo maana nilikuwa nadhani ni muhimu sana ukaguzi wa ufanisi tukaanza kuutilia mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa ufanisi maana yake ni nini? Tumetoa shilingi bilioni moja ikajenga hospitali, je, imeenda kujenga na imejenga kwa *standard* iliyotakiwa? Je, imetimiza yale malengo tuliyotaka hiyo hospitali ikafanye kazi? Kama ni *100 percent,* tunasema *tick*. Siyo leo mnatoa fedha kujenga hospitali shilingi milioni moja, anakuja Mkurugenzi anasema niongezeni 300. Anaongezewa 300, haitoshi, anasema niongezeni 600. Yaani tunakuwa tuko kwenye *vicious circle*.

Mheshimiwa Spika, sasa tukianza kufanya ukaguzi wa ufanisi, na tukikuta mambo ni safi, ndiyo tutasema sasa tunaenda, lakini hii ya hati hizi za ukaguzi, hizi ni *story* tu ndugu zangu. Kwa hiyo, nataka hilo pia liwekwe wazi, kama *we are genuine* na kweli tunataka kuisaidia nchi hii tuvuke, twende *beyond* kufanya zile *standards* za kimataifa za kuandaa hesabu, hilo ni la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za mapato ya ndani kutokupelekwa kwenye miradi ya maendeleo, nadhani nahitaji kulizungumzia hili. Wabunge wamesema hapa kwamba kati ya changamoto nyingine kubwa ambayo Serikali mkiweza kuifanyia

kazi tutasogea ni watu ambao wamepewa dhamana ya kusimamia fedha za umma kufuata sheria, taratibu na miongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri zote 184 ambazo mimi nimekutana nazo, zote hakuna anayefuata sheria, taratibu na miongozo. Nitawapa mifano michache na nitawapa mifano kuhusiana na hizi fedha za maendeleo kutokana na makusanyo ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI ilitoa maelekezo yenye kumbukumbu Namba CBD.421/422/01/43 mwaka 2018 Januari na TAMISEMI kama mpo hapa, kama nasema uongo mnyanyuke mnipe taarifa. Barua hii ilizitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambazo kipindi hicho zilikuwa zimegawanywa katika kundi 'A' na 'B', na zilitoa maelekezo kwa mamlaka hizo kutenga 60% na 40% ya mapato yao ya vyanzo vya ndani kwa miradi ya maendeleo mtawalia.

Mheshimiwa Spika, baadae ikaja ikaongezeka mpaka *30% to 70%* katika Majiji, na hivi juzi mmebadilisha *20% to 80%,* japokuwa sisi kama Kamati tuna-*dispute* kwa sababu tunaona mnataka ku-*create* uzembe. Sasa hiyo ni hoja ya maelekezo ya TAMISEMI chini ya 2018.

Mheshimiwa Spika, vilevile, aya ya 83.3 na aya ya nne ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mipango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023 ya Novemba 2021, iliwaagiza Maafisa Masuuli ambao mapato yao ya ndani yanazidi shilingi bilioni tano kutenga 60% ya mapato yao kwa shughuli za maendeleo na Halmashauri ambazo mapato yao ya ndani yako chini ya shilingi bilioni tano kutenga 40% ya mapato yao ya ndani kwa shughuli za maendeleo. Hii ina-*compliment* nilichokizungumza, lakini inaenda mbele zaidi kuelezea kwa mantiki ya kwamba ilikuwa ni mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti, hiyo ni 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, sasa leo mkaguzi anatuambia fedha hazijaenda. Sasa najiuliza, Mkurugenzi unapoteuliwa kwenda kwenye eneo, hivi aliyekuteua anakuteua kwa sababu anataka uende tu ubadilishe makazi ama anataka uende kubalisha

maisha ya wananchi uliotumwa ukawatumikie? Yaani maana ya kutuma wataalam kule ni nini? Ni kwamba maisha ya Watanzania yaweze kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuna kanuni hizi na kuna miongozo hii inakiukwa. Hili siyo jambo jipya. Ukiangalia Maazimio ya Bunge ya mwaka 2023, tatizo linajirudia. Maazimio ya Bunge ya mwaka 2022, tatizo linajirudia na mwaka huu 2023, tumekuta hayo mabilioni ambayo tumeyasema ambayo sitaki kuyarudia; tuseme haya Majiji matatu, fikiria Jiji kama la Dar es Salaam, tujiulize, hivi shilingi bilioni 21 zingeleta *impact* gani? Shilingi bilioni 21, na ninavyolizungumzia Jiji la Dar es Salaam nazungumzia Jimbo la Ilala na Ukonga. Si Majimbo mawili tu! Na Segerea ni Majimbo matatu. Hii hela ingeleta *impact* kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Majiji haya yanakusanya mabilioni ya fedha, nendeni mwaulize, mna mradi gani wa kimkakati? Dada yangu wa Temeke sijui yupo? Yupo hapa! Yaani waulizwe, hivi mmefanya mradi gani? Hakuna. Sasa unajiuliza, yule wa kule Bunda Vijijini asemeje? Yule wa kule Nkasi asemeje?

Mheshimiwa Spika, Singida hatukuwataja, lakini mmo, mnapaswa kupeleka shilingi bilioni nne, mnapeleka shilingi bilioni 2.3 katika kipindi cha miaka mitatu. Sasa wananchi wataendelea? Haiwezekani. Sasa mnategemea Mheshimiwa Rais kawateua, yaani unajua kuna vitu vingine unawaonea huruma hata watu ambao ni viongozi wakuu wa nchi, kwa sababu wao wameteuliwa wakawe miguu yake, mikono yake na wakawe pumzi yake, halafu unaenda unatulia. Hatuwezi kuruhusu hivi! Ndiyo maana tunaumia sana tunapoona tunatoa Maazimio ya Bunge na hayafanyiwi kazi kwa utekelezaji wake. Haionekani watu wana uchungu wa kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema kwa niaba ya Bunge, mlitupa kazi, ndiyo hivyo; tatizo waliopewa dhamana hawafuati sheria. Hili alizungumza Mheshimiwa Zahor, na kwamba wanakiuka miongozo wanayopaswa kuifuata, hatua hazichukuliwi na fedha za umma zinatumika ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani anasimama Mweka Hazina wa Jiji la Dar es Salaam, alikuja pale, unamwuliza, hizi shilingi bilioni 21, kwanza mlizitumia wapi? Anasema, tulitumia kwenye matumizi ya kawaida. Yaani kutokana na mabilioni ya Jiji, wanatakiwa 30% watumie kwenye matumizi ya kawaida na 70% wapeleke kwenye maendeleo. Bahati mbaya, tena pamoja na utajiri wao huo, bado Serikali inawapelekea *OC*. Unakuja unamuuliza, kwa nini hujapeleka shilingi bilioni 21 kwa ajili ya wananchi wapate maendeleo? Anasema, fedha za *OC* hazitoshi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Ilala pale yaani ukichukua bodaboda unaizunguka uinaimaliza yote. Sasa hayo Majimbo ya wenzetu huko ambayo ukifika kutoka Kata moja kwenda nyingine unatoka asubuhi mpaka jioni; wakati Dar es Salaam ukichukua bodaboda ukijaza mafuta unazunguka unaimaliza ile Ilala. Sizungumzii Dar es Salaam. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya wazabuni, tunaiomba Serikali ilifanyie kazi kwa umakini na tunaomba mkafanye *harmonization* ya taarifa zenu, kwa sababu linaweza likaonekana ni deni dogo kwa *figure,* lakini Mkaguzi anasema katika Mamlaka 37 kati ya 184 madai yameongezeka toka shilingi bilioni 64 mpaka shilingi bilioni 87, yaani ongezeko la 35%.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HALIMA J. MDEE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu kengele imegongwa nitaenda haraka haraka. Naiomba Serikali hili eneo bado kuna *gap* kubwa, wakalifanyie kazi kwa ufanisi mzuri, kwa vile tatizo lililopo ni kubwa, kwa sababu sisi tunakutana na Halmashauri moja moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya 10% imejibiwa kwa kadri ilivyojibiwa, lakini tulisema kwenye hotuba yetu kwamba Kamati tatu zilikutana na tulikutana na Mheshimiwa Naibu Waziri, tukapitishwa, kwa sababu Bunge halikushirikishwa kwa namna yoyote kuweza kushauri kufuatia huu utaratibu mpya. Sisi tulifanya kupitishwa wakati mambo mengine yanaendelea, Kamati ya Bajeti, *LAAC* na TAMISEMI tuliona kuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, unajua Serikali huwa ndiyo imeshikilia; sijui niseme sisi tuko kwenye makali, sijui *the other way round,* lakini inavyoonekana Serikali ikiamua jambo lake inaenda kutekeleza tu hata msemeje, inaenda kutekeleza tu, *you know*. Naishauri TAMISEMI, yale maoni ambayo tumeeleza hapa, mkasome mfanye marekebisho, kwa sababu sasa hivi shilingi bilioni 79, Mheshimiwa Waziri umesema mmelipa shilingi bilioni 20, lakini sasa tatizo la masuala ya kikaguzi siyo maneno matupu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dugange hapa ni rafiki yangu, haiwezekani tuko wote kwenye Kamati, hizi hoja zipo, Mkaguzi hajui kama mlishalipa shilingi bilioni 20, imeshuka kutoka 20. Maana yake unafanya *79 minus* 20. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba kwa sisi Kamati ya *LAAC* mpaka sasa tumekuja hapa madeni, chechefu ni shilingi bilioni 79 yaliyokuwa nje ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, yaliyokuwa ndani ya mkataba ni changamoto nyingine; kwa sababu huko chini unakuta kwa mfano, umepewa mkopo, kwa mkataba unatakiwa ulipe ndani ya mwaka, unakuta mtu hajarejesha mwezi wa kwanza, mwezi wa pili, mwezi wa tatu na mwezi wa nne. Wale Wamama Maendeleo wanasema, huyu alitakiwa arudishe shilingi 800,000 kwa miezi nane, lakini miezi nane hajarudisha hata shilingi 100/=, lakini kwa sababu bado yuko ndani ya mkataba, hatuna shida naye.

Mheshimiwa Spika, sasa unajiuliza kama kwenye miezi nane alishindwa kurudisha shilingi 800,000/=, hivi huyo mwezi wa Tisa na Kumi ndiyo atarudisha shilingi milioni moja? Hiyo ni *common sense!* Kwa hiyo, hayo hatujayazungumzia hapa. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Naibu Mawaziri, naona Waziri yuko *busy* sana leo hayupo, hili jambo mkaliangalie, kwa sababu mnatarajia kwenda kutoa shilingi bilioni 227, tumeshauri muanze na *pilot* kwenye *few* Halmashauri ili tujifunze. Mkiamua kwenda kibabe, sawa tutakuja kukutana tu hapa hapa, halafu nadhani kipindi hicho tukishakutana tutaweza kunyooshana pia vizuri, kwa sababu *Hansard* za Bunge zipo *clear* kwamba tumewaonya.

Mheshimiwa Spika, mradi kutokukamilika ni hoja ambayo mwaka 2023 ilikuwa shilingi bilioni 112, mwaka huu 2023 ni shilingi bilioni 206. Maana yake ni nini? Ni kwamba Maazimio ya Bunge yaliyoelekeza wakatatue hii changamoto ya shilingi bilioni 112 hawakwenda kuitafutia ufumbuzi, imeongezeka imefika shilingi bilioni 206.

Mheshimiwa Spika, sasa tukisema inaonekana kama tuna nongwa, lakini lazima tuseme kwa sababu hii ni nchi yetu. Huwezi kuahirisha tatizo leo, yaani unapooza unasema kesho mimi si nitaondoka atakuja mwingine, lakini si tunaishi hapa hapa! Yaani lazima tuwe na *mentality* kwamba unapiga mzigo kama vile hufi. Siyo unafanya kazi tu asteaste ukiamini kwamba kesho nitatolewa hapa nitapelekwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kuna Mkurugenzi mmoja kwenye taarifa yetu ya mwaka 2022 Bunge liliagiza kukafanyike kaguzi maalumu kwenye Halmashauri yake kwa sababu alikuwa amefanya ovyo kwenye halmashauri yake, sitataja mtu jina. Akatolewa akapelekwa Halmashauri nyingine, tukakutana naye tena kwenye Halmashauri nyingine. Tukamwambia, wewe umeshahama? Anasema, ndiyo. Juzi tena tunakutana kwenye Kamati kwenye Halmashauri nyingine, tukamwambia ndugu yetu una bahati, wewe unahamishwa vituo tu; lakini msingi wake wa kwanza, tuliomba ukaguzi maalumu, kwa sababu *you didn't perform* kwenye Halmashauri yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo inakuja hoja, namna gani tunawapata Wakurugenzi? Mzee wa Mipango Mheshimiwa Profesa, naomba msugue kichwa mtuambie, siyo mipango ya *story*! Kwa sababu hapa kuna mtu alisema hivi, taasisi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Endelea, taasisi... usije ukakatisha sentensi sasa, tutakuwa hatujaelewa ulichokuwa unataka kusema. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, nasema hivi, mafanikio ya taasisi yoyote ama mafanikio ya familia yoyote

nyumbani, yanategemea *head,* ama *head of institution* ama *head of the family* yukoje. Ukiwa na *head of the family* kiazi, ukiwa na *head of the institution* kiazi, mafanikio hayapo, kwa sababu tuna utaratibu wa kuangalia mkubwa aliye juu yetu ana *vision* gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana utaratibu wa upatikanaji wa Wakurugenzi, kama ambavyo wenzetu wa *PAC* wamesema, kuwe na utaratibu mahsusi unaofanyiwa *research* ya kutosha na uliofanyiwa vipimo ukapata ithibati ya kutosha. Tukiweza kufanikiwa, hapo, tunaweza tusimalize matatizo, lakini tutapunguza tatizo kwa sehemu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, jana kuna hoja ya Biharamulo iliyozungumzwa, niweke *clear* kwa ufupi sana kwa sababu iligusa jicho la Bunge. Kwanza, ni muhimu Bunge likajua, tulikutana na Halmashauri ya Biharamulo juzi Oktoba 2024 na hapa kuna barua ya Mkurugenzi ambaye anaitwa Innocent Mukandala. Taarifa ambazo zimeandikwa kwenye ripoti ya *LAAC* ambayo chanzo chake ni ripoti ya *CAG,* na *CAG* anafanyia *financial statements* za kwenye Halmashauri, hatoi vitu vyake kichwani.

Mheshimiwa Spika, ile taarifa iliyozungumzwa kuhusiana na Biharamulo na nimepitia *LAAC Book* yao, Kitabu chao cha Halmashauri kina kurasa karibia 551. Ukitaka nitakupatia nakala. Kilichoandikwa na Kamati ndicho halisi. Sasa kama Mkurugenzi amesikia Halmashauri yake inatajwa anataka kujitetea ili labda asiliwe kichwa, aende akarekebishe hesabu zake kwa sababu Mkaguzi anaangalia taarifa zao za fedha kuanzia pale ndiyo anakuja na maoni na mapendekezo na kushauri. Warekebishe nyumba zao, siyo wana-*panic.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie, nashukuru kwa kunivumilia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima kwa sababu...

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo.

**SPIKA:** Subiri kwanza, kwa sababu unazungumza hapo taarifa Rasmi za Bunge hatutaelewa unazungumzia nini?

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, *okay,* nitazungumza kwa ufupi kwa sababu sina rejea hapa. Kati ya Halmashauri ambazo tulisema hazijatimiza malengo yake ya makusanyo, miongoni mwa Halmashauri hizo ilikuwa ni Biharamulo ambayo ilifanya *estimation* ya shilingi bilioni 3.5, ikaja ikakusanya shilingi bilioni mbili na kadhaa hivi lakini ikawa kuna *deficit* ya 35%.

Mheshimiwa Spika, alivyokuja Mheshimiwa, lakini alizungumza vizuri tu, nami wala sina shida na alichokizungumza, alikiri kwamba kulikuwa kuna *misinformation* na vitu kama hivyo. Sina shida na alichokizungumza, ila kwa kuwa limeguswa jicho ambalo ni la Bunge ikanilazimu nikarejee kile kitabu cha Halmashauri chenyewe kwa ukubwa wake ili kuangalia hiki kitu kimetolewa huku ama kimetolewa wapi? Nikakuta kile ambacho kilikuwa *reported* kule ndicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakija hawa ndugu zetu huwa tunawasomea. Kikao chetu tunaonekana tunachimba mikwara, lakini tunawaambia ukweli.

**SPIKA:** Ngoja, unaposema "Mheshimiwa", unamaanisha Mbunge au unamaanisha "Waziri wa TAMISEMI?"

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Biharamulo.

**SPIKA:** Mbunge wa Biharamulo.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ahaa *okay.*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, ndio alikuja na hoja kuonesha kwamba hiyo siyo. Sasa ndiyo maana nimesema...

**SPIKA:** Sawa. Sasa ili taarifa zetu zikae vizuri, yeye kasema hivyo sivyo, lakini wewe ulivyoenda kusoma umezikuta hizo taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, *yes*.

**SPIKA:** Kamati, tangu taarifa hii itoke mwezi wa tatu mwaka huu hamjaletewa taarifa yoyote ya ziada.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, hatujaletewa na uzuri ni kwamba, taarifa zikishatoka mwezi wa Tatu, maana yake Wakaguzi wanarudi tena kule kwenye maeneo yenye hoja za kurekebisha.

**SPIKA:** Kwa hiyo, hakuna jambo jipya.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, hakuna jambo jipya ambalo tumeletewa. Kwa hiyo, nilisema tu niliweke wazi hili kwa ajili ya kumbukumbu nzuri za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa, maazimio ambayo sisi tumewasilisha mbele ya Bunge lako ni maazimio makubwa 11 ambayo ndani yake yana A, B, C, D na E, ambapo kuna maazimio 33 hivi kwa ujumla wake ambayo tumeyaleta mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kimekuwa tofauti sasa hivi, kwa sababu Halmashauri tumekuwa tukikubaliana nao kwenye vikao, tumeweka na mwaka wa utekelezaji wa maagizo husika, tumeweka kabisa kwamba *by this date*, kwa kuzingatia mazingira tofauti tofauti ya kifedha na mambo mengine ambayo tulijadili nao, tumeweka kwamba *by this*, na wao wamekubali kwamba muwe mmetekeleza.

Mheshimiwa Spika, hapa vilevile tumeleta hivyo hivyo kusoma taarifa yetu, *deadline*, kwa Halmashauri na Serikali Kuu, kwa hiyo, tunaamini kwamba kwa kuwa tumewasaidia kuwawekea tarehe, tutakuwa katika muktadha huo huo wa kusukumana ili wajue kwamba tusipofanya, tutaonekana hatujafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba; sasa Bunge likubali maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ili yawe Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji baada ya hoja hii kuungwa mkono.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu Zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023 iliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki, ahsanteni sana. Kwa hiyo, yale ambayo awali yaliletwa kama Mapendekezo kwa Bunge sasa ni Maamuzi ya Bunge baada ya kuwahoji. Kwa ngazi hii, kwa sababu ni katika ile kazi tunayoifanya ya kuisimamia Serikali, haya yanaenda upande wa Serikali, siyo

kama maoni na mapendekezo tena kwa sababu yameshakuwa maazimio yanakuwa ni maagizo upande wa Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* Mheshimiwa Augustine Holle Vuma aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. VUMA A. HOLLE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA *(PIC)*:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nyingine ya kusimama hapa kwa mara nyingine tena ili niweze kuhitimisha Hoja ya Kamati iliyowasilishwa hapa Bungeni siku ya tarehe 29 Oktoba, 2024.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja zote tatu na kimsingi wamechangia kwa uzalendo mkubwa sana na uchungu wa hali ya juu taarifa hizi. Kwa upande wa taarifa ya *PIC,* moja ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegusia ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka kwa utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini;

(ii) Kusuasua kwa utendaji wa baadhi ya mashirika ya umma;

(iii) Upungufu wa mitaji;

(iv) Msukumo mdogo wa taasisi na mashirika ya umma kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(v) Miradi ya uwekezaji kutokamilika kwa wakati;

(vi) Upembuzi wa wakandarasi wanaopatiwa miradi ya uwekezaji kutofanyika kwa kina;

(vii) Namna ya upatikanaji wa Watendaji Wakuu wa Taasisi pamoja na Wajumbe wa Bodi na mifumo ya uwajibishaji;

(viii) Mashirika na taasisi za umma kutotumia fursa walizonazo; na

(ix) Kushindwa kutumia vyanzo mbadala vya upatikanaji wa mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge takribani 26. Naomba kwa sababu ya muda nisiwataje, lakini nawapongeza na kuwashukuru wachangiaji wote waliochangia katika taarifa ya Kamati ya *PIC* kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa lengo la kusisitiza yale tuliyowasilisha kwenye Taarifa ya Kamati na pia kufuatia michango ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani kwa siku hizi tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba niguse mambo machache ili niweze kuweka msisitizo. Jambo la kwanza ni kuhusu taasisi na mashirika ya umma kuongeza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha mashirika haya ni ili yajiendeshe kwa ufanisi na baadaye yaweze kujitegemea, lakini hali ni tofauti, utegemezi unaongezeka mwaka hadi mwaka, hata kwenye kipengele cha mishahara na matumizi ya kawaida, hali inayotia mashaka.

Mheshimiwa Spika, tulitegemea kama Bunge kwamba kwenye taasisi hizi angalau wadai au waombe ruzuku kutoka Serikalini kwenye miradi ya maendeleo, yaani kwenye fedha za maendeleo, lakini kwa bahati mbaya sana hata mishahara na matumizi ya kawaida ya taasisi hizi bado wanategemea ruzuku kutoka Serikalini jambo ambalo kwa kweli halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mashirika ambayo yanajiendesha kibiashara nayo yanaongeza utegemezi badala ya kupunguza. Kimsingi hiki ni kigezo ambacho wamewekewa kama kigezo cha utendaji. Kama Kamati, tunataka kuona Msajili wa Hazina, ambaye ndiye Msimamizi wa Mashirika haya, akikaa na haya mashirika ya kibiashara, achambue sababu zao, achambue changamoto zao ili aweze kuwafungulia minyororo ya kiutendaji kwa sababu kuna changamoto ya minyororo ya kiutendaji katika mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, unakuta taasisi ina mtendaji mzuri kwa maana ya Mkurugenzi Mkuu, ina bodi nzuri, ina mipango mkakati mizuri lakini wakitaka kuanza kutekeleza baadhi ya mipango yao au wachukue hatua kwenye utekelezaji wa majukumu yao, kuna minyororo ya kiutendeji ambayo inawafunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, unakuta taasisi inaweza kuajiri, na ina uwezo wa kuajiri watumishi, lakini kutafuta vibali vya ajira ni changamoto. Wanaomba vibali waweze kuajiri kwa hela zao, lakini Serikali inachelewa kutoa vile vibali vya ajira. Wakati mwingine hata wakitoa, wanatoa vya muda mfupi. Kwa mfano, hapa kuna taasisi ya *CPB*, ile Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Wao huwa wanaomba vibali kwenye mamlaka ili waweze kuajiri, lakini mamlaka inakuwa inawapa vibali vya miaka miwili. Yaani wanatoa kibali kwamba ajiri watu 20 kwa miaka miwili miwili. Maana yake ni nini? Wakija pale wale watu wanaanza kufundishwa kufanya kazi vizuri, wakisha-*capture* vizuri wakaelewa namna nzuri ya kufanya kazi yao vizuri, kwa sababu hapa hakuna uhakika wa ajira, wanapata ajira sehemu nyingine wanaondoka. Kwa hiyo, bodi inaanza tena upya kutafuta watu wengine baada ya kupata kibali. Kwa hiyo, hii minyororo ya kiutendaji ni changamoto sana. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, pia ziko taasisi ambazo zina uwezo wa kukopesheka kutokana na mizania ya hesabu zao jinsi ilivyo. Wanataka kukopa lakini ili waweze kukopa lazima waombe kibali kutoka Hazina. Wakienda kuomba kibali, unakuta mchakato wa kupata kibali ili waweze kukopa unachukua muda mrefu mno.

Mheshimiwa Spika, ziko taasisi ambazo shughuli zao ni za msimu. Kwa mfano, taasisi inafanya shughuli ya mazao, inataka ichukue mkopo ili iweze kuwahi msimu wa zao fulani, wanaomba kibali wakope benki fulani, lakini mchakato wa kuwapa kibali unachukua muda mrefu. Kibali wanakuja kukipata ile fursa ya biashara imeshapita, inakuwa haina maana tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwenye manunuzi huwezi kuamini ziko taasisi ambazo hata vifungashio kwenye miradi yao, kwa mfano *NFRA* na *CPB* hata vile vifungashio, kununua madumu ya kuwekea mafuta wanayotengeneza na magunia yale,

wanafuata mchakato wa manunuzi. Sasa huyu atashindanaje na kampuni binafsi? Anafuata mchakato wa ununuzi kununua magunia na madumu ili kuweza kufunga bidhaa akauze sokoni. Kwa hiyo, huyu ni ngumu sana kuweza ku-*compete* na *private sector*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni upungufu wa mitaji. Katika mashirika ambayo uchambuzi umefanyika na kuonekana kuwa yanapaswa kupewa mtaji kutoka Serikalini, tunataka Serikali itoe mtaji kwa mashirika hayo kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kuweza kuongeza ufanisi kwenye taasisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri hapa ni benki ya *TIB*. *TIB* kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali iliji-*commit* kuwapa mtaji wa shilingi bilioni 118, lakini mpaka leo haijakwenda hata shilingi 10/=. Waliji-*commit* baada ya kuona hesabu zao zilivyo, kwa sababu walibadilisha *management*, wakaleta *DG* mpya pale, mambo yanakwenda vizuri, lakini mtaji hawana. Wametuambia wao Bungeni kwamba watapeleka shilingi bilioni 118, lakini hapa tunavyoongea leo hata shilingi 10/= haijaenda. Halafu, mwaka huu wa fedha tunaoutekeleza hawajawatengea hata shilingi 10/=. Hii haiwezi kukubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *MSD*. Hawa tuliwatengea shilingi bilioni 500 hapa hapa Bungeni. Kwa nini? Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi tulilalamika sana kwamba Ofisi ya Rais ambayo Waziri ni Rais mwenyewe, anakwenda kujenga vituo vya afya majimboni kwetu, anatoa hela ya kununua vifaatiba kupitia halmashauri zetu, halmashauri zetu zinapeleka hela *MSD* kwa ajili ya kununua vifaatiba, *MSD* kwa sababu hawana mtaji wa kutosha anakuwa tena siyo *Medical Store Department,* anakuwa ni *Medical Agent Department*. Kwa sababu, hana hivyo vifaatiba, hana dawa, anategemea halmashauri, tumpelekee fedha ndiyo aagize mzigo kutoka India au nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba, hapa sisi kama Wabunge tunaanza kulalamika, kwamba *MSD* haifanyi kazi yake vizuri. Halmashauri imetoa shilingi milioni 500 vifaatiba havijafika, huu ni mwezi wa saba au wa nane. Kumbe hawa hawana mtaji

wa kutosha, tulikubaliana tuwape shilingi bilioni 500 ili waende ku-*procure*, wanakuja ku-*store* kama ambavyo ndiyo kazi yao halafu tukitaka tukanunue kwao. Wakanunue, tena hawajapewa hata shilingi 10 mpaka tunavyoongea sasa hivi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tujifunze kutoka kwenye benki ya *TCB*. *TCB* walikuwa na changamoto kubwa sana ya mtaji, wakaja kwenye Kamati, tukazungumza nao, tukakaa na Serikali pamoja nao, wakawapa mtaji wa shilingi bilioni 131. Kwenye mwaka huu wa fedha unaoendelea kwa miezi sita ya mwanzo wametengeneza faida ya zaidi ya shilingi bilioni 20. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba ukiiwezesha taasisi ambayo unadhani kwamba inapaswa kuwezeshwa ni ukweli usiopingika kwamba inaweza ikafanya maajabu. Ndani ya miezi sita *TCB* imetengeneza zaidi ya shilingi bilioni 20 faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, taasisi ya *STAMICO* ilikuja kwenye Kamati ikiwa inachechemea miaka kama minne iliyopita nadhani. Wakati ule Waziri wa Madini, kwanza walikuja tukawafukuza kwenye Kamati halafu tukawaambia waje na Mheshimiwa Waziri kutoa *commitment*. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wakati ule akiwa Waziri wa Madini, akaja akaji-*commit* vizuri pale. Akabadilisha menejimenti, aka-*equip* na mtaji wa kutosha. Leo hii *STAMICO* ni taasisi ya Serikali inayojiendesha yenyewe na inatoa gawio kubwa kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi taasisi zote ambazo tumejiridhisha kwamba zinapaswa kupewa mtaji na Serikali, wapewe. Pia, mashirika yale ambayo yanajiendesha kibiashara ambayo mizania yake ya kifedha iko vizuri na wanayo fursa ya kutumia masoko ya mitaji, hapa, kuna hisa na hatifungani. Yale ambayo yako vizuri, Serikali iondoe minyororo ambayo inashindwa kuwawezesha kutimiza hilo.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri hapa, tunao *TANGA-UWASA*, Mamlaka ya Maji ya Tanga. Wali-*list* hatifungani zinaitwa *green bond* kwenye soko la hisa, wamekusanya zaidi ya shilingi bilioni 50. Wangetegemea fedha hizi zitoke Serikalini, inawezekana wangesugua benchi sana na wasizipate. Kwa hiyo, nadhani Serikali iweke mazingira mazuri na wezeshi. Hii nayo ni *alternative*

*way of financing,* miradi yetu ambayo tunaitekeleza kupitia mashirika yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna ubia na *private sectors*. Hii ameongea Mheshimiwa Tarimo leo. Kuna kile kiwanda cha ngozi cha Moshi, tija pale haipo kabisa kwa sababu kina-*operate* sijui chini ya 20%. Pale kama sisi hatuwezi, siyo dhambi kufanya ubia na *private sector*. Wakaja pale wakaongeza mtaji, wakaongeza teknolojia, wakaongeza ufanisi na hatimaye kiwanda kifanye kazi vizuri. Huwa tunakwenda kutembelea pale, na kila tukitembelea wanakuwa na viatu *pair* chache ambazo wanawapatia, lakini haisaidii chochote. Kiwanda kizuri, *very potential*. Tusiogope kufanya maamuzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ninataka kusisitiza ni kuhusu uchangiaji kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Sheria inayataka mashirika na taasisi za umma kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia: moja, gawio; mbili, michango ya 15%; na tatu, michango mingineyo.

Mheshimiwa Spika, msukumo wa taasisi na mashirika ya umma kuchangia bado ni mdogo sana, kwa maana ya kwamba uchangiaji hauridhishi, lakini pia hakuna mifumo ya uwajibishaji kwa ambao hawatekelezi takwa hili la kisheria. Hali ni mbaya zaidi kwenye taasisi na mashirika ambayo Serikali tuna hisa nyingi ukilinganisha na kule ambako tuna hisa chache. Yaani wale ambao tunamiliki 51% kwenda juu, ndiyo ambao kimsingi wanafanya vibaya zaidi katika kutokupeleka gawio na michango Serikalini. Hawa ambao umewekeza kidogo, labda kwa sababu kuna mchanganyiko na *private sector,* ndio wanaojitahidi na ambao michango yao inaongezeka mwaka hadi mwaka. Hawa wengine wanafanya vibaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inapaswa kuzisimamia kikamilifu taasisi hizi na kuhakikisha kwamba zinachangia kwa mujibu wa sheria. Serikali pia iweke mifumo ya uwajibishaji kwa wanaokiuka. Haiwezekani mtu anakuja kutoa mchango au gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali mpaka ajisikie yeye mwenyewe, na hakuna namna ambavyo anawajibishwa. Yaani mtu hapeleki mchango, mkikagua hesabu zake anapaswa kupeleka mchango

zaidi, lakini anapeleka kidogo au hapeleki kabisa na hawajibishwi. Hatuwezi kwenda namna hii, hapana. Hili ni takwa la kisheria, kwamba taasisi hizi zipeleke mchango kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Kasulu Vijijini tunahitaji fedha kwa ajili ya maendeleo kwenye miradi mbalimbali. Kwa hiyo, haya mashirika yakiongeza uchangiaji kwenye gawio na michango mingineyo na hii 15% tunaamini hata Kasulu zitafika kwa Mheshimiwa Mzee Lukuvi zitafika, Kibakwe zitafika, kote zitafika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja ya msingi hapa ni kuwasimamia vizuri ili kuhakikisha kwamba wanaongeza mchango kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Wote tunategemea Mfuko Mkuu wa Serikali. Sasa kama hawapeleki, tutapata kitu gani? Kwa hiyo, kuwe na utaratibu. Bodi imeshindwa, kwa sababu hiki ni moja ya kigezo cha utendaji wa bodi na taasisi hizi, yaani ni moja ya *KPI*. Ameshindwa kutekeleza hilo, basi bodi na menejimenti wawajibishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne nataka kuzungumzia kidogo kwenye upatikanaji wa watendaji wa taasisi na mashirika ya umma. Suala hili la upatikanaji wa Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma limeongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini ninaomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge. Kamati imepata fursa ya kuchambua Muswada wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma ambao Serikali imeuleta Bungeni, *so far* uko Bungeni. Ibara ya 16(a) imeweka sharti la upatikanaji wa Watendaji wa Mashirika yanayojiendesha kibiashara kwa ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumefanya *discussions, of course* tumekubaliana na Serikali kwa maana ya yale mashirika ambayo yanafanya biashara, upatikanaji wa Watendaji Wakuu wake; baadaye kama Muswada ukija kadri Mheshimiwa Spika atakavyopanga ratiba zake, basi itakuwa ni sheria sasa kwamba watendaji hawa tutawapata kwa namna ya ushindani. Kwa hapo tunaamini muda siyo mrefu tutatoka kwenye huo mkwamo ambao tulikuwanao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Wakati anachangia leo hoja hizi tatu kimsingi amenikosha sana moyo wangu na Kamati nzima. Moja, amekubaliana na mapendekezo yote ambayo tumeyapendekeza kama Kamati na pia, amekubaliana na changamoto ambazo tumezibainisha kwenye taarifa yetu kama Kamati, kwa sababu Msajili wa Hazina yuko chini yake, yeye ndio bosi wake na ndio mlezi wa mashirika haya, tunaamini watafanya kazi bega kwa bega ili kuhakikisha wanafanyia kazi mapendekezo yetu na yale yote ambayo tume-*discuss* hapa kwa lengo la kuleta tija kwenye uwekezaji mkubwa ambao Serikali imeufanya na inaendelea kuufanya kwenye mashirika ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi nilioutoa hapo juu, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka 2022/2023 ili yawe Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada sasa nitawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 iliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya ambayo yamesemwa kwenye Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa

Mitaji ya Umma, yalikuja hapa Bungeni kama Maoni na Mapendekezo na sasa baada ya Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hoja ya Mwenyekiti wetu kuhusu taarifa hiyo, pia baada ya kuwahoji na ninyi nyote na kusema ndiyo, basi haya yote yanakuwa ni maamuzi ya Bunge. Kwa hiyo, yanaenda Serikalini kama Maagizo kwa sababu ngazi hii ni ya kuisimamia Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa zetu hizi tatu tumezihitimisha siku ya leo kwa haya ambayo yametajwa kwenye kila taarifa na upande wa Serikali wameshayasikia hapa kwa utaratibu wa kawaida, kama ambavyo tulifanya kipindi kilichopita, pamoja na mapendekezo yaliyotolewa hapa ambayo nitayasema hivi punde.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu unayesimamia Sera, Bunge na Uratibu upo hapa, ili tuwe tunaenda vizuri, ili Bunge liwe linapata mrejesho, utaratibu ambao tumeuweka, nadhani ni mzuri kwa sababu yale mapendekezo ya mpango huwa yanasomwa tarehe 11 Machi, kila mwaka na tunafanya hivyo kabla ya kuanza Kamati. Basi taarifa hii kama ambavyo tuliagiza kipindi kilichopita, ilifikie Bunge mwishoni mwa mwezi wa Pili, ili Bunge liweze kupitia hizo kwenye Kamati, tuone haya maagizo ambayo Bunge imetoa mmefika nayo wapi? *(Makofi)*

Mengi ni ya kipindi cha muda mfupi, yanatakiwa tu kufanyiwa maamuzi halafu mabadiliko yaonekane, mengine ni ya muda wa kati. Kwa hiyo, mtatueleza wakati huo mtakuwa mmefika wapi? Yale ya muda mrefu pia tutayasikia kutoka kwenu kwamba mmejipanga kuyafanyia kazi kwa sura gani? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mwishoni mwa mwezi wa Pili tupate mrejesho, katika hii miezi mitano mtakuwa mmeyafanyia kazi mangapi? Kwa kiasi gani na tunasonga namna gani?

Waheshimiwa Wabunge, maazimio haya ambayo yamefanywa na Bunge siku ya leo, sina haja ya kuyarejea kwa sababu yako kwenye vitabu na sote tumeshayajua ni yapi. Ni

muhimu sana upande wa Serikali, yale ambayo yanaliingizia Taifa hasara kadri muda unavyokwenda hayo msiyaweke kwenye mipango ya muda mrefu, myaweke kwenye muda mfupi ili ile hasara isiendelee. *(Makofi)*

Kwa mfano, haya maelezo yaliyotolewa na Kamati yetu ya *LAAC* kuhusu Benki ya *DCB* na kwamba zile halmashauri za Dar es Salaam fedha yao inazidi kuporomoka; mpaka sasa hivi wameshapoteza zaidi ya shilingi bilioni 16. Maana yake fedha zinavyozidi kubaki hapo zilipo zinaendelea kuporomoka. Kwa hiyo, mambo kama hayo lazima yafanyiwe kazi kwa haraka ili kutokuendeleza hiyo hasara iliyopo. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo ni la muda mfupi pamoja na kwamba wakati mwingine kwa nchi inayoendelea kama yetu, kwa kweli vipaumbele vinakuwa vingi na kila mahali ni lazima uguse na kunakuwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha.

Kwa yale yaliyoelezwa na yale maeneo ambayo fedha hizo zinaweza kukusanywa na zikafanya kazi vizuri, kwa kweli wale wajasiriamali ambao sasa wamekuwa wazabuni wa halmashauri, walipwe fedha zao. Wanavyochelewesha, maana yake aliyekuwa mamantilie amekua sasa, maana ametoa huduma upande wa halmashauri; unataka umrejeshe tena kwenda mamantilie badala ya kuwa mzabuni. Pia, yule aliyekuwa babantilie vivyo hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuangalie namna ambayo halmashauri zetu zitaweka kipaumbele kwenye kuwalipa hawa wazabuni wazawa, lakini wakati huo huo watumishi. Haipendezi watumishi wanakuwa hawalipwi fedha zao, halafu wanaona huku na kule na kule, pesa zinaonekana zimeingia hapa, zimetokea hapa, zimeingia hapa, zimetokea pale. Wakati mwingine haya tunayoyalaumu yanasababishwa na mambo kama hayo.

Wakati mawazo haya yakitolewa, hili moja halipo kwenye sehemu ya haya ambayo yamependekezwa na Kamati, lakini ni jambo ambalo Serikali pengine wanatakiwa kwenda kulifanyia kazi waone namna bora ya kwenda nalo. Hii ni kwa sababu ile nia ya kugatua Madaraka, nadhani yanaitwa kugatua madaraka.

Maana nisije nikachanganya mambo hapa mbele watu wakasema sasa Mheshimiwa wewe si unasema tuongee Kiswahili fasaha? *(Kicheko)*

Basi kugatua yale Madaraka; ziko halmashauri ambazo zinaweza kufanya vizuri zaidi zikiachiwa kazi hiyo zifanye zenyewe, kwa sababu zinao uwezo wa kukusanya mapato na zinao uwezo wa kujiendesha kwa kutumia hayo mapato. Ule utaratibu wetu pengine unawafanya wasiweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi, zinaweza kutazamwa na zenyewe mkaona pengine kuanza na halmashauri hata mbili, tatu tuone zinafanyaje kazi. Halafu kadiri tunavyokwenda tunaweza kushangaa kwamba hizi halmashauri zimeweza kufanya vizuri, zikaupunguzia mzigo Serikali, na zile fedha zikaelekea kwenye maendeleo sehemu nyingine ambako halmashauri hizo pengine hazina uwezo wa kuleta maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naamini hayo yanaweza kutusaidia. Upande wa Serikali itatazama kama ni jambo linalowezekana, lakini ninaamini linawezekana, kwa sababu ni hoja tu ya kufanya maamuzi na kuanza kufikiri tofauti. Kwa nini nchi yetu ni nchi ambayo inaendelea? Ni kweli, lakini tuna miaka 60 sasa na tunasonga mbele. Kama hivyo ndivyo, lazima tufike mahali pa kujitathmini na wakati tukijitathmini, basi kuna mambo ambayo tunaweza kufikiri tofauti ili nchi yetu iweze kupiga hatua. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati ikihitimishwa hoja hapa, kuna mapendekezo ambayo yametolewa. Kwanza, ilikuwepo hoja kuhusu mahudhurio ya Waheshimiwa Mawaziri. Hili ni jambo ambalo nadhani limeshazungumzwa mara kadhaa hapa Bungeni, lakini sasa naona bado kuna changamoto, kwa sababu wakati mwingine vikao vinaitishwa na upande wa Serikali muda ambao ni wa Bunge na yote ni ya muhimu. Wakati mwingine sasa hivi na vikao vinafanyika kwa njia ya mtandao. Kwa hiyo, mwingine anaweza kuwa anafanya kikao, yupo hapa Dodoma, lakini ana kikao, kwa hiyo, kidogo tunapata hiyo changamoto.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo hili tumeshalizungumza leo siyo mara ya kwanza, ni mara nyingi sana.

Hata ambaye hayuko kwenye kikao anatumia nafasi hii sasa kwamba aliitwa kwenye simu. Watu lazima walipe kipaumbele Bunge. Ndiyo maana, kwa sababu hilo halikuwa jambo la siri, Mheshimiwa Rais alishaagiza kwa wazi kabisa, kipindi cha Bunge, Mawaziri wawe Bungeni, na Naibu Mawaziri wawe Bungeni, ambavyo wanakuwa hawapo, kwa sababu sasa pia sote tunajua ukishalisema jambo moja, mara nyingi sana na ukaona hakuna mabadiliko, maana yake aidha, ni namna unavyolisema au ni vile mtu ameona hakuna kitu unaweza kufanya hata asipofuata. *(Makofi)*

Sasa, kwa upande wa Bunge, kwa sababu huwa tunataka Serikali iwepo itusikilize tunapowashauri, pamoja na kwamba kuna utaratibu wa yale mawasiliano, lakini Wabunge ni wanadamu, wanatamani wasikilizwe na mhusika wakati wakitoa huo ushauri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa uko hapa umesikia haya na haya mambo yalishazungumzwa mara kadhaa, sasa, tusifike mahali ambapo Waziri atakuwa hayupo halafu tukaahirisha Bunge ili tumsubiri yeye aje, ili Bunge liweze kuendelea, tusifike huko. Tunatamani ile heshima ambayo tunaheshimiana mihimili iendelee kuwepo, lakini kila upande umheshimu mwenzake kwa muktadha huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, limetoka pendekezo hapa kuhusu siku ya taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwamba, tuingize kwenye kanuni. Sasa kwa sababu tumeshalifanya mara moja, na mwaka wa fedha huu, lakini mwaka unaokuja kwa maana ya 2025, tutakapolifanya tutaona sasa namna bora. Hata kama tunaweka kwenye kanuni, tuliweke kwa sura gani ili Wabunge wawe wanapata mrejesho ambao ni rahisi zaidi kwamba, maazimio yalikuwa haya, na Serikali imeweza kufanya kwa hatua gani? *(Makofi)*

Hata hivyo, katika utaratibu uliopo sasa siyo kwamba hatupati mrejesho, lakini tunapata mrejesho kwa maana ya zile Kamati zinazohusika, Wabunge wengine wanakuwa hawafahamu. Pia, wananchi kwa sababu haya wanakuwa wameyasikia, hayo mengine wanakuwa hawajapata nafasi ya kuyasikia kwamba, Serikali imetuambia nini? Kwa sababu, katika

hali ya kawaida, Serikali huwa inaleta taarifa ya wamefikia wapi na utekelezaji? Ndiyo utaratibu uliopo hata sasa.

Tuliweka huu utaratibu wa kuleta ili Wenyeviti wa hizi Kamati waje waseme hapa, kwa sababu wanakuwa wamesema hapa haya maazimio. Kwa hiyo, tutalitazama tuone namna bora ya kulifanya hili pendekezo ambalo ameleta Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo amelizungumza ni kuhusu ile 10% ambayo Serikali baada ya kuona kuna changamoto nyingi na nyingine zilibainishwa na *CAG* katika mwaka ule mwingine kabla ya huu ambao tunautazama sasa wa 2022/2023. Ilikuwa mwaka 2021/2022 changamoto walizokuwa wamezisema zikasabbisha Serikali kusitisha utoaji wa hii mikopo ili waweze kutafuta njia bora zaidi ambayo itasababisha vikundi vinavyopewa visiwe vikundi hewa na wakati huo huo waweze kurejesha yale marejesho ili kutoa fursa kwa watu wengine pia kufaidika na mikopo hii.

Sasa, katika hayo maboresho, wakati akitoa ufafanuzi Mheshimiwa Mwenyekiti akasema kwamba, Kamati hizi zimeshirikishwa kwa ngazi kwa maana ya kwamba, sasa hatua zinazoenda kuchukuliwa ndiyo Kamati zimeshirikishwa na kwamba, mwanzoni hazikushirikishwa.

Nafikiri ufafanuzi hapa ni kwamba, ni sawa kwa upande wa Serikali kwa sababu hili ni jambo la utendaji. Kwa hiyo haikuwa lazima Waheshimiwa Wabunge kushirikishwa katika ngazi hii. Walivyotushirikisha ngazi hii, wanataka ushauri kutoka kwetu. Sasa Mheshimiwa alisema, wakati mwingine unaweza ukashauri halafu ndiyo kama hivyo, Bunge tunasema, wao wanaamua tu kwenda, akasema wakati mwingine wanaenda kibabe, siyo?

Waheshimiwa Wabunge, uhalisia ni kwamba, namna Bunge linavyofanya kazi na Serikali kuna muda ambao Bunge linaishauri Serikali na kuna muda ambao Bunge linaisimamia Serikali. Katika hoja kama hii, na kwa sababu haijaja hapa ndani, wao waliwapelekea hawa Kamati kama vile wawe wanafahamu, waliwapelekea ili wafahamu. Hata kwamba, walikuwa wanataka ushauri, sina uhakika sana, nadhani walipeleka ili tu wawe

wanajua kama ambavyo Serikali inaweza kusema tuna semina kwa ajili ya jambo hili kama ambavyo nitaeleza hivi punde kuhusu semina ya kesho. Kimsingi siyo kwamba, Bunge linapaswa kuchukua maamuzi yoyote kwenye jambo kama hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa ngazi hii ni ushauri. Serikali kwenye hoja ya ushauri inaweza ikachukua ama ikakataa. Jambo ambalo haiwezi kukataa ni maazimio ya Bunge kama haya tuliyoazimia. Wakati wa ushauri inaweza ikachukua ama ikakataa. Ikikataa wakati wa kuisimamia, ikionekana jambo ambalo Bunge pengine huko nyuma liliwahi kushauri na wao wakakiuka, pale sasa ndiyo inakuwa ni kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeona nitoe huo ufafanuzi kwa maana ya ufafanuzi wa ziada alioutoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI kwamba, wanachukua, nadhani alitaja baadhi ya zile halmashauri na akataja kwa namba kwamba, idadi hii wataenda kwa huu utaratibu mpya; idadi nyingine wataenda kwa namna ambavyo wao wamejipanga. Kwa ngazi hii, kama Bunge kwa kweli hatuna uwezo wa kuzuia Serikali kwamba msitoe ama mtoe kwa sababu haijaja hapa ndani kwamba tunaweza kutoa hayo maazimio.

Wao walikuwa wanafanya hivyo kama vile kushirikisha kwamba na ninyi mfahamu tunachotaka kufanya. Kwa hiyo, wanaweza kuendelea vile ambavyo wao wamejipanga. Hoja ni kwamba jambo liende heri, na zile changamoto zilizokuwepo zisiwepo tena. Kama zikiendelea sasa uzuri itakuwa tu ni mzunguko wa mwaka mmoja, taarifa zitakuja na tutajua kama tunaenda vizuri ama hatuendi sawasawa. Katika ngazi hiyo tutaweza kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, hakuna hoja hapo ya unyonge wa upande wowote. Kila mmoja Katiba imempa kipindi chake cha kushika mpini na kipindi chake cha kushika makali.

Kwa hiyo, kwa wakati huu kwa ngazi hii kwa kile ambacho Serikali ilikileta wakati ambayo ni nje ya Bunge kwa zile Kamati tatu ambazo waliwaita, kwa kweli waliwaita ili na ninyi mjue tu kinachoendelea, lakini kwa maana ya wao kuendelea na utekelezaji, ni mamlaka yao, kwa sababu ni suala la utekelezaji.

Sisi tutawasimamia, ikiwa jambo hilo litaenda vizuri tutawapongeza. Ikiwa halikwenda sawa tutawasimamia na tutatoa maagizo wakati huo ambao tutaazimia kama wameshaanza kulifanyia kazi na halikwenda sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, baada yakusema hayo, nimeletewa ombi hapa kwamba nifafanue kuhusu kesho kitakachosomwa humu Bungeni na kile tutakachoenda kukifanya nje ya Bunge, baada ya lile tangazo nililotangaza kuhusu semina muhimu ya kesho, kwamba Wabunge wote ni muhimu tuwepo.

Semina ya kesho inahusu Dira ya Maendeleo. Hapa imeandikwa Dira ya Maendeleo, lakini nadhani kwenye hoja ya majina huko bado na wenyewe wanapokea mawazo kama iitwe Dira ya Maendeleo ya Taifa ama iitwe tu Dira ya Taifa. Kwa hiyo, vyovyote vile.

Waheshimiwa Wabunge, hii semina inahusu Dira ya Taifa ya Mwaka 2050. Uhusiano wake na kile tutakachokisoma hapa asubuhi ni kwamba, kinaweza kukupatia picha ukatoe mawazo gani kule, kipi kiendelee, kipi unaona vipi, hapana. Siyo kwamba ni vitu vinavyofanana kwa wakati huo, havifanani kwa sababu ile nyingine ni dira ambayo utekelezaji wake unaanza 2025 – 2050.

Kile ambacho kitasomwa hapa kesho ni yale mapendekezo ambayo yametajwa kwenye Kanuni yetu ya 113, ambapo Serikali inatarajiwa kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa muda mfupi, kwa maana ya mwaka mmoja kwa sababu wa muda mrefu tulishaupitisha. Kwa hiyo, ule mwaka wa fedha unaokuja mambo yatakayoelezwa kesho hapa ndiyo tunayoyatarajia. Ndiyo maana tulisisitiza kwamba, ni muhimu watu kuipitia kanuni hii kwa sababu kesho tutasikia mapendekezo ya vyanzo vipya vya mapato. Kwa hiyo, na wewe utaje vyako ulivyoviona huko ambavyo unaona Serikali haijaviona. Pia, wanakuja na mwongozo ambao utakuwa unatupatia picha ni vipaumbele gani vitakuwepo katika bajeti inayokuja? *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa haya yote ndiyo tutakayoyasema humu ndani na hili jambo litatuchukua siku tano tukiwa tunalijadili, ndiyo kanuni zetu zinataka hivyo. Kwa nini? Ngazi hii pia tunatoa ushauri

kwa Serikali. Wao wanaleta kwetu mapendekezo, tukishayapitia yale tunawashauri, wanachukua ule ushauri. Watakapoondoka nao kuna mengine watayachukua kwa sababu ni ushauri, mengine watayaacha, lakini tutakutana tena baadaye kwenye kuisimamia Serikali.

Kwa hiyo, hayo mambo mawili ni muhimu tuelewe hivyo. Ile tunayoshirikiswa kesho, tunashirikishwa kama wawakilishi wa wananchi kwa sababu wananchi wenzetu katika ngazi mbalimbali wamepata fursa ya kuongea na hao wataalamu wanaoandaa hii dira. Sisi kama Wabunge baadhi yetu tumeshiriki huko kwenye majimbo yetu, lakini baadhi yetu hawajapata nafasi ya kushiriki kwenye majimbo yetu.

Kesho ni nafasi ya wawakilishi wa wananchi kushiriki kama wadau, siyo watu ambao tunafanya maamuzi kesho, hapana. Kushiriki kama wadau, kutoa maoni yetu watatusikiliza na wao watatueleza waliyoyakusanya huko, basi tunaweza kusonga mbele kwa pamoja kama Taifa, ili nasi kama wawakilishi kwa sababu hili ni jambo la kihistoria na ndiyo maana nimesisitiza ni muhimu sote tuwepo.

*Insha Allah,* Mwenyezi Mungu atuweke hiyo 2050 tuseme tulikuwepo wakati wa dira hii. Pia kama ukitangulia utakuwa umeweka historia bila shaka. Naona kuna Mbunge anacheka, lakini ndiyo huo uhalisia. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.37 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 1 Novemba, 2024 Saa 3.00 Asubuhi)*